


**YANIPASA**

*Nifanye nini*

*nipate*



**KUOKOKA**



**Shemeji Melayeki**

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

## **Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?**

**©2021**

**Shemeji Melayeki**

**Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili bila ruhusa ya maandishi ya mwandishi isipokuwa kwa nukuu mbalimbali na matumizi ya kufundishia.**

SIMU: +255 714 548 565

+255 763 965 297

Email: *shemeji.melayeki@gmail.com*

YouTube: *Shemeji Melayeki*

Instagram: *apostle\_shemeji\_melayeki*

Twitter: *@melayeki*

Facebook: *Ap Shemeji Melayeki*

**ISBN - 978-9976-5427-8-3**

Kimepigwa Chapa Na: **CLIMAX SOLUTIONS – ARUSHA**

**+255 658 288 054**

**+255 687 699 862**

## **YALIYOMO**

TABARUKU .....	v
SHUKRANI.....	vi
UTANGULIZI .....	vii
SURA YA 1 .....	1
<i>YESU ALISEMA TUHUBIRI NINI?</i> .....	1
SURA YA 2 .....	11
<i>UJUMBE NI MMOJA.....</i>	11
SURA YA 3 .....	35
<i>TUBUNI MREJEE.....</i>	35
SURA YA 4 .....	46
<i>KUHUSU KUHESABIWA HAKI .....</i>	46
SURA YA 5 .....	69
<i>KUHUSU MATENDO MEMA .....</i>	69
SURA YA 6 .....	82
<i>KATIKA KRISTO TUNAO (SIYO TUTAPATA) MSAMAHA WA DHAMBI .....</i>	82
SURA YA 7 .....	86
<i>NIKUSANYIENI WACHA MUNGU WANGU; WALIOFANYA AGANO NAMI KWA DHABIHU.....</i>	86
SURA YA 8 .....	97
<i>TUKIZIUNGAMA DHAMBI ZETU.....</i>	97

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

SURA YA 9 .....	133
<i>KAMA TUKIFANYA DHAMBI KUSUDI</i> .....	133
SURA YA 10 .....	142
<i>ISIWE NIKIISHA KUWAHUBIRI WENGINE, MWENYEWE NIWE MTU WA KUKATALIWA</i> .....	142
SURA YA 11 .....	157
<i>HAIWEZEKANI KUWAFANYA UPYA TENA HATA WAKATUBU</i> .....	157
SURA YA 12 .....	193
<i>NA HUO UTAKATIFU, AMBAO HAPANA MTU ATAKAYEMWONA BWANA ASIPOKUWA NAO</i> .....	193
SURA YA 13 .....	203
<i>HALI YAO YA MWISHO IMEKUWA MBAYA KULIKO ILE YA KWANZA</i> .....	203
SURA YA 14 .....	214
<i>YANIPASA NIFANYE NINI NIPATE KUOKOKA?</i> .....	214



*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

## TABARUKU



Kwa jamii ya waaminio wenyewe kiu ya kumjua Mungu katika uhalisia wake, hasa wale waliokuwa wameshikilia ufahamu wa Mungu usio sawa juu ya Mungu na wokovu wake.

Kwa wachungaji na wanafunzi walioko chini ya huduma ya Globala Family Gatherings ambao wamekuwa wakinisaidia kwa sehemu kubwa kujibu maswali ya wanafunzi wengi walioko chini yao ambao kwa sababu ya idadi nisingeweza kumhudumia mmoja mmoja.



## SHUKRANI



**K**wa Mungu ambaye ni Baba wa roho zetu na aliyetuzaa katika ufuluo wa Kristo, nakushukuru kwa utulivu wakati wa kukiandaa kitabu hiki.

Kwa familia yangu, mara nyangi nimekuwa macho usiku wakati wamelala, kwa utulivu mkubwa walionipa. Mke wangu Neema amekuwa msaada mkubwa katika kuhakikisha nafanikisha uandaaji wa kitabu hiki.

Kwa timu ya watu waliojitolea kujifunza kupitia kwangu kwenye huduma ya Global Family Gatherings, madarasa ya God's Standards, wachungaji wetu na wengine wengi tunaowafikia kwa njia ya mitandao ya kijamii, wamekuwa sababu ya kunifanya nijitume zaidi.

Kwa wadau wanaofanya huduma pamoja na mimi kwa njia ya sadaka zao ili kuhakikisha kazi hii haikwami, wamekuwa waaminifu kwa rasilimali zao ili kweli hii ienee zaidi.

Mchungaji Musa Joseph aliyechukua maandishi yote niliyokuwa naandika kila siku mtandaoni maana ndiyo yaliyotumika kuandaa kitabu hiki. Kazi yake ni njema sana.

## UTANGULIZI



**W**atu wengi wanaosema "wameokoka" aidha wamesingiziwa kuwa wameokoka au wanajidanganya wameokoka au hawajaambiwa "KWELI" kwamba wameokoka kutoka kwenye nini ama ile sala ya toba waliyoongozwa pengine ndiyo wanafikiri ni wokovu!

Kwa kutokujua hili wamekuwa waathirika wa vitu vyatya ajabu na huku wakifanya "Wokovu" uonekane ni dini tu au mtindo wa kuitana unaotokana na kuwa au kuhamia "dhehebu" fulani. Ndiyo maana kuna baadhi ya watu wanakuuliza "Umeokoka? Ukisema ndiyo, wanaongeza "Unasali wapi?" Ukijibu dhehebu fulani watakuambia aidha hujaokoka "vizuri" au hamia dhehebu letu ili uokoke vizuri. Je, kuna uhusiano wowote wa wokovu na madhehebu fulani fulani. Watu wengi hawajui kabisa maana ya wokovu. Wengine hawajui kabisa wameokoka kutoka kwenye nini na sasa hivi wako kwenye nini? Siku hizi kila mtu anasema ameokoka na anaishi kwenye hofu ya mambo lukuki yaliyopita, yaliyopo na yajayo. Ndiyo maana mtu anaweza kukuambia nimeokoka au nimeamini. Muulize, "Unaamini nini?" Mwingine unamuuliza mtu "Umeokoka?" Anakujibu "Ndiyo" Ukizunguka ukamuuliza "Kwa hiyo utaenda mbinguni?"

Hapo kwanza anasita na anakula kamuda akiwazaaa ...  
Baadaye anakujibu "Sina uhakika" mwingine akanijibu  
"inategemea"

Nikauliza "Inategemea nini?"... Asilimia kubwa  
wakajibu "Inategemea watakufa wakati gani, yaani kabla  
ya kukata roho unatubu"

Nikauliza sasa "Ukiwa unasoma ujumbe kwenye simu  
yako kutoka kwa rafiki yako ukiwa ndani ya daladala  
huku hujaanza kutubu ghafla risasi ikapita kichwani  
paaah, Je, hapo hauendi mbinguni!?"

Akakaa, Kimya!.....

Nikauliza "Uliposema Umeokoka, Je, Umeokoka  
kutokana na nini?"

Ndiyo maana ni vyema upate utulivu, ukiwa na kalamu,  
daftari na Biblia yako tujifunza kuhusu wokovu kwa  
uchambuzi wa maandiko.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

# 1

SURA YA

**YESU ALISEMA TUHUBIRI NINI?**



**A** gizo kuu au Great Commission kama ambavyo wengi wamezoea kuita kwa kingereza ni mpango wa Mungu kuendeleza yale ambayo Yesu amefanya kwa ajili ya ulimwengu wote na kufundisha kwa wanafunzi wake ili kwamba nao wawafundishe watu wengine ambao nao watawafundisha watu wengine na hatimaye kila mtu kupata ujumbe uliokusudiwa. Agizo hili limewekwa wazi katika vitabu vinne vyta injili. Tuanze na Marko...  
**Marko 16:15-18**

**[15]Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, MKAIHUBIRI INJILI KWA KILA KIUMBE.**

**[16]Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa.**

**[17]Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya;**

**[18]watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya.**

**Mkaihubiri kwa kila kiumbi.** Mara nyingi watu huchanganya kuhubiri na kufundisha kama vile ni kama vitu viwili vinavyotofautiana kabisa. Lakini maneno yote mawili yanahusiana na kupeleka habari njema za upendo wa Mungu kwa watu. Ndiyo maana habari hiyo hiyo Mathayo anaita na KUWAFUNDISHA KUYASHIKA YOTE NILIYOWAAMURU.

**Mathayo 28:18-20**

**[18]Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.**

**[19]Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa WANAFUNZI, MKIWABATIZA kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu;**

**[20]na KUWAFUNDISHA KUYASHIKA YOTE NILIYOWAAMURU ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.**

Maneno kila kiumbe pia yamechukuliwa tofauti, wengine wakafikiri kila kiumbe (zaidi ya mwanadamu) anahitaji Injili. Lakini si kweli kabisa. Yesu alikuja kwa ajili ya watu. Mathayo 1:21

*[21]Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao.*

Ndiyo maana maelezo ya Mathayo ya Agizo Kuu anasema BASI, ENENDENI, MKAWAFANYE MATAIFA YOTE KUWA WANAFUNZI. Mataifa ni watu siyo mbuzi na kondoo.

Je, haya yote ni yapi?

Agizo hili limeandikwa pia na Luka. Na Luka atatuonyesha haya yote. Angalia Luka 24:46-47

*[46]Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu;*

*[47]na kwamba mataifa yote  
WATAHUBIRIWA kwa JINA LAKE lake  
habari ya TOBA na ONDOLEO la DHAMBI,  
kuanza tangu Yerusalemu.*

Kwa hiyo WANAFUNZI hufundishwa Kristo ameteswa na kufufuka siku ya tatu na kwa sababu hiyo wapokee (watubu) na kuamini juu ya ONDOLEO la DHAMBI zao kwa KUFA NA KUFUFUKA kwa Yesu Kristo.

Hiki ndicho alichosema malaika na si kitu kingine..

Mathayo 1:21

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

**[21]Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina  
lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa  
watu wake na dhambi zao.**

Ndicho pia alicoandika Yohana kwa habari ya Agizo  
Kuu. Yohana 20:21-23

**[21]Basi Yesu akawaambia tena, Amani iwe  
kwenu; kama Baba alivyonituma mimi, mimi  
nami NAWAPELEKA NINYI.**

**[22]Naye akiisha kusema hayo, akawavuvia,  
akawaambia, Pokeeni Roho Mtakatifu.**

**[23]Wo wote MTAKAOWAONDOLEA  
DHAMBI, WAMEONDOLEWA; na wo wote  
MTAKAOWAFUNGIA dhambi,  
WAMEFUNGIWA.**

Watu wengine wakisoma hivi wanadhani kwamba Yesu alimaanisha kuwa unakwenda tu kwa watu halafu unawaondolea dhambi labda kwa sababu zako mwenyewe na wengine unaamua kuwaambia mmefungiwa dhambi zenu. Lakini sicho alichomaanisha Bwana wetu.

Haya ni matokeo ya kuhubiri injili. ANAYEPOKEA INJILI ANAPOKEA ONDOLEO LA DHAMBI, LAKINI ANAYEKATAA INJILI HUYO DHAMBI YAKE INAKAA. ANGALIA. Marko alivyosema Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa.

Yohana pia ameandika.. Yohana 3:16-18

**[16]Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda  
ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili**

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

*kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*

*[17]Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye.*

*[18]Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu.*

Kwa hiyo WATU WANAAMINI KWA KUHUBIRIWA INJILI NA WANAHUKUMIWA KWA KUKATAA INJILI. Turudi kuangalia juu ya KUWAONDOLEA DHAMBI NA KUWAFUNGIA DHAMBI.

Wito mkuu umeandikwa kwa namna tofauti na Mathayo, Marko, Luka na Yohana. Ujumbe wao ni mmoja lakin i lughazimetofautiana.

Angalia *Mathayo 28:18-20*

*[18] Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.*

*[19] Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu;*

*[20] na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.*

Tena Angalia, **Marko 16:15-18**

[15] *Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.*

[16] *Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa.*

[17] *Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya;*

[18] *watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya.*

Luka naye... **Luka 24:44-49**

[44] *Kisha akawaambia, Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi.*

[45] *Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko.*

[46] *Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu;*

[47] *na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu.*

[48] *Nanyi ndinyi mashahidi wa mambo haya.*

[49] *Na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu.*

Yohana naye... ***Yohana 20:21-23***

**[21] Basi Yesu akawaambia tena, Amani iwe kwenu; kama Baba alivyonituma mimi, mimi nami nawapeleka ninyi.**

**[22] Naye akiisha kusema hayo, akawavuvia, akawaambia, Pokeeni Roho Mtakatifu.**

**[23] Wo wote mtakaowaondolea dhambi, wameondolewa; na wo wote mtakaowafungia dhambi, wamefungiwa.**

Sasa shida yetu kwa leo ni KUWAFUNGULIA DHAMBI NA KUWAFUNGIA DHAMBI.

Mathayo hajataja kabisa swala la dhambi... amesema tu kuwafanya wanafunzi kwa kuwafundisha...

Marko amegawa aina 2 za watu... AAMINIYE vs ASIYEAMINI.

(Kwa hapa tunajua AAMINIYE ameondolewa dhambi ASIYEAMINI dhambi yake inakaa kwa sababu hajaamini).

Luka pia... kasema MATAIFA YOTE WATAHUBIRIWA HABARI ZA TOBA NA ONDOLEO LA DHAMBI. Ni dhahiri ya kwamba siyo WOTE WALIAMINI. Kitabu cha Matendo ya mitume ni ushahidi mkubwa kwenye hili. Aliyeamini tu ndiye anapokea ONDOLEO LA DHAMBI. Mpaka hapa inaonekana ukihubiri INJILI... watu wakisikia... kuna uwezekano wa kutokea makundi mawili.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

1. WALIOAMINI = wanapokea ondoleo la dhambi... yaani kwa kuhubiri kwako umewafungulia dhambi zao.
2. WASIOAMINI = waliokataa Injili... hawa hawawezi kuondolewa dhambi maana wamekataa ondoleo... hawa dhambi zao zinakaa... hata usipowaambia "Bakini na dhambi zenu" ni automatic. Hawa wamefungiwa. Kwa sababu hawajaamini.

Yohana huyu huyu aliandika vizuri tu kwenye ***Yohana 3:16-18***

*[16] Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*

*[17] Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye.*

*[18] Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu.*

Angalia Yohana anavyoandika...

AMWAMINIYE asipotee... bali awe na uzima wa milele.

ASIYEAMINI amepotea... maana hana uzima wa milele.

AMWAMINIYE hahukumiwi...

ASIYEAMINI amekwisha kuhukumiwa...

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Hakuna namna yoyote ya kuondoa dhambi za watu bila kuwahubiria ONDOLEO LA DHAMBI kwa kazi ya ukombozi wa Kristo Yesu. Lakini wakati huo huo wengine watabaki na dhambi zao kwa kutokuamini... wasioamini wamekubali hukumu... ya kuwa wao wamepotea, wao wana dhambi na wanaishi katika dhambi.

Ukisoma kwa ujumla wake GREAT COMMISSION kwa Mathayo, Marko, Luka na Yohana utagundua... waliagizwa na Yesu kuhubiri, kufundisha au kutengeneza wanafunzi, kwa kuhubiri/kufundisha kufa na kufufuka kwake... na ahadi ni kwamba watapokea ondoleo la dhambi wanapoamini.... lakini si WOTE WATAKAOAMINI, ukweli ni kwamba wengine waliwatesa mitume na kuwaaua.

Jambo la mwisho kwenye hili ni kwamba... hakuna sehemu yoyote mitume walikwenda na kusema kwa MANENO (VERBALLY) "WEWE FULANI NA FULANI NATOA DHAMBI YAKO, WEWE FULANI NA FULANI NAWAFUNGIA", kuanzia Matendo ya mitume mpaka Ufunuo, hakuna kitu kama hicho.

Na bila shaka walitii agizo la Bwana wetu Yesu Kristo.

Walihubiri Injili tu. Na kwa sababu hiyo walitimiza ***Yohana 20:23...***

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Kwa hiyo, Injili ni mahubiri yahusuyo habari za Msamaha wa dhambi na kila mara hayo yanapowekwa wazi wengine hupokea na wengine hukataa.

# 2

SURA YA

## *UJUMBE NI MMOJA*



**I**njili ni ujumbe mmoja wa Mungu unaozungumzia WOKOVU kwa wanadamu. Ni ujumbe usiobadilika kulingana na aina ya watu wasikiao au mazingira yaliyopo.

Hauna sura tofauti mbele ya masikini na tajiri, haina tofauti mbele ya wasomi na wasio na elimu, mbele ya akina baba na akina mama. Hauangalii rangi au jinsia ya mtu... ujumbe ule ule unampa balozi wa nyumba kumi na raisi wa nchi... ndio huo huo utampa mwanasiasa na mtu asiye na cheo chochote.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Ukishabadilika... huo siyo ujumbe wa Mungu na kwa maana hiyo siyo Injili.

Angalia... Paulo anasema jinsi alivyofanya alipokuwa KORINTHO... **1 Wakorintho 2:1-2**

**[1] Basi, ndugu zangu, mimi nilipokuja kwenu, sikuja niwahubiri siri ya Mungu kwa ufasaha wa maneno, wala kwa hekima.**

**[2] Maana naliazimu nisijue neno lo lote kwenu ila Yesu Kristo, naye amesulubiwa.**

Paulo hakutaka azungumzie kitu kingine chochote kama injili ijapokuwa kuna mambo mengi huko Korintho ila alikomaa na Yesu Kristo aliyesulubiwa.

Petro mbele ya WATU WA AINA MBALIMBALI...

**Matendo ya Mitume 2:5,32,38-39,41**

**[5] Na walikuwako Yerusalemu Wayahudi wakikaa, watu watauwa, watu wa kila taifa chini ya mbingu.**

**[32] Yesu huyo Mungu alimfufua, na sisi sote tu mashahidi wake.**

**[38] Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.**

**[39] Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio**

*mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.*

*[41] Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu.*

Petro hakusema kwa sababu watu hawa ni jamii mbalimbali ngoja nitafute mambo fulani ya kusema ila alichambua maandiko akionyesha kuwa Kristo alisulubiwa, akafa na akafufuka na kwa ajili hiyo wapate kutubu (kumgeukia) waokolewe.

Petro mbele ya HEKALU, hakujifanya kusema Aah, hawa watu wanasomaga Torati na Manabii watakuwa wanaelewa. Hapana. Alihubiri kitu alichohubiri Matendo ya mitume 2.

Angalia... *Matendo ya Mitume 3:18-24*

*[18] Lakini mambo yale aliyohubiri Mungu tangu zamani kwa kinywa cha manabii wake wote, ya kwamba Kristo wake atateswa, ameyatimiza hivyo.*

*[19] Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana;*

*[20] apate kumtuma Kristo Yesu mliyewekewa tangu zamani;*

*[21] ambaye ilimpasa kupokewa mbinguni hata zije zamani za kufanywa upya vitu vyote,*

*zilizonenwa na Mungu kwa kinywa cha manabii  
wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu.*

*[22] Kwa maana Musa kweli alisema ya  
kwamba, Bwana Mungu wenu atawainulieni  
nabii, katika ndugu zenu, kama mimi; msikieni  
yeye katika mambo yote atakayonena nanyi.*

*[23] Na itakuwa ya kwamba kila mtu  
asiyemsikiliza nabii huyo ataangamizwa na  
kutengwa na watu wake.*

*[24] Naam, na manabii wote tangu Samweli na  
wale waliokuja baada yake, wote walionena,  
walihubiri habari za siku hizi.*

KUFA NA KUFUFUKA KWAKE NA MATOKEO YA  
KUAMINI HILI TU...

Alipokuwa mbele ya BARAZA... mbele ya watu "wakubwa" hakuchapia au kuleta ujumbe mpya bali alikomaa na Habari ile ile... *Matendo ya Mitume 4:8-12*

*[8] Ndipo Petro, akijaa Roho Mtakatifu,  
akawaambia, Enyi wakubwa wa watu na wazee  
wa Israeli,*

*[9] kama tukiulizwa leo habari ya jambo jema  
alilofanyiwa yule mtu dhaifu, jinsi  
alivyoponywa,*

*[10] jueni ninyi nyote na watu wote wa Israeli  
ya kuwa kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti,*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

*ambaye ninyi mlimsulibisha, na Mungu akamfufua katika wafu, kwa jina hilo mtu huyu anasimama ali mzima mbele yenu.*

*[11] Yeye ndiye jiwe lile lililodharauliwa na ninyi waashi, nalo limewekwa kuwa jiwe kuu la pembeni.*

*[12] Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.*

Ni kitu kile kile... WOKOVU KATIKA JINA LA YESU KRISTO (KUFA NA KUFUFUKA KWAKE). Wokovu huo ni katika dhambi (Mathayo 1:21).

Filipo mbele ya towashi mtu mwenye CHEO... hakuanza kumsifia wala kumpamba... alianza kumhubiri KRISTO...

Angalia *Matendo ya Mitume 8:26-35*

*[26] Malaika wa Bwana akasema na Filipo, akamwambia, Ondoka ukaende upande wa kusini hata njia ile itelemkayo kutoka Yerusalemu kwenda Gaza; nayo ni jangwa.*

*[27] Naye akaondoka, akaenda; mara akamwona mtu wa Kushi, towashi, mwenye mamlaka chini ya Kandake malkia wa Kushi,*

*aliyewekwa juu ya hazina yake yote; naye  
alikuwa amekwenda Yerusalem kuabudu,*

*[28] akawa akirejea, ameketi garini mwake  
akisoma chuo cha nabii Isaya.*

*[29] Roho akamwambia Filipo, Sogea karibu na  
gari hili, ukashikamane nalo.*

*[30] Basi Filipo akaenda mbio, akamsikia  
anasoma chuo cha nabii Isaya; akanena, Je!  
Yamekuelea haya unayosoma?*

*[31] Akasema, Nitawezaje kuelewa, mtu  
asiponiongoza? Akamsihi Filipo apande na  
kuketi pamoja naye.*

*[32] Na fungu la Maandiko alilokuwa akilisoma  
ni hili,*

*Aliongozwa kwenda machinjoni kama kondoo,  
Na kama vile mwana-kondoo alivyo kimya  
mbele yake amkataye manyoya,*

*Vivyo hivyo yeye naye hafunui kinywa chake.*

*[33] Katika kujidhili kwake hukumu yake  
iliondolewa.*

*Ni nani atakayeeleza kizazi chake?*

*Kwa maana uzima wake umeondolewa katika  
nchi.*

*[34] Yule towashi akamjibu Filipo, akasema,  
Nakuomba, nabii huyu; asema maneno haya  
kwa habari ya nani; ni habari zake mwenyewe  
au za mtu mwingine?*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

*[35] Filipo akafunua kinywa chake, naye,  
akianza kwa andiko lilo hilo, akamhubiri  
habari njema za Yesu.*

HABARI NJEMA ZA YESU SIYO KITU KINGINE  
BALI NI KUFA NA KUFUFUKA KWAKE NA  
MATOKEO YAKE KWA MWANADAMU, NA  
WAKAAMINI.

Petro mbele ya Kornelio, afisa wa jeshi. Hakuanza kubwabwaja na kutunga mambo ya kusema, hata kama afisa ana maono kama yote, anaongea na malaika. AKAKOMAA NA UJUMBE ULE ULE. Siyo unakutana na mtu anakwambia jana niliambiwa mtakuja kwenye maono unaanza kumwomba yeye ndo akuhubirie. Wewe hubiri wala usibadili ujumbe. Unaweza kuwa na maono na hujaamini.

Angalia Petro alichofanya, Matendo ya Mitume 10:1-2,34-44

*[1] Palikuwa na mtu Kaisaria, jina lake  
Kornelio, akida wa kikosi kilichoitwa Kiitalia,  
[2] mtu mtauwa, mchaji wa Mungu, yeye na  
nyumba yake yote, naye alikuwa akiwapa watu  
sadaka nyingi, na kumwomba Mungu daima.*

- [34] *Petro akafumbua kinywa chake, akasema, Hakika natambua ya kuwa Mungu hana upendeleo;*
- [35] *bali katika kila taifa mtu amchaye na kutenda haki hukubaliwa na yeye.*
- [36] *Neno lile alilowapelekea wana wa Israeli akihubiri habari njema ya amani kwa Yesu Kristo (ndiye Bwana wa wote),*
- [37] *jambo lile ninyi mmelijua, lililoenea katika Uyahudi wote likianzia Galilaya, baada ya ubatizo aliouhubiri Yohana;*
- [38] *habari za Yesu wa Nazareti, jinsi Mungu alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu naye akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na Ibilisi; kwa maana Mungu alikuwa pamoja naye.*
- [39] *Nasi tu mashahidi wa mambo yote aliyoyatenda katika nchi ya Wayahudi na katika Yerusalem; ambaye walimwua wakamtundika mtini.*
- [40] *Huyo Mungu alimfufua siku ya tatu, akamjalia kudhahirika,*
- [41] *si kwa watu wote, bali kwa mashahidi waliokuwa wamekwisha kuchaguliwa na Mungu, ndio sisi, tulio kula na kunywa pamoja*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

*naye baada ya kufufuka kwake kutoka kwa wafu.*

[42] *Akatuagiza tuwahubiri watu na kushuhudia ya kuwa huyu ndiye aliyeamriwa na Mungu awe Mhukumu wa walio hai na wafu.*

[43] *Huyo manabii wote humshuhudia, ya kwamba kwa jina lake kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi.*

[44] *Petro alipokuwa akisema maneno hayo Roho Mtakatifu akawashukia wote waliolisikia lile neno.*

Alihubiri toba iletayo ondoleo la dhambi na wakajazwa na Roho Mtakatifu.

Fikiria kama angebadili ujumbe...

Paulo alienda mji wenye watu wenye elimu zao, za dini tofauti tofauti, mji uliojaa sanamu na masinagogi. UJUMBE WAKE AKAUVUTA KULE KULE. Hakuanza na HASARA 50 ZA KUABUDU SANAMU (hili siyo fundisho la Kristo nimetoa mfano tu)... BALI ALIMLETA KRISTO KWENYE MWANGA.

Angalia Matendo ya Mitume 17:16-32

[16] *Paulo alipokuwa akiwangojea huko Athene na kuona jinsi mji ule ulivyojaa sanamu, roho yake ilichukizwa sana ndani yake.*

[17] *Basi katika sinagogi akahojiana na Wayahudi na waliomcha Mungu, na wale waliokutana naye sokoni kila siku.*

[18] *Na baadhi ya Waepikureo na Wastoiko, wenye ujuzi, wakakutana naye. Wengine wakasema, Mpuzi huyu anataka kusema nini? Wengine walisema, Anaonekana kuwa mtangaza habari za miungu migeni, kwa maana alikuwa akihubiri habari za Yesu na ufuluo.*

[19] *Wakamshika, wakamchukua Areopago, wakisema, Je! Twaweza kujua maana ya elimu hii mpya unayoinena?*

[20] *Kwa maana unaleta mambo mageni masikioni mwetu, tutapenda kujua, basi, maana ya mambo haya.*

[21] *Kwa maana Waathene na wageni waliokaa huko walikuwa hawana nafasi kwa neno lo lote ila kutoa habari na kusikiliza habari za jambo jipya.*

[22] *Paulo akasimama katikati ya Areopago, akasema, Enyi watu wa Athene, katika mambo yote naona ya kuwa ninyi ni watu wa kutafakari sana mambo ya dini.*

[23] *Kwa sababu nilipokuwa nikipita huko na huko na kuyaona mambo ya ibada yenu, nalionna madhabahu iliyoandikwa maneno haya, KWA MUNGU ASIYEJULIKANA. Basi*

*mimi nawahubirini habari zake yeye ambaye  
ninyi mnamwabudu bila kumjua.*

[24] *Mungu aliyeufanya ulimwengu na vitu  
vyote vilivyomo, yeye, kwa kuwa ni Bwana wa  
mbingu na nchi, hakai katika hekalu  
zilizojengwa kwa mikono;*

[25] *wala hatumikiwi kwa mikono ya  
wanadamu kana kwamba anahitaji kitu cho  
chote; kwa maana ndiye anayewapa wote uzima  
na pumzi na vitu vyote.*

[26] *Naye alifanya kila taifa la wanadamu  
kutoka katika mmoja, wakae juu ya uso wa nchi  
yote, akiisha kuwawekea nyakati alizoziamuru  
tangu zamani, na mipaka ya makazi yao;*

[27] *ili wamtafute Mungu, ingawa ni kwa  
kupapasa-papasa, wakamwone, ijapokuwa hawi  
mbali na kila mmoja wetu.*

[28] *Kwa maana ndani yake yeye tunaishi,  
tunakwenda, na kuwa na uhai wetu. Kama vile  
mmoja wenu, mtunga mashairi alivyosema,  
Maana sisi sote tu wazao wake.*

[29] *Basi, kwa kuwa sisi tu wazao wa Mungu,  
haitupasi kudhani ya kuwa Uungu ni mfano wa  
dhahabu au fedha au jiwe, vitu vilivyochongwa  
kwa ustadi na akili za wanadamu.*

[30] *Basi, zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu.*

[31] *Kwa maana ameweuka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua; naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua katika wafu.*

[32] *Basi waliposikia habari za ufufuo wa wafu wengine walifanya dhihaka; wengine wakasema, Tutakusikiliza tena katika habari hiyo.*

ALIKOMAA NA KUFA NA KUFUFUKA KWA YESU HATA KAMA WALIBEZA... THE MESSAGE IS STILL THERE.

Ukiona kila aina ya watu unaokutana nao una jumbe ambazo ni tofauti tofauti za kuwapa ili WAFIT VIZURI KWENYE HUO UJUMBE... HIYO SIYO INJILI.

INJILI NI MAHUSUSI (SPECIFIC).

Injili ya kweli haichagui mtu!

Kama masikini wanaweza KUPOKEA na matajiri HAWAWEZI hiyo siyo Injili. Kama Watanzania wataelewa halafu ukifika kwa Wamarekani unabadilisha ujumbe hiyo siyo Injili. Kama UKIWAAMBIA

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

wanawake wanapokea lakini ikawabagua wanaume hiyo siyo Injili.

Kama mabosi wanaelewa lakini wafanyakazi hawaelewii hiyo siyo Injili. Kama mtu mwenye matendo mabaya atapokea lakini mwenye matendo mema ataona hayamhusu hiyo siyo Injili.

Injili ya kweli ni *CROSS CULTURAL, CROSS BORDERS, CROSS STATUSES.*

*ALL MEN NEED IT!*

*Now you can see if you're preaching the GOSPEL OF JESUS CHRIST OR GOSSIPING OF MEN...*

Mara kadhaa wakati tunaporekebisha mitazamo ya watu kwa habari ya Injili kuhusiana na MALI AU MASWALA YA UCHUMI mijadala inayokuja kwenye vichwa vya watu yanawafanya wafikiri tunapigia "chapuo" umasikini wa kipato au pengine tunapingana na utajiri wa kipato. Ukweli ni kwamba...

***UNAWEZA KUWA TAJIRI WA MALI ZA DUNIA NA UKAWA TAJIRI KATIKA MUNGU (KIUMBE KIPYA) NA UNAWEZA KUWA TAJIRI WA MALI ZA DUNIA NA UKAWA MASKINI KATIKA MUNGU.***

Vile vile;

***UNAWEZA KUWA MASKINI WA MALI ZA DUNIA NA UKAWA TAJIRI KATIKA MUNGU (KIUMBE KIPYA) LAKINI PIA UNAWEZA KUWA MASKINI***

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

**WA MALI NA BADO UKAWA MASKINI KATIKA MUNGU.**

Hii ni sawa na kusema TAJIRI NA MASKINI WOTE WANAWEZA KUWA WATAKATIFU.

Utajiri wala umaskini haumpunguzii wala kumwongezea mtu hali ya UTAKATIFU isipokuwa IMANI katika Kristo Yesu.

Angalia Paulo anachosema... *Warumi 15:24-26*

*[24] wakati wo wote nitakaosafiri kwenda Spania [nitakuja kwenu.] Kwa maana nataraji kuwaona ninyi katika kusafiri kwangu, na kusafirishwa nanyi, moyo wangu ushibe kwenu kidogo.*

*[25] Ila sasa ninakwenda Yerusalemu, nikiwahudumu watakatifu;*

*[26] maana imewapendeza watu wa Makedonia na Akaya kufanya changizo kwa ajili ya watakatifu huko Yerusalemu walio maskini.*

HAWA NI WATAKATIFU WALIO MASKINI  
WANAOKAA YERUSALEMU AMBAO  
WALIKUWA KWENYE LIST YA WATU  
WANAOPLEKEWA MISAADA KWA MKONO WA PAULO.

Hii ina maana mtu anaweza kuwa Mtakatifu na MASKINI pia. Na mitume mahali popote

hawakuwadharau watu kwa sababu ya vipato vyao badala yake waliwaelekeza mitume wengine wawajali watu wa aina hiyo badala ya kuwazodoa na kuwafanya kuwa wamepunguka katika Kristo. Hawakuwafanya wajione "second class" katika ufalme wa Mungu... angalia jinsi Paulo alivyoelekezwa na jinsi alivyotii agizo... *Wagalatia 2:10*

*[10] ila neno moja tu walitutakia, tuwakumbuke maskini; nami neno lilo hilo nalikuwa na bidii kulifanya.*

Paulo anasema kuwa alijali sana hili wala hakuwaona hawafai. Mbali na kuchangisha kwa ajili ya mahitaji yao, ye ye mwenyewe alikuwa mfano katika kuwasaidia watakatifu walio katika uhitaji..

Angalia anavyosema mwenyewe... *Matendo ya Mitume 20:33-35*

*[33] Sikutamani fedha wala dhahabu, wala mavazi ya mtu.*

*[34] Ninyi wenyewe mnajua ya kuwa mikono yangu hii imetumika kwa mahitaji yangu na ya wale waliokuwa pamoja nami.*

*[35] Katika mambo yote nimewaonyesha ya kuwa kwa kushika kazi hivi imewapasa kuwasaidia wanyonge, na kuyakumbuka maneno ya Bwana Yesu, jinsi alivyosema mwenyewe, Ni heri kutoa kuliko kupokea.*

Na hapa alikuwa anaongea na viongozi wa kanisa la Efeso Leo ungesema PASTORS AND LEADERS CONFERENCE MILETUS CHAPTER. Angalia

***Matendo ya Mitume 20:17***

***[17] Toka Mileto Paulo akatuma watu kwenda Efeso, akawaita wazee wa kanisa.***

Hivi unafikiri mtazamo wa watu (viongozi) waliohuduria kwenye kikao cha Mileto kingekuwaje?

Bila shaka wangefanya kazi kwa bidii na kuwajali waamini wahitaji na siyo kuwadharau.

Wakati huo Paulo anamwagiza Timotheo kwa habari ya matajiri... uwaagize WASIJIVUNE, WASIINUE VICHWA, WASIJIONE WAKO "SUPER" KWA SABABU WANA PESA NYINGI "MPUNGA"... WAWEKE MACHO KWA MUNGU ALIYEWAOKOA KWANI HAKUNA WOKOVU KATIKA MALI ZAO.

Angalia ***I Timotheo 6:17-19***

***[17] Walio matajiri wa ulimwengu wa sasa uwaagize wasijivune, wala wasiutumainie utajiri usio yakini, bali wamtumaini Mungu atupaye vitu vyote kwa wingi ili tuvitumie kwa furaha.***

- [18] *Watende mema, wawe matajiri kwa kutenda mema, wawe tayari kutoa mali zao, washirikiane na wengine kwa moyo;*  
[19] *huku wakijiwekea akiba iwe msingi mzuri kwa wakati ujao, ili wapate uzima ulio kweli kweli.*

Angalia anaita UTAJIRI USIO YAKINI "UNCERTAIN RICHES" Kwa hiyo havifai kutumainiwa... lakini zaidi wajifunze kutoa mali zao kwani huo ndiyo moyo wa Mungu waliupokea katika Kristo Yesu. Wao ni watu wema... WATENDE MEMA... huko ndiko kudhirisha utajiri halisi waliupokea kwa kuiamini INJILI.

Yakobo alionya kwa habari ya kuwafanya matajiri wajione ni CLASSY kwenye Makusanyiko ya Waamini kama ambavyo mara nyingi yanafanyika... ***Yakobo 2:1-4***

- [1] *Ndugu zangu, imani ya Bwana wetu Yesu Kristo, Bwana wa utukufu, msiwe nayo kwa kupendelea watu.*  
[2] *Maana akiingia katika sinagogi lenu mtu mwenye pete ya dhahabu na mavazi mazuri; kisha akiingia na maskini, mwenye mavazi mabovu;*  
[3] *nanyi mkimstahi yule aliyevaa mavazi mazuri, na kumwambia, Keti wewe hapa mahali*

*pazuri; na kumwambia yule maskini, Simama  
wewe pale, au keti miguuni pangu,  
[4] je! Hamkufanya hitilafu moyoni mwenu,  
mkawa waamuzi wenyen mawazo mabovu?*

Injili inachonga namna tunavyotazama watu, yaani kwa sababu mtu amepiga pamba kali, ana mshiko mrefu, au kaja na gari kali siyo KIGEZO cha kumpeleka siti ya mbele na kumwondoa mtu mwingine arudi nyuma. Kufanya hivyo ni KUWA MWAMUZI MWENYE MAWAZO MABOVU.

Mbali na kwamba Injili haiwapi matajiri nafasi ya kujiona bora kuliko maskini ndani ya Kristo, iko wazi pia kuwa haiwapi "heko" maskini wakomae na umaskini wao hasa kwa sababu ya uvivu na uzembe.

Jambo la kujua ni kwamba watakatifu waliokuwa wanapelekewa MISAADA hawakuwa watu wavivu ila kulikuwa na majanga yaliyowasababishia hiyo hali.

Mitume hawakufanya maombi ya kuwasaidia wapate FINANCIAL BREAKTHROUGH ila waliona kama ni fursa ya kudhihirisha upendo wa Kristo ulioko ndani yao. Hili ni jambo muhimu sana sisi kujifunza kama kanisa. Maana si wakati wote watu wanahitaji maombi kwenye mazingira ambayo tunaweza kujitoa na

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

kuwasaidia. Ikiwa uko katika nafasi ya kusaidia usipige kona nyingi... toa msaada ni jambo jema.

Angalia Yohana anavyoandika... ***1 Yohana 3:17-18***

***[17] Lakini mtu akiwa na riziki ya dunia, kisha akamwona ndugu yake ni mhitaji, akamzuilia huruma zake, je! Upendo wa Mungu wakaaje ndani yake huyo?***

***[18] Watoto wadogo, tusipende kwa neno, wala kwa ulimi, bali kwa tendo na kweli.***

Tena Yakobo anaeleza kuwa hii ndiyo njia ya kudhihirisha imani uliyonayo... UPENDO.

Imani ya kweli inazaa UPENDO hivyo KUWAJALI wengine... angalia ***Yakobo 2:14-17***

***[14] Ndugu zangu, yafaa nini, mtu akisema ya kwamba anayo imani, lakini hana matendo? Je! Ile imani yaweza kumwokoa?***

***[15] Ikiwa ndugu mwanamume au ndugu mwanamke yu uchi na kupungukiwa na riziki,***

***[16] na mtu wa kwenu akawaambia, Enendeni zenu kwa amani, mkaote moto na kushiba, lakini asiwape mahitaji ya mwili, yafaa nini?***

***[17] Vivyo hivyo na imani, isipokuwa ina matendo, imekufa nafsini mwake.***

Kufanya matendo mema ni udhihirisho wa uhai wa imani yako kwa Mungu. Mungu kwa kutupenda

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

ALITOA na hivyo ametupa AMRI (PATTERN) ya upendo. TUTOE TUKIWA NA CHA KUTOA.

Mbali na kwamba moyo wa utoaji umejaa katika watakatifu haiwafanyi baadhi ya watakatifu kukaa upande wa SISI WA KUSAIDIWA... ikiwa wana nafasi ya kufanya kazi, wafanye tena kwa bidii wala wasiwe wavivu nao pia wakiwaza KUDHIHIRISHA MATENDO YAO MEMA KWA KUTOA KWA WAHITAJI.

Paulo ameagiza haya mara nyingi tena kwa Yeye mwenyewe kuwa mfano.

*Matendo ya Mitume 20:33-35*

*[33] Sikutamani fedha wala dhahabu, wala mavazi ya mtu.*

*[34] Ninyi wenyewe mnajua ya kuwa mikono yangu hii imetumika kwa mahitaji yangu na ya wale waliokuwa pamoja nami.*

*[35] Katika mambo yote nimewaonyesha ya kuwa kwa kushika kazi hivi imewapasa kuwasaidia wanyonge, na kuyakumbuka maneno ya Bwana Yesu, jinsi alivyosema mwenyewe, Ni heri kutoa kuliko kupokea.*

KATIKA MAMBO YOTE NIMEWAONYESHA NAMNA... “THE PATTERN”.

Kwenye barua ya kwanza kwa Wathesalonike aliwaambia juu ya KUFANYA KAZI ZAO KWA BIDII. Angalia 1 Wathesalonike 4:9-12

- [9] *Katika habari ya upendano, hamna haja niwaandikie; maana ninyi wenyewe mmefundishwa na Mungu kupendana.*
- [10] *Kwa maana mnafanya neno hili kwa ndugu wote walio katika Makedonia yote. Lakini twawasihi, ndugu, mzidi sana.*
- [11] *Tena mjitätidi kutulia, na kutenda shughuli zenu, na kufanya kazi kwa mikono yenu wenyewe, kama tulivyowaagiza;*
- [12] *ili mwenende kwa adabu mbele yao walio nje, wala msiwe na haja ya kitu cho chote.*

Hili ni agizo aliloweka... Watulie, wafanye kazi zao wenyewe... Waache kurandaranda, maana yake mwishowe watakuwa WAHITAJI NA KISHA KUWALEMEA WENGINE. Kutowalemea wengine ni mwenendo wa upendo pia.

Lakini kwenye barua ya Pili alirudia tena (pengine hawa ndugu walikuwa na shida sana). Kwenye 2 Wathesalonike 3:7-8

- [7] *Mwajua wenyewe jinsi iwapasavyo kutufuata; kwa sababu hatukuenda bila utaratibu kwenu;*

*[8] wala hatukula chakula kwa mtu ye yote bure; bali kwa taabu na masumbufu, usiku na mchana tulitenda kazi, ili tusimleme mtu wa kwenu awaye yote.*

Tena kwa kukumbushia, mwenendo wao kama watumishi wa Mungu waliokuwa wakiwahudumia kanisa la Thesalonika kuwa "WALIPIGA KAZI"

Tena anawaonya tena... 2 *Wathesalonike 3:9-12*

*[9] Si kwamba hatuna amri, lakini makusudi tufanye nafsi zetu kuwa kielelezoo kwenu, mtufuate.*

*[10] Kwa kuwa hata wakati ule tulipokuwapo kwenu tuliwaagiza neno hili, kwamba ikiwa mtu hataki kufanya kazi, basi, asile chakula.*

*[11] Maana twasikia kwamba wako watu kwenu waendao bila utaratibu, hawana shughuli zao wenyewe, lakini wanajishughulisha na mambo ya wengine.*

*[12] Basi twawaagiza hao, na kuwaonya katika Bwana Yesu Kristo, watende kazi kwa utulivu na kula chakula chao wenyewe.*

Kwamba walitakiwa kupewa vya mwilini kwa sababu waliwapa vya rohoni bado alitaka kuwa mfano katika "KUCHAPA KAZI"

Kama mtu anaona kufanya kazi ni ngumu si azire na kula pia? Kwa nini awekeze katika kulemea wengine

wakati anaweza kufanya kazi na akapata na yeye cha kuwapa wengine?

Waache kuchunguza biashara za watu na za kwao zinakufa. Wafanye kazi kwa bidii. Watu watakaoonywa na wasionyeke kwenye hili eneo wasishirikiane nao ili wajitafakari. Siyo kuwachukia ila wapate KUTAFAKARI NJIA ZAO. Kanisa zima lionyeshe kупingana na mwenendo wao.

*Anaandika 2 Wathesalonike 3:13-15*

*[13] Lakini ninyi, ndugu, msikate tamaa katika kutenda mema.*

*[14] Na ikiwa mtu awaye yote halishiki neno letu la waraka huu, jihadharini na mtu huyo, wala msizungumze naye, apate kutahayari;*

*[15] lakini msimhesabu kuwa adui, bali mwonyeni kama ndugu.*

Wakati mwingine inaweza kwenda mbali, kwa sababu ya uvivu, kukosa mahitaji watu wanaweza kuwa wezi, wadokozi... na hii ni mbaya zaidi. Anawaambia tena...

*Waefeso 4:28*

*[28] Mwibaji asiibe tena; bali afadhali afanye juhudhi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe, apate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji.*

Wafanye kazi wahame kwenye WIZI HADI KWENYE UGAWAJI maana huwezi kutoa usicho kuwa nacho.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Nirudie kwa kusoma alichosema Paulo... **I**  
**Wathesalonike 4:11-12**

*[11] Tena mjütahidii kutulia, na kutenda shughuli zenu, na kufanya kazi kwa mikono yenu wenyewe, kama tulivyowaagiza;*

*[12] ili mwenende kwa adabu mbele yao walio nje, wala msiwe na haja ya kitu cho chote.*

Paulo anasema...

1. INALETA HESHIMA KWA WALE WALIOKO NJE (WASIOAMINI)
2. INASABABISHA KUSIWEPO NA MAHITAJI YASIYO YA LAZIMA
3. TUNAACCHA KULEMEA WENGINE.

**My brother and my sister, "MONEY IS MAN  
MADE, WORK TO GET THEM"**

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

# 3

SURA YA

**TUBUNI MREJEE**



Jambo la kwanza ni kwamba watu wengi wakisikia Neno TOBA AU KUTUBU akili zao zinawaza DHAMBI AU MAKOSA.

Pili, watu wengi wakisikia TOBA au KUTUBU moja kwa moja wanafikiri ni "maneno ya kunyenyeyekea unayoyasema baada ya kukosea"

Nenda ukatafute kwenye Biblia yako utashangaa sana. Sehemu rahisi kabisa ambayo napenda kufundishia TOBA AU KUTUBU ni mfano alioutoa Yesu. Mfano huu utatufundisha TOBA ilivyofanyika kwa vitendo zaidi. Angalia Mathayo 21:28-32

*[28] Lakini mwaonaje? Mtu mmoja alikuwa na wana wawili; akamwendea yule wa kwanza, akasema, Mwanangu, leo nenda kafanye kazi katika shamba la mizabibu.*

*[29] Akajibu akasema, Naenda, Bwana; asiende.*

*[30] Akamwendea yule wa pili, akasema vile vile. Naye akajibu akasema, Sitaki; baadaye akatubu, akaenda.*

*[31] Je! Katika hao wawili ni yupi aliyefanya mapenzi ya babaye? Wakamwambia, Ni yule wa pili. Basi Yesu akawaambia, Amin nawaambia, watoza ushuru na makahaba wanatangulia mbele yenu kuingia katika ufalme wa Mungu.*

*[32] Kwa sababu Yohana alikuja kwenu kwa njia ya haki, ninyi msimwamini; lakini watoza ushuru na makahaba walimwamini, nanyi hata mlipoona, hamkutubu baadaye, ili kumwamini.*

Jambo la kutazama hapa ni kwamba; aliyesema ANAENDA HAKWENDA... na aliyesema HATAKI, BAADAYE ALIENDA...

Hii inaonyesha ya kuwa TOBA SI MANENO BALI NI KUBADILISHA DIRECTION (MWELEKEO). Anawaambia HAMKUTUBU ili KUMWAMINI.

Tatizo hapa ni WALIPOSIKIA, HAWAKUBADILI FIKRA ZAO NA KUMPOKEA YESU (KUMWAMINI).

Kwenye Biblia yako utaona mara nyingi wameandika...  
Tubuni Mrejee...

Tubuni mkabatizwe...

Tubuni ufalme wa Mungu umekaribia...

Ukisoma habari za hao vijana WAWILI Kiswahili kinasema "BAADAYE AKATUBU AKAENDA" Version nyingi za Kingereza hutumia maneno "HE CHANGED HIS MIND/HEART AND WENT"

Hii ina maana alitafakari akaona Hii siyo njia sahihi akabadilika akafanya KINYUME na alivyowaza mwanzoni.

Kwa hiyo TOBA siyo MANENO... Ni hatua anayochukua mtu inayoonyesha badiliko la ndani... Ndiyo maana yule mwingine alisema *Naenda, Bwana; asiende*. Lakini yule mwingine alisema *Sitaki; baadaye akatubu, akaenda*. Sasa unawenza kuona toba ilivyofanyika. Hayakuwa maneno. Maana unawenza

kusema kwa mdomo kitu ambacho huamini moyoni.  
Yeye alibadili tu nia yake akaenda.

### ***It's a change of MIND and direction...***

Neno la asili ya Kigiriki lililotumika kama KUTUBU  
kwenye ***Mathayo 21:29*** ni “***metamellomai***” ambapo  
shina lake TOBA “***metanoea***” limeundwa na Maneno  
mawili “***meta***” na “***noeo***”

META ikiwa na maana ya "***baada ya***"

NOEO ikiwa na maana ya "***kujali, kutafakari***"

Kwa hiyo hili ni badiliko linalotoka ndani baada ya mtu  
kupata taarifa fulani na hivyo kuchukua hatua za  
makusudi. Kwa hiyo mtu anapokosea Jumatatu hadi  
Jumamosi ili JUMAPILI akatubu (kwa maana ya  
kwenda kukiri dhambi zake) huwa haelewi kabisa maana  
ya TOBA... Ndiyo imekuwa desturi tu za kawaida kwa  
sababu watu walifundishwa vibaya.

Je, hii inafanana na KUJUTA baada ya kufanya kosa au  
dhambi? HAPANA.

Mtu anaweza KUJUTA, hata kulia lakini baadaye  
AKARUDI kufanya yaliyomliza na kujutia...

Je, mtu akifanya dhambi asitubu? Hapana ATUBU,  
yaani ABADILIKE NA KUACHA.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Sasa ile kumwomba Mungu anisamehe kwa machozi na kujuta ina kazi gani? HAIMSAIDII MUNGU KUKUSAMEHE... INAKUSAIDIA KUJISIKIA VIZURI TU KIHISIA KWA SABABU YA ULICHOKIFANYA. (Siyo mbaya)

Mungu ALIKUSAMEHE kwa sababu ya SADAKA YA YESU KRISTO. Hicho ni kitu pekee ambacho Mungu anakiangalia.

Na ukifikiri wingi wa Machozi yako au Maneno yako ya kuomba Msamaha ndiyo yatakayomfanya Mungu akusamehe dhambi ni KUIDHARAU KAZI YA MSALABA. (haya tutaelezea zaidi mbeleni).

Kwa tafsiri hii ya toba... hakuna sehemu nimeona kwenye maandiko Yesu au mtume yejote akifundisha juu ya **MAOMBI YA TOBA...**

**TOBA YA KWELI SIYO MAOMBI WALA MANENO.**

Sasa tuangalie sehemu ambazo Maneno "toba, kutubu, tubuni, n.k) yametumika na lengo la Matumizi yake.

## 1. TOBA

Niliposema *Toba si Maombi watu wengi wanashangaa...* kwa sababu wamezoea KUOMBA TOBA... Tuangalie hapa... *Mathayo 3:8*

*[8] Basi zaeni matunda yapasayo toba;*

Hapa Yohana alikuwa anawaambia Mafarisayo na Masadukayo waliokuja awabatize kwamba KAMA WAMEAMINI UBATIZO WAKE NA WAONYESHE MATOKEO YAKE KWA VITENDO.

Simple...

Watu walikuwa wakienda kwa YOHANA anawahubiria, wakishaelewa ujumbe wake anawabatiza... hakuwa anafanya maombi ya TOBA...

Angalia na hapa...*Marko 1:4*

*[4] Yohana alitokea, akibatiza nyikani, na kuuhubiri ubatizo wa toba liletalo ondoleo la dhambi.*

Kama toba ingekuwa ni maombi, angehubirije?

Lakini hapa anahubiri watu wamgeukie Yeye Ajaye mwenye uwezo wa kuondoa dhambi ambaye ni Yesu Kristo.

Angalia na hapa pia...*Luka 24:47*

*[47] na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu.*

Angalia *MAHUBIRI YA TOBA NA ONDOLEO LA DHAMBI*. Yaani wahubiri WAMGEUKIE Yesu ili dhambi zao ziondolewe au zifutwe maana tunajua Yeye peke yake awezaye kuondoa dhambi.

SASA, UKICHUNGUZA MISTARI YOTE YENYE NENO TOBA... UTAGUNDUA MAMBO YAFUATAYO:

1. *Toba haina uhusiano na maombi.*
2. *Toba haina uhusiano wa moja kwa moja na dhambi.*

Ila...

1. *Toba ina uhusiano na kubadilika kutoka njia moja au imani moja au mtazamo mmoja kwenda Mwingine.*
2. *Toba ni tendo linalofanywa na mtu aliyesikia injili na kumgeukia Yesu ili apate ondoleo la dhambi zake.*

**Njia rahisi ya kuwapa watu Toba ni: Kuwahubiria Injili ya kweli.**

Yohana alihubiri TOBA... hakuomba...

Paulo alihubiri TOBA... hakuomba...

Mungu anatuvuta kwa upendo ili TUTUBU (tumgeukie)...

Yohana Alitaka watu watubu (wabadi like kifikra ili KUPOKEA ufalme wa Mungu).

## **TUWAFUNDISHE WATU KWELI YA KRISTO ILI WATUBU KWELI KWELI**

Mafundisho ndiyo njia ya kupeleka watu kwenye toba siyo matisho. Kweli ndiyo itubishayo.

Naamini tangu nianze kukufundisha unaona BADILIKO kwenye ufahamu wako na hata maisha yako ya UKRISTO... kama ni kweli basi endelea kutubu.

### **2. TUBUNI**

Katika Biblia yangu ya Kiswahili SUV neno TUBUNI limetajwa Mara tano (5).

Ambazo ni Mathayo 3:2 (Yohana), Mathayo 4:17 (Yesu), Marko 1:15 (Yesu), Matendo 2: 38 (Petro), 3:19 (Petro)

Moja ikiwa imesemwa na Yohana Mbatizaji, Mbili na Yesu na Mbili na Petro.

Cha kushangaza kabisa...hawakusema TUBUNI DHAMBI bali ni vinginevyo.

Hebu tuangalie moja baada ya nyingine... ***Mathayo 3:1-3***

- [1] *Siku zile aliondokea Yohana Mbatizaji akihubiri katika nyika ya Uyahudi, na kusema,*
- [2] *Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia.*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

**[3] Kwa sababu huyo ndiye aliyenenwa na nabii Isaya, akisema, Sauti ya mtu aliaye nyikani, Itengenezeni njia ya Bwana, Yanyosheni mapito yake.**

Yohana Mbatizaji alikuwa anawaandaa watu wampokee Yesu ndiyo maana mstari wa tatu akaandika unabii unaohusu kazi yake ya kuwaandaa watu wampokee YESU KRISTO. Angalia pia **Mathayo 4:17**

**[17] Tokea wakati huo Yesu alianza kuhubiri, na kusema, Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia.**

Yesu aliwaambia wapokee habari alizozileta za ufalme wa Mungu na si vinginevyo. Kumbuka anahubiri habari ambazo Wayahudi walikuwa KINYUME nayo. Kumbuka hapa ndiyo anaanza huduma yake kwa hiyo anawaandaa WAPOKEE. Angalia na **Marko 1:14-15**

**[14] Hata baada ya Yohana kutiwa gerezani, Yesu akaenda Galilaya, akiihubiri Habari Njema ya Mungu,**

**[15] akisema, Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni, na kuiamini Injili.**

Habari hii haina tofauti na ile ya Mathayo 4:17. Tuendelee na **Matendo ya Mitume 2:37-38**

[37] *Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, Tutendeje, ndugu zetu?*

[38] *Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*

Hapa Petro baada ya kuona wamechomwa mioyo yao akawaambia tubuni, yaani geukeni muamini hiki ninachowaambia ili mpokee Roho Mtakatifu. **Matendo ya Mitume 3:18-19**

[18] *Lakini mambo yale aliyohubiri Mungu tangu zamani kwa kinywa cha manabii wake wote, ya kwamba Kristo wake atateswa, ameyatimiza hivyo.*

[19] *Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana;*

PETRO ALIKUWA ANAWAKAZIA JUU YA KUMWAMINI KRISTO ALIYESULUBIWA ILI WAPOKEE MSAMAHA WA BURE... (hana ni baada ya watu kushangaa muujiza wa kiwete kwenye tao la Sulemani.

Hapa ndiyo mahali Petro ametaja **ILI DHAMBI ZENU ZIFUTWE...**

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Na ukweli ni kwamba dhambi zinafutwa kwa  
KUMWAMINI YESU KRISTO KAMA SADAKA YA  
ONDOLEO LA DHAMBI. Angalia... ***Wakolosai 1:14***

**[14] ambaye katika yeye (YESU) tuna  
ukombozi, yaani, msamaha wa dhambi;**

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

# 4

SURA YA

**KUHUSU KUHESABIWA HAKI**



**M**tazamo wa watu wengi juu ya msamaha wa dhambi ni hivi...

- MUNGU ANAPIMA DHAMBI ZAKO DHIDI YA MEMA YAKO.
- DHAMBI ZAKO ZIKIZIDI MEMA YAKO "IMEKULA KWAKO"
- MEMA YAKO YAKIZIDI DHAMBI ZAKO "UNA BAHATI SANA"

**Na huu ndio uongo na udanganyifu mkuu!**

Ukweli ni kwamba Yesu (mwanakondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu) amechukua dhambi... lakini wengi wao hawajapokea ONDOLEO. Hawajapokea kwa sababu wanaamini kwa kujitahidi kutenda mema watajiokoa wenyewe. Huku ni kujihakikishia kushindwa, kwa sababu, kama mwanadamu angeweza kujiokoa basi kusingekuwa na haja ya MWOKOZI. Kutopokea huo msamaha ni kumtukana huyo MWOKOZI. Ni kusema hakufanya kitu. Ni kuidharau ahadi ya Mungu kumwokoa mwanadamu, ahadi ambayo ameitimiza kwa UKAMILIFU WOTE.

Mungu ambaye ni Baba yetu aliyetuzaa katika Kristo Yesu kwa njia ya UFUFUO wake wakati tulipoiamini Injili ndiye anayetuhesabia haki tena bure. Angalia

**Warumi 5:1-2**

*[1] Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na mwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo,*

*[2] ambaye kwa yeye tumepata kwa njia ya imani kuifikia neema hii ambayo mnasimama ndani yake; na kufurahi katika tumaini la utukufu wa Mungu.*

Ukisoma maneno haya ya Waraka wa Paulo ni kama anaagiza kuwepo na amani kwa Mungu lakini ukisoma kwenye KJV. **Rom 5:1 KJV**

***Therefore, being justified by faith, we have peace with God through our Lord Jesus Christ:***

Kwenye KJV anatumia hali ya utimilifu TUNA AMANI NA MUNGU (WE HAVE PEACE) kwa sababu tumeweka imani yetu kwa Kristo hatusimami wakati wowote na hofu mbele za Baba yetu.

Ukiacha kuanza sura ya 5:1 na kurudi nyuma utaona sababu ya kuhesabiwa haki.

Angalia mstari wa mwisho wa Warumi 4 yaani...  
***Warumi 4:25***

***[25] ambaye (KRISTO) alitolewa kwa ajili ya makosa yetu, na kufufuliwa ili mpate kuhesabiwa haki.***

Kuhesabiwa haki ni matokeo ya kuamini katika kufa (kwa ajili ya makosa yako) na kufufuka (ili uhesabiwe haki) kwa Yesu Kristo.

Kuamini katika kufa na kufufuka kwa Yesu Kristo ndiyo KIGEZO **pekee** cha kuhesabiwa haki.

Paulo anaandika pia, ***Warumi 4:6-8***

***[6] Kama vile Daudi aunenavyo uheri wake mtu yule ambaye Mungu amhesabia kuwa na haki pasipo matendo,***

***[7] Heri waliosamehewa makosa yao, Na waliositiriwa dhambi zao.***

***[8] Heri mtu yule ambaye Bwana hamhesabii dhambi.***

Hii inaonyesha kuwa haki haipatikani kwa matendo (yaani kile anachokifanya mtu ili Mungu afanye) bali kwa kuamini au kukubali KUPOKEA kama zawadi kutoka kwa Mungu.

Vivyo hivyo anawaita WALIOSITIRIWA DHAMBI ZAO AU AMBAO HAWAHESABIWI DHAMBI.

Maneno haya Paulo aliyachukua kwenye **Zaburi 32:1-2**

*[1] Heri aliyesamehewa dhambi, Na kusitiriwa makosa yake.*

*[2] Heri BWANA asiyemhesabia upotovu, Ambaye rohoni mwake hamna hila.*

Hii inaonyesha kuwa swala la Mungu kumhesabia mtu haki siyo swala mtambuka... Daudi aliona na kutabiri juu ya ahadi hiyo kwa kila amwaminiye Yesu Kristo.

Daudi anasema rohoni mwake hakuna hila ni sawa na kusema rohoni mwako kuko sawa... hana udanganyifu (guile) au KUTOAMINI. Angalia Paulo alivyoandika...

**Warumi 3:21-26**

*[21] Lakini sasa, haki ya Mungu imedhihirika pasipo sheria; inashuhudiwa na torati na manabii;*

*[22] ni haki ya Mungu iliyo kwa njia ya imani katika Yesu Kristo kwa wote waaminio. Maana hakuna tofauti;*

*[23] kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu;*

*[24] wanahesabiwa haki bure kwa neema yake,  
kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu;*

*[25] ambaye Mungu amekwisha kumweka awe  
upatanisho kwa njia ya imani katika damu  
yake, ili aonyeshe haki yake, kwa sababu ya  
kuziachilia katika ustahimili wa Mungu dhambi  
zote zilizotangulia kufanywa;*

*[26] apate kuonyesha haki yake wakati huu, ili  
awe mwenye haki na mwenye kumhesabu haki  
ye ye amwaminiye Yesu.*

Torati na manabii zina ujumbe mmoja tu HAKI KWA IMANI... Yaani hakuna mtu atakayehesabiwa haki mbele za Mungu na kuonekana kwamba amestahili uzima wa milele *ila* KWA IMANI TU yaani **KUKUBALI KAZI YA MSALABA (KUFA NA KUFUFUKA KWA YESU KRISTO).**

**KWA HIYO YESU NI MWENYE HAKI (NDIYE ALIYEKUFA NA KUFUFUKA) NA KWA SABABU HIYO YEYE NDIYE MWENYE KUHESABIA HAKI ANAYEMWAMINI.**

Yeye ndiye upatanisho na anawahesabia watu HAKI BURE (Kazi ya mwanadamu ni KUPOKEA tu haki hiyo). Si ya bure kwamba haina gharama *ila* kwa sababu anayetoe ni MTOAJI (GENEROUS).

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

*A free gift is not necessarily a cheap gift. It so expensive that no man can match the price and the best thing is the owner to give freely.*

That's our RIGHTEOUSNESS.

Ndiyo maana anaendelea kusema, *Warumi* 3:27

*[27] Ku wapi, basi, kujisifu? Kumefungiwa nje.  
Kwa sheria ya namna gani? Kwa sheria ya matendo? La! Bali kwa sheria ya imani.*

Hakuna mwanadamu anayeweza kujisifu juu ya haki ya Mungu kwani haitolewi kwa vigezo vyta kibinadamu bali udhihirisho wa upendo wa Mungu. LOVE GIVES. Anaongeza kwa kusema, *Wagalatia* 2:16

*[16] hali tukijua ya kuwa mwanadamu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria, bali kwa imani ya Kristo Yesu; sisi tulimwamini Kristo Yesu ili tuhesabiwe haki kwa imani ya Kristo, wala si kwa matendo ya sheria; maana kwa matendo ya sheria hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki.*

Hii inafunga kesi kabisa... HAKUNA MWENYE MWILI KWA MATENDO YA SHERIA AU KUJITAHIDI KUFIKA VIWANGO FULANI ILI AHESABIWE HAKI.

Paulo anaongeza kwenye, *Wagalatia* 2:20-21

*[20] Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani*

*yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.*

**[21] Sübatali neema ya Mungu; maana, ikiwa haki hupatikana kwa njia ya sheria, basi Kristo alikufa bure.**

Paulo anasimama kuonyesha kuwa MATESO ALIYOPITIA KRISTO NI YA KWAKE, KUFUFUKA KWAKE NI KWA AJILI YAKE wala HAHITAJI tena kufanya jambo lolote ili astahili kuhesabiwa haki.

Anaonyesha ya kuwa Kristo alipata mateso na kushinda MAUTI kwa ajili yake... angalia, **2 Wakorintho 5:21**

**[21] Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye.**

Hii ni sawa na kusema alikaa sehemu ya **ADHABU** yako ili wewe upate **HAKI** yake. Alikubali Mshahara wako wa **MAUTI** ili Akupe **UZIMA WAKE BURE**. Angalia, **Warumi 6:23**

**[23] Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.**

KARAMA (UTOAJI BURE) YA MUNGU NI UZIMA WA MILELE KATIKA KRISTO YESU BWANA WETU. Kila mwamini anatakiwa kutembea katika uhalisia huo. Anayo haki yenye uzima... yaani Mungu

amemkubali na kumpa uzima wake ndani yake bila ye ye  
kufanya chochote ila KUAMINI KAZI KUBWA YA  
UKOMBOZI ULIO KATIKA KRISTO YESU.

***NDUGU YANGU, UMEHESABIWA NA MUNGU YA  
KUWA UMESTAHILI YALE AMBAYO HUSTAHILI  
KWA SABABU UMEMWAMINI KRISTO YESU.***

Mimi ni haki ya Mungu,  
Nimehesabiwa haki,  
Ninayo amani na Mungu,  
Nimepatanishwa na Mungu,  
Ninayo haki ya uzima ndani yangu.

Tumeshaweka sawa ya kuwa KUHESABIWA HAKI NI  
ZAO LA IMANI KATIKA KRISTO YESU PEKEE na  
hakuna mtu anayeweza kutengeneza na hivyo hana la  
kujisifia ila kushukuru. Angalia, Warumi 3:21-24

*[21] Lakini sasa, haki ya Mungu imedhihirika  
pasipo sheria; inashuhudiwa na torati na  
manabii;*

*[22] ni haki ya Mungu iliyo kwa njia ya imani  
katika Yesu Kristo kwa wote waaminio. Maana  
hakuna tofauti;*

*[23] kwa sababu wote wamefanya dhambi, na  
kupungukiwa na utukufu wa Mungu;*

*[24] wanahesabiwa haki bure kwa neema yake,  
kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu;*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

WANAHESABIWA HAKI BURE. Paulo anakazia kwa, Wagalatia 2:21

*[21] Sübatili neema ya Mungu; maana, ikiwa haki hupatikana kwa njia ya sheria, basi Kristo alikufa bure.*

Kwa hiyo kufa kwake huleta HAKI BURE kama watu wanatafuta haki kwa matendo ya sharia basi ALIKUFA KRISTO BURE. Nasi tunajua hakufa bure.

Mara nyingi watu wakianza kuelewa juu ya Haki Bure IPATIKANAYO kwa imani katika Kristo Yesu kitabu cha Yakobo kinarejea kichwani hasa kwenye Mistari ifuatayo... *Yakobo 2:24*

*[24] Mwaona kwamba mwanadamu huhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo yake; si kwa imani peke yake.*

Na Yakobo 2:26

*[26] Maana kama vile mwili pasipo roho umekufa, vivyo hivyo na imani pasipo matendo imekufa.*

LAKINI YAKOBO ALIKUWA ANAMAANISHA NINI? Yakobo alitofautiana na Paulo? Maana kweli kwa USHAHIDI mwingi tumeona ya kuwa MWANADAMU HUHESABIWA HAKI KWA IMANI PEKE YAKE MBELE ZA MUNGU. Sasa Yakobo aliandika nini? Je, alitofautiana na Paulo aliyeandika

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

kwa Warumi na Wagalatia kwa habari ya Kuhesabiwa haki bure kwa Imani?

Hebu tuanze habari ilipoanza... *Yakobo 2:14*

*[14] Ndugu zangu, yafaa nini, mtu akisema ya kwamba anayo imani, lakini hana matendo? Je! Ile imani yaweza kumwokoa?*

Hapa Yakobo alikuwa anaelezea imani isibaki peke yake bali ioneckane kwenye mwenendo au matendo.

Sote tunajua ya kuwa imani yetu inakuja na matendo lakini matendo yetu hayaleti imani.

Yaani hatufanyi ili tuwe wema, tumepokea Roho mwema ili tutende matendo mema. Kuelewa alichokuwa anamaanisha Yakobo, Paulo ameelezea wazi... Angalia Waefeso 2:8-10

*[8] Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu;*

*[9] wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.*

*[10] Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo.*

Angalia alivyosema... TUMEOKOLEWA KWA NEEMA si kwa jitihada zetu. Kipawa cha MUNGU yaani (unapewa kazi yako ni KUPOKEA huna cha

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

kuongeza kwenye hiyo kazi). Na ndiyo maana huwezi kujisifu... YOU DID NOTHING AT ALL.

Tu kazi yake (KIUMBE kipyा siku ulipoamini ulifanywa KIUMBE kipyा ndani ya Kristo) TUTENDE... YAANI HIYO IKO KWENYE ROHO YA KIUMBE KIPYA. TUMEUMBWA NAYO KATIKA KRISTO SIYO ILI YATUOKOE BALI TUENENDE NAYO.

Settled?

Angalia USHAHIDI mwingine wa Paulo kwa *Tito 3:4-8*

*[4] Lakini wema wake Mwokozi wetu Mungu, na upendo wake kwa wanadamu, ulipofunuliwa, ALITUOKOA;*

*[5] si kwa sababu ya MATENDO ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu;*

*[6] ambaye alitumwagia kwa wingi, kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu;*

*[7] ili TUKIHESABIWA haki kwa NEEMA yake, tupate kufanywa warithi wa uzima wa milele, kama lilivyo tumaini letu.*

*[8] Ni neno la kuaminiwa; na mambo hayo nataka uyanene kwa nguvu, ili wale WALIOMWAMINI MUNGU WAKUMBUKE*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

***KUDUMU KATIKA MATENDO MEMA. Hayo ni mazuri, tena yana faida kwa WANADAMU.***

Angalia alivyoweka. Kwanza ameonyesha namna WOKOVU au kuhesabiwa haki kulivyopatikana (HATUOKOKI KWA MATENDO WALA KUHESABIWA HAKI KWAYO) Kisha anaagiza kwa habari ya MWENENDO.

*ANGALIA... WALIOMWAMINI MUNGU  
WAKUMBUKE KUDUMU KATIKA MATENDO  
MEMA. Hayo ni mazuri, tena yana faida kwa  
WANADAMU.*

Walioamini ndiyo wenyе kuhesabiwa haki bure, anataka WAKUMBUSHWE KUDUMU katika Matendo mema si kwa sababu Mungu anayataka ila YANA FAIDA KWA WANADAMU.

Yaani hata kama Mungu hakuhesabii haki kwa MATENDO MEMA... WANADAMU WANAYATAKA. FANYA KWA SABABU UMEUMBIWA (ASILI YAKO KATIKA KRISTO) KAMA KIUMBE KIPYA ULIPOZALIWA KWA KUPOKEA ROHO WA UZIMA NDANI YAKO.

Tuendelee na Yakobo... angalia anavyoelezea alichomaanisha hapo juu mstari wa 14... ***Yakobo 2:15-17***

**[15] Ikiwa ndugu mwanamume au ndugu mwanamke yu uchi na kupungukiwa na riziki,**

**[16] na mtu wa kwenu akawaambia, Enendeni zenu kwa amani, mkaote moto na kushiba, lakini asiwape mahitaji ya mwili, yafaa nini?**

**[17] Vivyo hivyo na imani, isipokuwa ina matendo, imekufa nafsini mwake.**

Umeona hayo Matendo? Ni Matendo Mema ya Mwamini! Alichosema Yakobo haina tofauti pia alichosema Yohana kwenye ***1 Yohana 3:16-18***

**[16] Katika hili tumelifahamu pendo, kwa kuwa YEYE ALITOA UHAI WAKE KWA AJILI YETU; imetupasa na sisi kuutoa uhai wetu kwa ajili ya hao ndugu.**

**[17] Lakini mtu akiwa na riziki ya dunia, kisha akamwona ndugu yake ni mhitaji, akamzilia huruma zake, je! Upendo wa Mungu wakaaje ndani yake huyo?**

**[18] Watoto wadogo, tusipende kwa neno, wala kwa ulimi, bali kwa tendo na kweli.**

Huku ndiko kuonyesha imani kwa matendo... kwa sababu imani hutenda kazi katika upendo. ***Wagalatia 5:6***

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

**[6] Maana katika Kristo Yesu kutahiriwa hakufai neno, wala kutokutahiriwa, bali imani itendayo kazi kwa upendo.**

Anaendelea kusema... *Yakobo 2:18-20*

**[18] Lakini mtu atasema, Wewe unayo imani, nami ninayo matendo. Nionyeshe imani yako pasipo matendo, nami nitakuonyesha imani yangu kwa njia ya matendo yangu.**

**[19] Wewe waamini ya kuwa Mungu ni mmoja; watenda vema. Mashetani nao waamini na kutetemeka.**

**[20] Lakini wataka kujua, wewe mwanadamu usiye kitu, kwamba imani pasipo matendo haizai?**

HAIZAI?

Usiye na kitu?

Yes. Imani yako iko moyoni tu... lakini wanadamu tutajuaje wewe ni mwema usipofanya jambo?

Nitakuonyesha imani yangu kwa njia ya matendo.

Kilichotangulia ni Imani...

Ni sawa na kusema TUTAJUAJE HUYU NI MBWA ASIPOBWEKA? Habweki ili awe mbwa, anabweka kwa sababu ni mbwa. Anaonyesha Yeye ni nani?

Anaendelea... *Yakobo 2:21-24*

**[21] Je! Baba yetu Ibrahimu hakuhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo, hapo alipomtoa Isaka mwanaawe juu ya madhabahu?**

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

**[22] Waona kwamba imani ilitenda kazi pamoja na matendo yake, na ya kwamba imani ile ilikamilishwa kwa njia ya matendo yale.**

**[23] Maandiko yale yakatimizwa yaliyonena, Ibrahimu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa ni haki; naye aliitwa rafiki wa Mungu.**

**[24] Mwaona kwamba mwanadamu huhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo yake; si kwa imani peke yake.**

Ukisoma kwa haraka unaweza kufikiri amepingana na yote aliyosema hapo juu...

Tendo la Ibrahimu kwenda kumtoa Isaka ni kwa sababu aliamini kwenye UFUFUO wa Yesu Kristo. Yes.

Angalia... *Warumi 4:1-3*

**[1] Basi, tusemeje juu ya Ibrahimu, baba yetu kwa jinsi ya mwili?**

**[2] Kwa maana ikiwa Ibrahimu alihesabiwa haki kwa ajili ya matendo yake, analo la kujisifia; lakini si mbele za Mungu.**

**[3] Maana maandiko yasemaje? Ibrahimu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa haki.**

Hapa hakuna MATENDO. *Warumi 4:9-10*

**[9] Basi je! Uheri huo ni kwa hao waliotahiriwa, au kwa hao pia wasiotahiriwa?**

*Kwa kuwa twanena ya kwamba kwake  
Ibrahimu imani yake ilihesabiwa kuwa ni haki.  
[10] Alihesabiwaje basi? Alipokwisha  
kutahiriwa, au kabla hajatahiriwa? Si baada ya  
kutahiriwa, bali kabla ya kutahiriwa.*

Hapa pia MATENDO YAMETUPWA NJE.

Ibrahimu tena... *Warumi 4:19-25*

*[19] Yeye asiyekuwa dhaifu wa imani, alifikiri  
hali ya mwili wake uliokuwa umekwisha kufa,  
(akiwa amekwisha kupata umri wa kama miaka  
mia), na hali ya kufa ya tumbo lake Sara.*

*[20] Lakini akiiiona ahadi ya Mungu hakusita  
kwa kutokuamini, bali alitiwa nguvu kwa imani,  
akimtukuza Mungu;*

*[21] huku akijua hakika ya kuwa Mungu aweza  
kufanya yale aliyoahidi.*

*[22] Kwa hiyo ilihesabiwa kwake kuwa ni haki.*

*[23] Walakin haikuandikwa kwa ajili yake tu  
kwamba ilihesabiwa kwake;*

*[24] bali na kwa ajili yetu sisi mtakaothesabiwa  
vivyo hivyo, sisi tunaomwamini yeye  
aliyemfufua Yesu Bwana wetu katika wafu;*

*[25] ambaye alitolewa kwa ajili ya makosa yetu,  
na kufufuliwa ili mpate kuhesabiwa haki.*

Ibrahimu aliamini kwenye UFUFUO wa Yesu Kristo  
kama ahadi. Na ikahesabiwa kwake kuwa HAKI. Sasa  
hili tendo la kumtoa Isaka lilikuwa na kazi gani? Ni

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

kumfundisha mtoto wake Isaka juu ya Ahadi ya Mungu ya ukombozi katika Kristo (KWAMBA MUNGU ATAMTOA MWANAKONDODA WAKE KWA AJILI YA ONDOLEO LA DHAMBI).

Isaka alitaka kujua kondoo yuko wapi... *Mwanzo 22:7-8*

*[7] Isaka akasema na Ibrahimu baba yake, akinena, Babangu! Naye akasema, Mimi hapa, mwanangu. Akasema, Tazama! Moto upo, na kuni zipo, lakini yuko wapi mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa?*

*[8] Ibrahimu akasema, MUNGU ATAJIPATIA MWANA-KONDODA kwa hiyo sadaka, mwanangu. Basi wakaendelea wote wawili pamoja.*

Mwana-kondoo huyo ni Yesu Kristo. Angalia *Yohana 1:29*

*[29] Siku ya pili yake amwona Yesu anakuja kwake, akasema, Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu!*

Angalia pia *Yohana 3:16*

*[16] Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*

Huyo mwana-kondoo ni Mwanae Yesu Kristo.

Angalia *Mwanzo 22:13*

*[13] Ibrahimu akainua macho yake, akaangalia, na tazama, kondoo mume yuko nyuma yake, amenaswa pembe zake katika kichaka. Basi Ibrahimu akaenda akamtwaa huyo kondoo, akamtoa awe sadaka ya kuteketezwa badala ya mwanaawe.*

Kwa hiyo IBRAHIMU aliamini kwamba Bwana atajipatia... hapo ndiyo YEHOVA YIRE ILIPOTOKA... YEHOVA YIRE ni ahadi ya kuwa Mungu atamtoa Mwanae na si vinginevyo. Yakobo anasema Ibrahimu alihesabiwa ana haki kwa kumtoa MWANAWE. Ukiangalia vizuri aliyeiona hiyo haki ni ISAKA kwani Ibrahimu alikuwa anaamini TAYARI. Ibrahimu alikuwa amekwishaamini kabla ya KITENDO cha Kumtoa Isaka kwenye sura ya 22. Rudi nyuma hadi sura ya 15. Kumtoa Isaka ni tendo linaloonyesha imani siyo ili ahesabiwe haki ila kwa sababu ameamini na amehasabiwa haki.

### *Mwanzo 15:5-6*

*[5] Akamleta nje, akasema, Tazama sasa mbinguni, kazihesabu nyota, kama ukiweza kuzihesabu. Akamwambia, Ndivyo utakavyokuwa uzao wako.*

*[6] Akamwamini BWANA, naye akamhesabia jambo hili kuwa haki.*

Kwa Ibrahimu hayakuanza matendo, ilianza IMANI akatenda kwa sababu aliamini.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Kumbuka Muktadha...

YANAFAA KWA WANADAMU (*Tito 3:8*) ALIYE UCHI NA KUPUNGUKIWA RIZIKI ANASAIDIKA (*Yakobo 2:15,16*).

Kwa sababu Ibrahimu alikuwa na haki tayari. Yakobo mwenyewe anafunga ukurasa kwenye *Yakobo 2:23* kwa kusema...

*[23] Maandiko yale yakatimizwa yaliyonena, Ibrahimu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa ni haki; naye aliitwa rafiki wa Mungu.*

Alipokuwa anaenda kumtoa Isaka tayari alikuwa na haki. Angalia *Waebraania 11:8-10*

*[8] Kwa imani Ibrahimu alipoitwa aliitika, atoke aende mahali pale atakapopapata kuwa urithi; akatoka asijue aendako.*

*[9] Kwa imani alikaa ugenini katika ile nchi ya ahadi, kama katika nchi isiyo yake, akikaa katika hema pamoja na Isaka na Yakobo, warithi pamoja naye wa ahadi ile ile.*

*[10] Maana alikuwa akiutazamia mji wenyе misingi, ambao mwenye kuubuni na kuujenga ni Mungu.*

Kitendo cha kutoka kwao na kufuata Maelekezo ya kwenda asipopajua alikuwa na imani...

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Rahabu ni mfano Mwingine pia. ***Yakobo 2:25-26***

*[25] Vivyo hivyo na Rahabu, yule kahaba naye, je! Hakuhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo, hapo alipowakaribisha wajumbe, akawatoa nje kwa njia nyininge?*

*[26] Maana kama vile mwili pasipo roho umekufa, vivyo hivyo na imani pasipo matendo imekufa.*

Naomba tujue ya kuwa Rahabu aliokolewa kwa kitendo ALICHOKIFANYA... lakini kitendo kile hakikumpa IMANI ILI AHESABIWE HAKI BALI ALITENDA ALICHOTENDA KWA SABABU ALIAMINI JUU YA MUNGU WA ISRAELI. Kitendo hicho kilionekana na wanadamu (WAPELELEZI) lakini Mungu alishamhesabia haki kwa sababu tayari aliamini.

Angalia ***Waebraania 11:31***

*[31] Kwa imani Rahabu, yule kahaba, hakuangamia pamoja na hao walioasi; kwa kuwa aliwakaribisha wale wapelelezi kwa amani.*

Kuonyesha ya kuwa Rahabu alikuwa na imani ni kwa sababu YEYE NA WATU WENGINE WA YERIKO WALIKUWA NA HABARI JUU YA MUNGU ALIVYOWAPIGANIA WAISRAELI lakini badala ya KUAMINI wao walitafuta kuwaua WAPELELEZI wale.

Rahabu angekuwa na imani moyoni na asingeckukua hatua ya kuwakaribisha wale WAPELELEZI, wangejuaje? Angalia *Yoshua 2:1-15*

[1] *Yoshua, mwana wa Nuni, akawatuma watu wawili kutoka Shitimu kwa siri, ili kupeleleza, akawaambia, Enendeni mkaitazame nchi hii, na Yeriko. Wakaenda wakafika nyumbani kwa kahaba mmoja jina lake aliitwa Rahabu, wakalala huko.*

[2] *Mfalme wa Yeriko akaambiwa, kusema, Tazama, watu wawili wa wana wa Israeli wameingia humu leo usiku, ili kupeleleza nchi.*

[3] *Mfalme wa Yeriko akatuma watu kwa Rahabu, akasema, Watoe watu wale waliokuja kwako, walioingia ndani ya nyumba yako, maana wamekuja ili kupeleleza nchi.*

[4] *Yule mwanamke akawatwaa wale watu wawili, akawaficha, akasema, Naam, wale watu walikuja kwangu, lakini sikujua walikotoka;*

[5] *ikawa kama wakati wa kufungwa lango la mji, kulipokuwa giza, watu wale wakatoka, wala sijui walikokwenda; wafuateni upesi, maana mtawapata.*

[6] *Lakini yeye alikuwa amewapandisha darini, akawaficha kwa mabua ya kitani, aliyokuwa ameyatandika juu ya dari.*

[7] *Basi hao watu wakawafuata kwa njia iendayo Yordani mpaka vivukoni; na mara wale watu waliowafuatia walipokwisha kutoka, wakalifunga lango.*

[8] *Tena kabla hawajalala akawaenda juu darini,*

[9] *akawaambia wale wanaume, Mimi najua ya kuwa BWANA amewapa ninyi nchi hii, na ya kuwa hofu imetuangukia mbele yenu, na ya kuwa wenyeji wote wa nchi wanayeyuka mbele yenu.*

[10] *Maana tunesikia jinsi BWANA alivyoyakausha maji ya bahari ya Shamu mbele yenu, hapo mlipotoka Misri, tena mambo hayo mliyowatenda wafalme wawili wa Waamori waliokuwa huko ng'ambo ya Yordani, yaani, Sihoni na Ogu, mliowaangamiza kabisa.*

[11] *Na MARA TULIPOSINKIA HAYO MIOYO YETU ILIYEYUKA, wala HAUKUSALIA UJASIRI wo wote katika mtu awaye yote, kwa sababu yenu; kwa kuwa BWANA, Mungu wenu, yeye ndiye Mungu, katika mbingu juu na katika nchi chini.*

[12] *Basi sasa, nawasihi, niapieni kwa BWANA, kwa kuwa nimewatenda ihisani, ya kwamba ninyi nanyi mtaitenda ihisani nyumba ya baba yangu; tena nipeni alama ya uaminifu;*

*[13] ya kwamba mtawaponya hai baba yangu na mama yangu, na ndugu zangu wanaume na wanawake, na vitu vyote walivyo navyo, na kutuokoa roho zetu na kufa.*

*[14] Wale wanaume wakamwambia, Uhai wetu badala ya uhai wenu, ikiwa hamwitangazi habari ya shughuli yetu hii; kisha itakuwa, wakati BWANA atakapotupa nchi hii, tutakutendea kwa ihisani na uaminifu.*

*[15] Ndipo akawashusha kwa kamba dirishani, maana nyumba yake ilikuwa katika ukuta wa mji; naye alikaa ukutani.*

Kwa hiyo Rahabu aliamini alipopata Taarifa na hivyo aliheسابيوا haki. NA KWA SABABU HIYO ALITENDA SAWA SAWA NA IMANI YAKE. HIVYO IMANI IMEZAA MATENDO MEMA (HAKI MACHONI KWA WAPELELEZI).

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

# 5

SURA YA

***KUHUSU MATENDO MEMA***



**M**ara nyingi **watu** wakijifunza juu ya haki ya Mungu na msamaha wa milele, kwa sababu wamelelewa katika kuamini kwenye jitihada zao, maswali yao mara nyingi ni yale yale. Kwa hiyo tunaweza kujiachia tu, tunaweza kufanya chochote muda wowote? Na maswali yanayofanana na hayo. Hili ni rahisi kabisa kama tukichambua maandiko sawa sawa.

**Angalia Wagalatia 2:21**

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

**[21] Sübatili neema ya Mungu; maana, ikiwa haki hupatikana kwa njia ya sheria, basi Kristo alikufa bure.**

**KWELI KABISA: Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zangu na kufufuka ili nihewabiwe haki. HILI NIMELIPOKEA KWA MIKONO MIWILI. SINA NIA MBILI. NAMWAMINI NA HAKI YAKE NINAYO!**

Settled! Limeisha!..

Kama Yesu alikufa ili tuwe na maadili mazuri; basi alishindwa mapema sana maana tayari aliwakuta Wayahudi wenyewe maadili mazuri. Sasa alikufaje kwa ajili yao? Wenyewe wangeshangaa sana. Maadili mema ni mazuri kweli tena yanafaa kusisitizwa; kila jamii na utamaduni, mila na desturi hata shule na taasisi mbalimbali zinafundisha juu ya hayo, kabla ya Yesu kuja na baada ya kufufuka yalikuwa ni maisha ya kawaida. Watu wengi hata wasio wakristo wana maadili mazuri, tena wakati mwengine hata wakristo hawawafikii kwa maadili. JE, TUSEME WAMEOKOKA?

Pamoja na msisitizo wote juu ya maadili mema, hata ukiwa unatembea barabarani kwa tahadhari ili usikanyage sisimizi... sembuse kumkosea mwenzio bado unaweza kuwa hauna WOKOVU, yaani hujaokoka kabisa, unaishi Jehanamu, yaani unatembea na mauti

kabisa, unaweza kuwa umepotea kabisa na uzima wa milele unasikilizia kwenye bomba (hautauona).

Uwe unavaa sketi ndefu, unafunika hadi uso yaani na umepaka matope watu wasikutamani, unatembea na mgolole au ukiona msichana unaangalia juu au pemberi ili usikosee... unasema umeagana na macho yako kama Ayubu, ukisikia Bongo Fleva unaweka pamba masikioni ili usinajisike... ukipita mitaa yenye dada poa (wanaojiuza) unaenda kujitakasa na kujiosha kwa OMO na sabuni ya takasa... Unaweza kuwa hujawahi hata kuujua WOKOVU.

Unaweza ukawa umevuka kutoa fungu la kumi yaani unatoa la 70, unawahi ibadani unafagia, unaongoza maombi, unachelewa kutoka kwa unyenyekevu kabisa, unambebea mtumishi begi na kujitahidi sana... lakini unaweza bado usiwe kwenye familia ya Mungu.

Unaweza ukawa unawatembelea watoto yatima, unawasaidia wajane, unaguswa sana na shida za wazee, kila siku uko mahospitalini unawaosha mpaka wagonjwa wasio na ndugu zao, unawaonea huruma wanaoteswa una kambi nyumbani ya watu wasiojiweza... unaweza ukawa huna Mungu kabisa.

Haya mambo si mabaya hata kidogo, wala mtu hahitaji kuwa na Mungu (kuamini) ili aweze kuyafanya haya. Wala hayakupi uzima wa milele/msamaha wa dhambi/kuhesabiwa haki/kukaliwa na Roho/kufanyika mwana wa Mungu.

Kama unafanya ili upate uzima wa Mungu, UMEPOTEA KABLA HUJAANZA SAFARI! WOKOVU ni kazi ya Mungu ndani ya Kristo Yesu kwa kufa kwake dhambi zako zimeondolewa, amefufuka ili akutangazie ushindi yaani kakuhesabia haki bure bila wewe kufanya chochote. Kazi yako ni KUAMINI alichokifanya... Yeye ndiye aliona kuwa unazama uko hoi bin taabani, huwezi kujiokoa halafu wewe kwa ujinga kabisa unasema NAJIOKOA KWA MATENDO YANGU. Kwamba Yesu alikuja kuuza sura eeh? UWE NA ADABU BASI.

Ukiona unajitahidi kufanya jambo zaidi ya kuamini kazi kamilifu ya Yesu Kristo basi unajua kabisa unaidharau hiyo kazi... hicho ni kiburi kikuu kabisa! Utakifananisha na nini kiburi cha kuidharau kazi ya Mungu katika Kristo Yesu? angalia *Waefeso 2:8-9*

*[8] Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu;*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

**[9] wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.**

HUNA CHA KUJISIFIA. Yaani unamsifia Yesu Kristo aliyefanya kwa ajili yako. HUKO NDIKO KUMHESHIMU MUNGU! Angalia *Tito 3:4-7*

**[4] Lakini wema wake Mwokozi wetu Mungu, na upendo wake kwa wanadamu, ulipofunuliwa, alituokoa;**

**[5] si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu;**

**[6] ambaye alitumwagia kwa wingi, kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu;**

**[7] ili tukihesabiwa haki kwa neema yake, tupate kufanywa warithi wa uzima wa milele, kama lilivyo tumaini letu.**

Paulo anamwambia mwanae katika imani (Tito). Ni wema wake Mwokozi wetu Mungu, na upendo wake kwa wanadamu, ulipofunuliwa, alituokoa; si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi (HAPANA); bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa, kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu ndiyo kuhesabiwa haki kwa neema yake (siyo jitihada zetu), kufanywa

warithi (unafanya kazi urithi?) wa uzima wa milele (si wa kitambo ni wa milele).

Ndiyo maana mitume hawakuwahi kufundisha KUOKOLEWA KWA JITIHADA AU MATENDO YETU... Walifundisha matendo mema kama zao la imani... yaani TUNDA LA ROHO wala siyo mzizi au chanzo. Unatenda mema siyo ILI MUNGU akuhesabie haki... bali kwa sababu ni asili yako katika Kristo. UNA ROHO MWEMA NDANI YAKO. *Wagalatia 5:22-23*

*[22] Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, [23] upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria.*

Kujitahidi kumshawishi Mungu ni kujihesabia haki, hiki ndicho Mungu anaita kiburi. Yesu aliwahi kutoa mfano huu kwenye *Luka 18:9-12*

*[9] Akawaambia mfano huu watu waliojikinai ya kuwa wao ni wenye haki, wakiwadharau wengine wote.*

*[10] Watu wawili walipanda kwenda hekaluni kusali, mmoja Farisayo, wa pili mtoza ushuru.*

*[11] Yule Farisayo akasimama akiomba hivi moyoni mwake; Ee Mungu, nakushukuru kwa kuwa mimi si kama watu wengine, wanyang'anyi, wadhalimu, wazinzi, wala kama huyu mtoza ushuru.*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

**[12] *Mimi nafunga mara mbili kwa juma;  
hutoa zaka katika mapato yangu yote.***

Kataja mambo mazuri mazuri, mambo ambayo watu wa dini wakikusikia wanakupigia makofi, wanakuona wa kiroho kabisa. Lakini loh! kumbe ni uchafu mbele za Mungu! **Luka 18:13**

**[13] *Lakini yule mtoza ushuru alisimama mbali,  
wala hakuthubutu hata kuinua macho yake  
mbinguni, bali alijipiga-piga kifua akisema, Ee  
Mungu, uniwie radhi mimi mwenye dhambi.***

Usifikiri mtoza ushuru hajawahi kufanya hata jambo moja jema. Lakini hakutaja hata moja... alitegemea tu REHEMA ZA MUNGU. KJV wameandika HAVE MERCY ON ME/Be merciful to me.

Yesu anamaliza kwa kusema **Luka 18:14**

**[14] *Nawaambia, huyu alishuka kwenda  
nyumbani kwake amehesabiwa haki kuliko  
yule; kwa maana kila ajikwezaye atadhiliwa,  
naye ajidhiliye atakwezwa.***

Kujikweza ni kuudharau wema wa Mungu na kutukuza matendo au jitihada zako! Au kiburi kinakutawala kama Yule Farisayo? Urahisi wake ni kwa sababu ni kazi ya Mungu, ukiona wewe na Mungu mnapambana ili WOKOVU uje basi ujue kazi ya Mungu ina kasoro.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

**Good News: Haina kasoro... ni kazi kamili na kamilifu tena imkamilishayo kila AAMINIYE.**

Yaani mtu atasoma mambo yote haya na halafu atakuja na hitimisho... *KWA HIYO MATENDO MEMA SI MUHIMU?* Ni muhimu sana. Lakini Mungu hayatumii kukuhesabia haki. Angalia Warumi **3:19-20**

*[19] Basi twajua ya kuwa mambo yote inenayo torati huyanena kwa hao walio chini ya torati, ili kila kinywa kifumbwe, na ulimwengu wote uwe chini ya hukumu ya Mungu;*

*[20] kwa sababu hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki mbele zake kwa matendo ya sheria; kwa maana kutambua dhambi huja kwa njia ya sheria.*

Paulo anaandika kwa Warumi... HAKUNA MWENYE MWILI ATAKAYEHESABIWA HAKI MBELE ZAKE (MUNGU) KWA MATENDO YA SHERIA. Paulo karudia tena kwa *Wagalatia 2:16*

*[16] hali tukijua ya kuwa mwanadamu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria, bali kwa imani ya Kristo Yesu; sisi tulimwamini Kristo Yesu ili tuhesabiwe haki kwa imani ya Kristo, wala si kwa matendo ya sheria; maana kwa matendo ya sheria hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki.*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

MAANA KWA MATENDO YA SHERIA HAKUNA  
MWENYE MWILI ATAKAYEHESABIWA HAKI.

Umeona?

Matendo mema ni ya muhimu kwa ajili ya maisha yetu  
ya hapa duniani, ukiiba utapigwa, utafungwa,  
**hutaaminika** na kama hujauawa bahati yako...

Lakini ukiacha kuiba na Yesu haumwamwini imekula  
kwako. Paulo kwa *Tito 3:4-6*

*[4] Lakini wema wake Mwokozi wetu Mungu,  
na upendo wake kwa wanadamu,  
ulipofunuliwa, alituokoa;*

*[5] si kwa sababu ya matendo ya haki  
tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake, kwa  
kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa  
upya na Roho Mtakatifu;*

*[6] ambaye alitumwagia kwa wingi, kwa njia ya  
Yesu Kristo Mwokozi wetu;*

Tena Tito 3:7-8

*[7] ili tukihesabiwa haki kwa neema yake,  
tupate kufanywa warithi wa uzima wa milele,  
kama lilivyo tumaini letu.*

*[8] Ni neno la kuaminiwa; na mambo hayo  
nataka uyanene kwa nguvu, ili wale  
waliomwamini Mungu wakumbuke kudumu*

*katika matendo mema. Hayo ni mazuri, tena yana faida kwa wanadamu.*

Paulo anasema... wale WALIOMWAMINI Mungu wakumbuke kudumu katika MATENDO mema. Hayo ni mazuri, tena yana FAIDA KWA WANADAMU.

**NOTE: SI KWA MUNGU!**

*“Doing good works is good, but doing good works for bad reasons is even dangerous... i.e. outside Christ, those good works become dead works.”*

*“Trying to save yourself by good works is a sure way to LOSE yourself”*

SASA TUWEKE HIVI, IMANI ISIYO NA MATENDO MEMA ILE IMANI **IMEKUFA** NA MATENDO MEMA YASIYO YA IMANI NA YENYEWE **YAMEKUFA (MAFU)** yanaitwa matendo mafu. Imani iliyokufa tumemalizana nayo kwa Yakobo. Sasa, mara nyingi ukitaja matendo mafu ni rahisi kuwaza moja kwa moja kwamba ni matendo mabaya. Ukweli ni kwamba matendo mafu ni matendo mema au mazuri wala si matendo mabaya. Sasa kinachofanya matendo mema yawe mafu ni nini? NI MTAZAMO WA MTENDAJI HASA JUU YA MUNGU.

Kwa mfano; Kwenye kitabu cha Luka 18 kuna Farisayo mmoja alikuwa anataja matendo mema anayoyafanya mbele za Mungu kama **KIGEZO CHA MUNGU**

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

KUMHESABIA HAKI AU KUMKUBALI AU KUWA  
KIGEZO CHA MUNGU KUJIBU MAOMBI YAKE.  
Angalia anavyosema, **Luka 18:11-12**

*[11]Yule Farisayo akasimama akiomba hivi  
moyoni mwake; Ee Mungu, nakushukuru kwa  
kuwa mimi si kama watu wengine,  
wanyang'anyi, mdhalimu, wazinzi, wala kama  
huyu mtoza ushuru.*

*[12]Mimi nafunga mara mbili kwa juma; hutoa  
zaka katika mapato yangu yote.*

Ni kweli Yeye si mnyang'anyi, mdhalimu wala mzinzi LAKINI si mbele za Mungu bali kwa kujifananisha na wengine. Ni kweli anafunga mara mbili kwa juma na kutoa zaka lakini Mungu hatumii mambo haya kukuhesabia HAKI. Ninajuaje hilo? Angalia Mtoza ushuru alivyosema maombi yake **Luka 18:13**

*[13]Lakini yule mtoza ushuru alisimama mbali,  
wala hakuthubutu hata kuinua macho yake  
mbinguni, bali alijipiga-piga kifua akisema, Ee  
Mungu, uniwie radhi mimi mwenye dhambi.*

Siamini kama mtoza ushuru hana jambo lolote zuri alilolifanya maisha yake yote...ATAKUWA NAYO ila Yeye ALITAZAMA REHEMA ZA MUNGU NA TUMAINI HALIKUWA KWENYE MATENDO YAKE

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

MEMA. Hii ndiyo hukumu ya matendo mafu... Bwana Yesu aliweka wazi... **Luka 18:14**

*[14]Nawaambia, huyu alishuka kwenda nyumbani kwake amehesabiwa haki kuliko yule; kwa maana kila ajikwezaye atadhiliwa, naye ajidhiliye atakwezwa.*

Hivyo ukitaka kutunza matendo yako mema yasioze (YAWE MAFU) MTAZAME YESU PEKE YAKE KAMA KIGEZO CHA UTAKATIFU WAKO NA KUKUBALIKA MBELE ZA MUNGU. Ndiyo maana Yesu Kristo alikufa ili TUTAKASWE KWENYE DHAMIRI TUSIWE NA CHEMBE YA MATENDO MAFU. Angalia **Waebrania 9:13-14**

*[13]Kwa maana, ikiwa damu ya mbuzi na mafahali na majivu ya ndama ya ng'ombe waliyonyunyiziwa wenyewe uchafu hutakasa hata kuusafisha mwili;*

*[14]basi si zaidi damu yake Kristo, ambaye kwamba kwa Roho wa milele alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na mawaa, itawasafisha dhamiri zenu na matendo mafu, mpate kumwabudu Mungu aliye hai?*

Yale Maneno unatumia kwenye maombi, "Ee Mungu sijawahi kumkosea mtu, sijawahi kutukana,

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

nimekutumikia kwa uaminifu, nimeenda hadi porini, nipe Mume mzuri kwa sababu nimejitunza, nk." Huku ni kutoelewa haki ya Mungu, MAANA HAKUNA MWENYE MWILI ATAOKUWA NA HAKI YAKE MBELE ZA MUNGU hata kama amepewa **cheti** cha matendo mema duniani. YAPE MEMA YAKO MAISHA... MTAZAME YESU tu.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

# 6

SURA YA

***KATIKA KRISTO TUNAO (SIYO  
TUTAPATA) MSAMAHA WA DHAMBI***



**K**ati ya mambo ambayo yamewekwa wazi katika nyaraka ni uhakika wa mwamini kuwa na UHAKIKA juu ya kusamehewa dhambi.

Ukisoma kwa utaratibu nyaraka kwa kuangalia nyakati "tenses" zilizotumika utagundua kuwa...

- 1. Msamaha hupokelewa siyo huombwa...**
- 2. Anayepokea anaumiliki...**

Utagundua ya kuwa msamaha wa dhambi kutoka kwa Mungu siyo jambo analolifanya kimwitikio "reacting" ni jambo ambalo Mungu hajafanya kwa kushawishiwa alikuwa "proactive"... ni mpango wake mwenyewe.  
Angalia **Waefeso 1:6-7**

*[6] Na usifiwe utukufu wa neema yake, ambayo ametuneemesho katika huyo Mpendwa.*

*[7] Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake.*

TUNAO UKOMBOZI WETU, MSAMAHYA WA DHAMBI.

Yaani huu ukombozi ni msamaha wa dhambi. Angalia **Wakolosai 1:13-14**

*[13] Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake;*

*[14] ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani, msamaha wa dhambi;*

TUNA UKOMBOZI YAANI MSAMAHYA WA DHAMBI.

Baadhi ya Versions za Kingereza wanatumia "WE HAVE" yaani imekuwa MALI YAKO. **Eph 1:7 KJV**

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

*In whom WE HAVE REDEMPTION through his blood, THE FORGIVENESS of sins, according to the riches of his grace;*

Katika *Col 1:14 KJV*;

*In whom WE HAVE REDEMPTIONS through his blood, even the FORGIVENESS of sins:*

Petro mbele ya baraza... anasema *Matendo ya Mitume 5:30-31*

*[30] Mungu wa baba zetu alimfufua Yesu, ambaye ninyi mlimwua mkimtundika katika mti.*

*[31] Mtu huyo Mungu amemtukuza kwa mkono wake wa kuume, awe Mkuu na Mwokozi, AWAPE Waisraeli TOBA na MSAMAHA wa dhambi.*

NI KITU CHA KUPOKELEWA KUTOKA KWA HUYO MKUU NA MWOKOZI AMBAYE NI YESU KRISTO.

Paulo wakati anaeleza jinsi alivyotokewa na Yesu... anasema *Matendo ya Mitume 26:15-18*

*[15] Nami nikasema, Wewe u nani, Bwana? Bwana akaniambia, Mimi ni Yesu, ambaye wewe unaniudhi.*

*[16] Lakini inuka, usimame kwa miguu yako, maana nimekutokea kwa sababu hii, nikuweke wewe uwe mtumishi na shahidi wa mambo haya*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

*uliyoyaona, na wa mambo ambayo katika hayo  
nitajidhihirisha kwako;*

*[17] nikikuokoa na watu wako, na watu wa  
Mataifa, ambao nakutuma kwao;*

*[18] uwafumbue macho yao, na kuwageuza  
waiache giza na kuielekea nuru, waziache na  
nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu; kisha  
**WAPATE MSAMAHA WA DHAMBI ZAO**, na  
urithi mionganoni mwao waliotakaswa kwa imani  
iliyo kwangu mimi.*

WAPATE MSAMAHA WA DHAMBI ZAO, ina maana  
ni kitu kinapatikana!

Swali ni kwamba, *Je, wewe umepokea?*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

# 7

SURA YA

***NIKUSANYIENI WACHA MUNGU WANGU;  
WALIOFANYA AGANO NAMI KWA  
DHABIHU.***



Siku ya kwanza kuanza kutafakari **Zaburi 50:5**  
*[5] Nikusanyieni wacha Mungu wangu  
Waliofanya agano nami kwa dhabihu.*

Nilikuwa nawaza mambo mengi sana. Kwa ufahrenu wa awali nilidhani Mungu akitaka kufanya agano na mtu anamuagiza atoe sadaka. Nikawa naamini hivyo muda mrefu. Kwanza nilipoanza kuangalia neno lililopo pale si sadaka tu bali "**dhabihu**" ikanifanya niende mbali zaidi.

Neno "**dhabihu**" pale si pesa wala kitu kingine isipokuwa "**sadaka za KUTEKETEZWA**" au "**sacrifice**" kwa Kingereza. Maana neno la Kiebrania lilioko pale ni **ZEBACH** ambao mzizi wake ni "**zâbach**" ambalo maana yake ni "**to SLAUGHTER an animal**" yaani kuchinja mnyama.

Kwa hiyo dhabihu pale si fedha, au mali bali ni kuchinja mnyama au Wanyama (dhabihu)...!

Sasa ukisikia mtu anapayuka "Kama hutoi sadaka akimaanisha pesa basi Mungu hawezi kufanya Agano na wewe ujue tu kakimbia kwa speed kwenye kusoma"

Dhabihu pale si fedha ni **WANYAMA**. Swalii ni kwamba **MUNGU ALIKUWA ANAWASIFIA KWAMBA WANATOA DHABIHU?**

Mistari inayofuata... inajibu vizuri hili... Angalia **Zaburi 50:7-8**

*[7] Sikieni, enyi watu wangu, nami nitanena,  
Mimi nitakushuhudia, Israeli;*

*Mimi ndimi niliye MUNGU, Mungu wako.*

*[8] Sitakukemea kwa ajili ya dhabihu zako,  
Na kafara zako ziko mbele zangu daima.*

Mungu anasema hatawakemea kwa dhabihu na kafara zao.

Kwa nini? **Zaburi 50:9-12**

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

*[9] Sitatwaa ng'ombe katika nyumba yako,  
Wala beberu katika mazizi yako.*

*[10] Maana kila hayawani ni wangu,  
Na makundi juu ya milima elfu.*

*[11] Nawajua ndege wote wa milima,  
Na wanyama wote wa mashamba ni wangu*

*[12] Kama ningekuwa na njaa singekuambia,  
Maana ulimwengu ni wangu, navyo viujazavyo.*

Hii ni kuonyesha ya kuwa Mungu hataki hao WANYAMA. Ni kama vile waliona Mungu ana shida na mifugo yao akasema NO NO NO NO... Ningetaka kwanza ningekuwa najiulia zangu porini tu nakula.

So, kwa nini wao walitoa sasa? *Zaburi 50:13*

*[13] Je! Nile nyama ya mafahali!  
Au ninwe damu ya mbuzi!*

Hapo unaona sentensi hizo mbili ni mshangao na swali...  
Angalia anavyosema... *Zaburi 50:14*

*[14] Mt Olee Mungu dhabihu za kushukuru;  
Mt imizie Aliye juu nadhiri zako.*

MUNGU ANATAKA DHABIHU? YES... LAKINI ZA  
KUSHUKURU si wanyama! Angalia jinsi  
anavyomalizia Zaburi ya 50. *Zaburi 50:23*

*[23] Atoaye dhabihu za kushukuru,*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

*Ndiye anayenitukuza.  
Naye autengenezaye mwenendo wake,  
Nitamwonyesha wokovu wa Mungu.*

Syo anayetoa wanyama, syo amwagaye damu, siyo atoaye kafara au sadaka za KUTEKETEZWA... Hapana. Bali ANAYESHUKURU.

Sasa angalia kwa makini **ALIWAITA WALIOFANYA AGANO KWA DHABIHU ILI AWAAMBIE SITAKI DHABIHU NATAKA MSHUKURU.**

Kama ni kushukuru basi kuna kitu Mungu kafanya...

Amefanya nini?

Kutoa dhabihu za kushukuru, ndiyo kumtukuza Mungu, ndiyo kutengeneza mwenendo ndiyo atakayeona WOKOVU WAKE.

Kwa hiyo Mungu alitaka WAONE WOKOVU WAKE WASHUKURU NA SIYO KUTOA WANYAMA.

Daudi anaandika kwenye **Zaburi 40:6**

*[6] Dhabihu na matoleo hukupendezwa nazo,  
Masikio yangu umeyazibua,  
Kafara na sadaka za dhambi hukuzitaka.*

Kasema HUKUPENDEZWA NAZO!ILA MASIKIO YANGU UMEZIBUA.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Zaburi ya 50 tumeona kuwa WANATAKIWA KUONA WOKOVU WA BWANA. Hapa anasema MASIKIO YANGU UMEYAZIBUA. Hivyo ANATAKIWA KUSIKIA. Mambo mawili..

...KUONA

...KUSIKIA

**ondoka na hii:** HAKUPENDEZWA NAZO,  
HAKUZITAKA. ANGETAKA ASINGEMUOMBA  
MTU! ANGEJITWALIA WANYAMA WANONO!

Anaendelea kwa kusema **Zaburi 40:7-8**

*[7] Ndipo niliposema, Tazama nimekuja,  
(Katika gombo la chuo nimeandikiwa,)*

*[8] Kuyafanya mapenzi yako,  
Ee Mungu wangu, ndiyo furaha yangu;  
Naam, sheria yako imo moyoni mwangu.*

Nani huyu anakuja? Mapenzi hayo ni yapi? Kwa nini Mungu hakuyataka? Habari hii imerudiwa kwenye **Waebirania 10:1-4**

*[1] Basi torati, kwa kuwa ni kivuli cha mema  
yatayakayokuwa, wala si sura yenye we ya mambo  
hayo, kwa dhabihu zile zile wanazozitoa kila  
mwaka daima, haiwezi wakati wo wote  
kuwakamilisha wakaribiao.*

*[2] Kama ndivyo, je! Dhabihu hazingekoma  
kutolewa; kwa maana waabuduo, wakiisha*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

*kusafishwa mara moja, wasingejiona tena kuwa na dhambi?*

[3] *Lakini katika dhabihu hizo liko kumbukumbu la dhambi kila mwaka.*

[4] *Maana haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi.*

Ilikuwa ni kivuli, au zinaelezea jambo la Kiroho. Wao wakadhani Mungu anataka dhabihu... kumbe Musa alikuwa anatumia mambo yanayoshikika kuelezea mambo yatakayotokea baadaye... yaani Katika KRISTO.

Angalia tena *Waebrania 10:5-7*

[5] *Kwa hiyo ajapo ulimwenguni, asema,  
Dhabihu na toleo hukutaka,  
Lakini mwili uliniwekea tayari;*

[6] *Sadaka za kuteketezwa na sadaka za dhambi  
hukupendezwa nazo;*

[7] *Ndipo niliposema, Tazama, nimekuja  
(katika gombo la chuo nimeandikiwa)  
Niyafanye mapenzi yako, Mungu.*

Kilichoongezeka hapo kwenye Waraka kwa Waebrania ni **LAKINI MWILI ULINIWEKEA TAYARI**.

Kwa sababu dhabihu za wanyama hazikuwa na uwezo na Musa aliagiza kwenye torati... SIYO ILI WATOE bali WAZIBUE MASIKIO YAO, WAONE WOKOVU WA

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

## BWANA KISHA WASHUKURU NA HUKO NDIKO KUMTUKUZA MUNGU!

Sasa, huu mwili ni wa nani? Anaendelea **Waibrania 10:8-10**

*[8] Hapo juu asemapo, Dhabihu na matoleo na sadaka za kuteketezwa na hizo za dhambi hukuzitaka, wala hukupendezwa nazo (zitolewazo kama ilivyoamuru torati),*

*[9] ndipo aliposema, Tazama, nimekuja niyafanye mapenzi yako. Aondoa la kwanza, ili kusudi alisimamishe la pili.*

*[10] Katika mapenzi hayo mmeputa utakaso, kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja tu.*

MAPENZI YA MUNGU SIYO DHABIHU ZA WANYAMA BALI NI KUTOLEWA KWA MWILI WA YESU KRISTO ambapo ndani yake **pekee** ndipo kulipo na UTAKASO KWA KUTOLEWA MARA MOJA TU. HAYO NI MAPENZI YA MUNGU. HILI NDILO LAFAA KUSHUKURU KWALO.

Kwenye hiyo hiyo **Waibrania 10:15-18**

*[15] Na Roho Mtakatifu naye amshuhudia; kwa maana, baada ya kusema,*

*[16] Hili ni agano nitakaloagana nao baada ya siku zile, anena Bwana,*

*Nitatia sheria zangu miyoni mwao,  
Na katika nia zao nitaziandika;  
ndipo anenapo,  
[17] Dhambi zao na uasi wao sitaukumbuka  
tena kabisa.  
[18] Basi, ondoleo la hayo likiwapo, hapano  
toleo tena kwa ajili ya dhambi.*

HILI NDILO AGANO LA MUNGU KWA DHABIHU YAKE MWENYEWE siyo KWA DHABIHU ZAO WENYEWE. Ikae kwenye ufahamu wako kuwa lengo la Zaburi ya 50 siyo kukushawishi utoe dhabihu za wanyama bali ushuruku kwa dhabihu ya Yesu Kristo ambalo ni Agano jipya ambalo ndani yake hakuna kumbukumbu la dhambi wala uovu wetu haukumbukwi. HAPA NI KUSHUKURU TU. HII NDIYO DHABIHU YA AGANO JIPYA. KUSHUKURU KWA SABABU YA WOKOVU WAKE.

Baba wa imani, Ibrahimu alifanya tofauti wakati anampeleka Isaka mlimani... baada ya kuulizwa juu ya kondoo wa sadaka. Angalia *Mwanzo 22:7-8*

*[7] Isaka akasema na Ibrahimu baba yake,  
akinena, Babangu! Naye akasema, Mimi hapa,  
mwanangu. Akasema, Tazama! Moto upo, na  
kuni zipo, lakini yuko wapi mwana-kondoo kwa  
sadaka ya kuteketezwa?*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

*[8] Ibrahimu akasema, Mungu atajipatia mwana-kondoo kwa hiyo sadaka, mwanangu. Basi wakaendelea wote wawili pamoja.*

MUNGU ATAJIPATIA MWANA-KONDOO. Hii ni kuamini ahadi ya kutolewa kwa Yesu Kristo. Ibrahimu anaongea kama nabii.

Angalia kilichotokea *Mwanzo 22:13-14*

*[13] Ibrahimu akainua macho yake, akaangalia, na tazama, kondoo mume yuko nyuma yake, amenaswa pembe zake katika kichaka. Basi Ibrahimu akaenda akamtwaan huyo kondoo, akamtoa awe sadaka ya kuteketezwa badala ya mwanawe.*

*[14] Ibrahimu akapaita mahali hapo Yehova-yire, kama watu wasemavyo hata leo, Katika mlima wa BWANA itapatikana.*

KUPAITA PALE YEHOVA-YIRE NI ALAMA KWAMBA IBRAHIMU ALIAMINI KWAMBA KONDOO ATAPATIKANA KATIKA MLIMA WA BWANA AU BWANA ATATOA KONDOO MWENYEWE.

Huu ulikuwa ni unabii wa kutolewa kwa Yesu Kristo kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu. Ndiyo maana Yohana alivyomwona alisema wazi kwenye *Yohana 1:29*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

**[29] Siku ya pili yake amwona Yesu anakuja kwake, akasema, Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu!**

Kondoo za Agano la Kale zilikuwa ZINAZUNGUMZIA habari za Yesu Kristo na siyo kondoo wenyewe. Wale kondoo walitakiwa kuzibua masikio kuja Mungu alikuwa anazungumza kuwa ATAMTOA MWANAE KWA AJILI YA DHAMBI ZA WANADAMU.

Na hii ilitimia kabisa... baada ya kufufuka kwake. Angalia kwenye *Luka 24:44,46-47*

**[44] Kisha akawaambia, Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyandoikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi.**

**[46] Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu;**

**[47] na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu.**

Kwa jina lake (KUFA NA KUFUFUKA KWAKE) kuwa MATAIFA YOTE WATAHUBIRIWA KWA

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

JINA LAKE HABARI YA TOBA NA ONDOLEO LA DHAMBI. Hili ndilo alilolitaka Mungu!

KWA HIYO **ZABURI 50:5** HAIKUANDIKWA KUHAMASISHA UTOAJI WA SADAKA (SPECIFICALLY DHABIHU) BALI KUZIPONDEA KWA WAO KUDHANI MUNGU ANAZIHITAJI ILI AFANYE AGANO NAO. NDIYO MAANA MISTARI ILIYOFUATA ALIONYESHA KUWA HAHITAJI NA KWAMBA KUTOLEWA KWA MWILI WA YESU KRISTO NDIYO AGANO LENYEWE, AGANO JIPYA.

Kwa hiyo... Mwandishi wa *Waebrania 13:15*

*[15] Basi, kwa njia yake yeye, na tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima, yaani, tunda la midomo iliungamayo jina lake.*

Midomo yetu imejaa shukrani kwa ajili ya Jina la Yesu Kristo (Ukombozi wetu).

Hapa ni shukrani tu!

Amefanya,

Amemaliza,

Tumekombolewa,

Tumetakaswa,

TWASHUKURU!

TUMEONA WOKOVU WA BWANA.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

# 8

SURA YA

**TUKIZIUNGAMA DHAMBI ZETU**



**M**ara nyingi watu wakifundishwa kuwa **msamaha** wa dhambi unapokelewa kwani tayari upo, hurukia kwenye **1 Yohana 1:9**

**[9] Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.**

Huu ni mstari maarufu unaotumika kufundisha KUUNGAMA DHAMBI... neno kuungama limetumika

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

kama "**CONFESS**" likiwa na maana nyingi zaidi Kiswahili ikiwa ni pamoja na KUUNGAMA na pia KUKIRI.

Ukiangalia kwenye lugha ya asili ya Kigiriki ni **HOMOLOGEO** ikiwa na **maneno** mawili **HOMO** ikiwa na maana ya MOJA AU KUFANANA na **LOGOS** ikiwa na maana ya KUSEMA/ KUTAMKA/ KUKUBALI/ KUWAZA.

Kwa hiyo ni sawa na kusema;  
...*Pande zaidi ya moja kukubaliana.*  
... *Kukiri sawa na...*  
... *kutamka sawa na...*  
... *kuwaza sawa na...*

Au KUWA KATIKA MAKUBALIANO.

Angalia hapa kwenye **Warumi 10:9**

*[9] Kwa sababu, UKIMKIRI Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka.*

Neno UKIMKIRI pale ni **HOMOLOGEO**... kwa hiyo hapo maana yake ni kukubaliana na UBWANA wa Yesu Kristo katika kuokoa mwanadamu. Yeye ni Bwana.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

*Vipi kuhusu kuungama dhambi? Je kuna haja ya mimi  
kukubali kuwa nina dhambi au kuzikiri dhambi zangu  
ndiyo Mungu awe mwaminifu kunisafisha na udhalimu  
wote?*

Hebu tuangalia Muktadha wa 1 Yohana 1 kuna nini...  
Mstari wa 1... **1 Yohana 1:1**

*[1] Lile lililokuwako tangu mwanzo,  
tulilolisikia, tuliloliona kwa macho yetu,  
tulilolitazama, na mikono yetu ikalipapasa, kwa  
habari ya Neno la uzima;*

Kwanza kabisa hatuoni hii barua iliandikwa kwa nani  
kama nyaraka zake zingine. Angalia 2 **Yohana 1:1**

*[1] Mzee, kwa mama mteule na watoto wake  
niwapendao katika kweli; wala si mimi peke  
yangu, bali na wote waijuaao ile kweli;*

Iko wazi... angalia na **3 Yohana 1:1**

*[1] Mzee, kwa Gayo mpenzi, nimpendaye katika  
kweli.*

Sasa tuendelee na **1 Yohana 1:2**

*[2] (na uzima huo ulidhahirika, nasi tumeona,  
tena twashuhudia, na kuwahubiri ninyi ule  
uzima wa milele, uliokuwa kwa Baba,  
ukadhihirika kwetu)*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Hapa kafundisha juu ya uzima wa milele. NASI (WATU GANI) na kuwahubiri NINYI (watu gani?). angalia **1 Yohana 1:3**

*[3] hilo tuliloliona na kulisikia, twawahubiri na NINYI; ili NANYI pia mpate kushirikiana NASI: na ushirika wetu ni pamoja na Baba, na pamoja na Mwana wake Yesu Kristo.*

NASI... NANYI... NINYI...

Hapa ni watu wa aina mbili tofauti. Kwa hiyo unaona mpaka hapa anongea na WATU WASIO NA USHIRIKA NA BABA, WASIO NA UZIMA WA MILELE...

Lakini kuna wengine pia wameandikiwa... **1 Yohana 1:4**

*[4] Na haya twayaandika, ili furaha yetu itimizwe.*

Hawa wana USHIRIKA na Baba na wana uzima wa milele. Angalia tena **1 Yohana 1:5**

*[5] Na hii ndiyo habari tuliyoisikia kwake, na KUIHUBIRI KWENU, ya kwamba Mungu ni nuru, wala giza lo lote hamna ndani yake.*

Hapa anazungumzia Injili waliyohubiri. **1 Yohana 1:6**

*[6] Tukisema ya kwamba twashirikiana naye, tena tukienenda gizani, twasema uongo, wala hatuifanyi iliyo kweli;*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Kwa sababu ameshatofautisha makundi mawili...

Je hawa ni akina nani? Angalia **1 Yohana 1:7**

*[7] bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote.*

If we walk in the light... **IF... WE... 1 Yohana 1:8**

*[8] Tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo mwetu.*

Mwamini au asiyeamini? Endelea kutafakari...

Sasa twende kwenye **1 Yohana 1:9**

*[9] Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.*

TUKIZIUNGAMA... SISI AKINA NANI?

Sasa angalia anavyotambulisha WAAMINI kwenye waraka HUU... hawaii SISI...

1 YOHANA 1:4 Na haya twayaandika (NINYI)

1 YOHANA 2:1 nawaandikia haya watoto wadogo (NINYI)...

1 YOHANA 2:7 Wapenzi, siwaandikii (NINYI)...

1 YOHANA 2:12-14 (NINYI... Watoto, wababa, vijana)

Hawa akina NINYI NI WAAMINI...

**Sasa akina sisi ni akina nani?**

**1 Yohana 1:6-8** ni wale walioko gizani, wasio na USHIRIKA na Baba na Mwana, wasio na uzima wa milele

Tukirudi mstari wa 7... **1 Yohana 1:7**

*[7] bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote.*

Ameonyesha KUWA MTU HUSAFISHWA KWA DAMU YA YESU, KUKUBALI HILI NI KUENENDA NURUNI, NA HAPO USHIRIKA WA BABA NA MWANA NDIPO ULIPO.

Dhambi yote HUSAFISHWA kwa damu ya Yesu.

Sio kwa kuzikiri! au kuziungama. Bali kuamini mauti yake (Kumwagika kwa hiyo damu)

Kwa mtazamo wa 1 Yohana 1:7 tumeona kuwa dhambi husafishwa kwa kuamini au kukaa katika nuru au kuamini katika damu ya Yesu.

Kwenye King James Version ameandika...

***1Jn 1:9 KJV If we confess our sins, he is faithful and just to forgive us our sins, and to cleanse us from all unrighteousness.***

Kwenye lugha ya Kigiriki ambapo KJV wametafsiri neno kwa neno huwa hawaweki alama kama KOMA (.). Hii ina maana WATAFSIRI NDIYO HUAMUA WAPI WAWEKE "KOMA" kulingana na namna walivyoelewa muktadha.

Halafu pia, mistari haikuwepo kwenye nyaraka hizi bali ziliongezwa karne ya 16. Sawa tukiweka hiyo "koma" mbele ya confess... itasoma.

**If we confess**, he is faithful and just to forgive us our sins, and to cleanse us from all unrighteousness.

Kwa nini? Kwa sababu huko nyuma tumeona "CLEANSING" is not the function of confession of sins but BLOOD. Kusafishwa siyo swala la kukiri au kuungama dhambi bali imani kwa damu ya Yesu.

1 Yohana 1:7 damu ya Yesu inasafisha...

1 Yohana 1:8 wakubali kuwa wana dhambi na wanahitaji kusafishwa...

1 Yohana 1:9 wakirri/wakubali/waungame kwamba damu ya Yesu inasafisha...

Kwa hiyo anawaambia WAKUBALI/KUKIRI ONDOLEO LA DHAMBI LIPATIKANAYO KWA AJILI YA DAMU YAKE ILIYOMWAGIKA.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Kwa sababu hao siyo WAAMINI. NDIYO MAANA WANATAKIWA KUFANYA HIVYO ILI WAJE KATIKA USHIRIKA NA BABA NA MWANA a.k.a KUPATA UZIMA WA MILELE.

Na hii ni kweli kwa sababu Yohana ameandika sehemu kadhaa kama **I Yohana 4:10**

*[10] Hili ndilo pendo, si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba yeye alitupenda sisi, akamtuma Mwanawe kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu.*

### **KIPATANISHO KWA DHAMBI ZETU.**

Angalia na **I Yohana 2:1-2**

*[1] Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akintenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki,*

*[2] naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwengu wote.*

### **KIPATANISHO KWA DHAMBI ZETU.**

Ukiri wetu au ungamo letu au imani yetu au kusema kwetu ni kazi ya msalaba, kazi aliyoifanya SIYO DHAMBI ZETU.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Kukiri dhambi zako HATA UFANYEJE hayo maneno yako hayana uwezo wa kukusafisha na udhalimu wote ISIPOKUWA DAMU YA MWANAYE.

Kuungama au kukiri dhambi inaonekana kwenye

1. Vitabu vya Agano la Kale na sheria za Musa, na
2. Huduma ya Yohana Mbatizaji...

Lakini kitu hicho hakipo Baada ya Yesu Kristo Kufa na kufufuka siyo huduma ya kusanyiko la kiumbe kipyka katika Kristo ambapo MSAMAHANA WA DHAMBI UNAPOKELEWA KWA IMANI TU!

Angalia kwenye baadhi ya vitabu vya Agano la Kale  
*Mambo ya Walawi 5:5*

*[5] kisha itakuwa, hapo atakapokuwa na hatia  
katika mambo hayo mojawapo, ndipo  
ATAKAPOLIUNGAMA jambo hilo alilolikosa;*

*Mambo ya Walawi 16:20-21*

*[20] Naye akiusha kufanya upatanisho kwa ajili  
ya mahali patakatifu, na hema ya kukutania, na  
madhabahu, atamleta yule mbuzi aliye hai.*

*[21] Na Haruni ataweka mikono yake miwili  
juu ya kichwa cha yule mbuzi aliye hai, na  
KUUNGAMA juu yake uovu wote wa wana wa  
Israeli, na makosa yao, naam, dhambi zao zote;  
naye ataziweka juu ya kichwa chake yule mbuzi,*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

*kisha atampeleka aende jangwani kwa mkono  
wa mtu aliye tayari.*

Zaburi 32:5

[5] *Nalikujulisha dhambi yangu,  
Wala sikuuficha upotovu wangu.  
Nalisema, Nitayakiri maasi yangu kwa  
BWANA,  
Nawe ukonisamehe upotovu wa dhambi yangu.*

HUDUMA YA YOHANA MBATIZAJI. (Huyu alikuwa nabii wa mwisho wa Agano la Kale ndiyo maana). Angalia *Mathayo 3:5-6*

[5] *Ndipo walipomwendea Yerusalemu, na  
Uyahudi wote, na nchi zote za kandokando ya  
Yordani;*  
[6] *naye akawabatiza katika mto wa Yordani,  
huku WAKIZIUNGAMA dhambi zao.*

Marko 1:5

[5] *Wakamwendea nchi yote ya Uyahudi, nao  
wa Yerusalemu wote, wakabatizwa katika mto  
wa Yordani, WAKIZIUNGAMA dhambi zao.*

HUDUMA YA AGANO JIPYA SIYO KUUNGAMA DHAMBI BALI KUPOKEA MSAMAHANA WA DHAMBI KWA IMANI.

Baada ya kuona kiuchambuzi ya kuwa Yohana hakumaanisha kuungama dhambi kama njia ya kupata Msamaha wa dhambi ili kuamini au kukiri na kukubali kile alichokifanya Yesu Kristo, sasa hebu tuangalie nyaraka zingine.

Katika nyaraka za mitume hakuna sehemu wamefundisha kukiri dhambi kwa waamini baada ya kukosa wala kukiri dhambi kwa WASIOAMINI ili wasamehewe.

Angalia Paulo alivyoandika... Hapa anaandikwa kwa Watakatifu. **Waefeso 1:1**

*[1] Paulo, mtume wa Kristo Yesu, kwa mapenzi ya Mungu; kwa watakatifu walioko [Efeso] wanaomwamini Kristo Yesu.*

Mstari wa 7 anawaambiaje hao watakatifu? **Waefeso 1:7**

*[7] Katika yeye huyo [YESU], kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake.*

Angalia TUNAO... Kwa hiyo mtu aliywamini Kristo ANAMILIKI MSAMAHA WA DHAMBI. ANAO TAYARI... HATAFUTI... AMESHAPATA...

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Nafikiri "tenses" ziko wazi hapo ni PAST PARTICIPLE TENSE. Ni ownership. WE HAVE FORGIVENESS OF SINS.

Kwenye Watakatifu walioko Kolosai... *Wakolosai 1:1-2*

- [1] *Paulo, mtume wa Kristo Yesu kwa mapenzi ya Mungu, na Timotheo, ndugu yetu,*
- [2] *kwa ndugu watakatifu, waaminifu katika Kristo, walioko Kolosai. Neema na iwe kwenu, na amani, zitokazo kwa Mungu Baba yetu.*

Anawaambiaje? *Wakolosai 1:14*

- [14] *ambaye katika yeye [YESU] tuna ukombozi, yaani, msamaha wa dhambi;*

ANGALIA "TUNA" hii siyo kujikweza ni kumheshimu Mungu... ni kujiona kwa namna anavyokuona "TUNA UKOMBOZI YAANI MSAMAHWA WA DHAMBI"  
WE HAVE... NI ABSOLUTE. Hakuna chenga labda uamue kujichenga mwenyewe!

WASIOAMINI WANAKIRI NINI?

WHAT DO THEY CONFESS? *Warumi 10:8-10*

- [8] *Lakini yanenaje? Lile neno li karibu nawe, katika kinywa chako, na katika moyo wako; yaani, ni lile neno la imani tulihubirilo.*
- [9] *Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

*mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu,  
utaokoka.*

*[10] Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata  
kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata  
wokovu.*

Kama unakumbuka maana ya neno kukiri... ni kuamini, ni kukubali, kuwa na usemi mmoja kuwa (kwa muktadha huu) Kristo alifufuka katika wafu... ANAOKOKA.

Hapa hakuna kukiri dhambi yake... ni kukubali kuwa Yesu alifufuka kwa ajili yake...

Kwa nini? Kwa sababu **Warumi 4:23-25**

*[23] Walakin haikuandikwa kwa ajili yake tu  
kwamba ilihesabiwa kwake;*

*[24] bali na kwa ajili yetu sisi mtakao hesabiwa  
vivyo hivyo, sisi tunaomwamini yeye  
aliyemfufua Yesu Bwana wetu katika wafu;*

*[25] ambaye alitolewa kwa ajili ya makosa yetu,  
na kufufuliwa ili mpate kuhesabiwa haki.*

Yaani UNAKUBALI KUWA ALIKUFA NA MAKOSA YAKO. Alifufuka (maana yake ameshinda nafasi yako) kwa ajili yako ili wewe UITWE MWENYE HAKI bila kufanya kitu chochote. Yohana naye anaandika juu ya KUKIRI. **1 Yohana 4:1-3**

*[1] Wapenzi, msiiamini kila roho, bali zijaribuni  
hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu; kwa*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

*sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani.*

*[2] Katika hili mwamjua Roho wa Mungu; kila roho ikiriyo kwamba Yesu Kristo amekuja katika mwili yatokana na Mungu.*

*[3] Na kila roho isiyomkiri Yesu haitokani na Mungu. Na hii ndiyo roho ya mpinga Kristo ambayo mmesikia kwamba yaja; na sasa imekwisha kuwako duniani.*

HAPO KUNA KUKIRI KUWA YESU ALIKUJA KATIKA MWILI.

Akarudia tena kwenye *1 Yohana 4:15*

*[15] Kila akiriye ya kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu, Mungu hukaa ndani yake, naye ndani ya Mungu.*

KUKIRI KUWA YESU NI MWANA WA MUNGU.

Kwenye waraka wake wa *2 Yohana 1:7*

*[7] Kwa maana wadanganyifu wengi wametokea duniani, wasiokiri ya kuwa Yesu Kristo yuaja katika mwili. Huyo ndiye yule mdanganyifu na mpinga Kristo.*

Kukiri kuwa Yesu alikuja katika mwili.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

UKICHANGANYA WARUMI NA YOHANA  
UNAONA KUKIRI YESU NA KAZI YAKE YA  
**UKOMBOZI** na si vinginevyo!

Paulo anaendelea kwenye Warumi **14:11**

*[11] Kwa kuwa imeandikwa, Kama niishivyo,  
anena Bwana, kila goti litapigwa mbele zangu;  
Na kila ulimi utamkiri Mungu.*

UTAMKIRI MUNGU...

*Wafilipi 2:10-11*

*[10] ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu  
vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya  
nchi;*

*[11] na kila ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTO  
NI BWANA, kwa utukufu wa Mungu Baba.*

UKIANGALIA MAZINGIRA YOTE YA UKIRI NI  
KUMKIRI YESU KATIKA KAZI YAKE YA  
UKOMBOZI. Kulingana na Warumi **10:9-10**

*[9] Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa  
chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni  
mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu,  
utaokoka. [10] Kwa maana kwa moyo mtu  
huamini hata kupata haki, na kwa kinywa  
hukiri hata kupata wokovu.*

Ni sahihi kusema IMANI IONDOAYO DHAMBI AU IKUPAYO MSAMAHA WA DHAMBI ni kukubali **moyoni** mwako na kukiri kwa kinywa chako kazi ya Ukombozi katika Kristo Yesu. Bila hiyo, dhambi yako inakaa hata kama unalia kwa machozi na kugaragara chini... Ndiyo maana Yesu aliagiza kabisa... **Luka 24:46-47**

*[46] Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu;*

*[47] na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu.*

Toba kwa maana ya kuamini au wamgeukie Mungu na kuamini kazi hiyo ya kufufuka kisha Wapokee Msamaha wa Dhambi.

YAANI MAHUBIRI YAO NI RAHISI KABISA.  
Mfano:

**MHUBIRI:** YESU AMEKUFA NA KUFUFUKA ILI WEWE USAMEHEWE DHAMBI ZAKO KWA AJILI YAKE.

**MSIKILIZAJI:** KUMBE, AISEE NAPOKEA.

**MHUBIRI:** SASA WEWE NI MTAKATIFU.  
IMEISHA HIYO.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Ijapokuwa somo linaweza kuwa refu (na maelezo ya kutosha) ila mantiki yake ni rahisi. Angalia Paulo alivyosema kirahisi kabisa... **2 Wakorintho 5:21**

**[21] Yeye [YESU] asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye.**

**HATUWI HAKI YA MUNGU KWA KULIA au KUUNGAMA DHAMBI... BALI KWA KUAMINI KUWA YEYE YESU ALIFANYIKA DHAMBI ILI MIMI NIWE HAKI TENA NI HAKI YA MUNGU.**

*SIMPLE.*

Ni RAHISI mpaka unaweza kudhani si kweli. Lakini ndiyo kweli kuu. Ila kwa sababu watu wamezoea kusikia UONGO MGUMU wanapata shida kusikia na kukubali KWELI RAHISI. Hii ni rahisi kwetu lakini gharama yake ni Uhai wa Kristo. Haleluya.

NDIYO MAANA NI UPENDO WA MUNGU ULIO WA AJABU SANA.

Tumeshaona kinagaubaga kuwa kwenye nyaraka hakuna sehemu mitume walifundisha KUUNGAMA DHAMBI kama njia au sababu ya Mungu kusamehe dhambi. Tumeona ya kuwa kukiri au kukubali au kutii kazi ya

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Ukombozi kwa njia ya Yesu Kristo ndiyo namna pekee ya mtu ya KUPOKEA (SIYO KUOMBA) Ondoleo la Dhambi.

Tunaona Yesu kwenye mafundisho yake ya mwisho baada ya kufufuka akiwaagiza wanafunzi wake wafundishe... NARUDIA TENA... wafundishe... ONDOLEO LA DHAMBI. Siyo wawaombeshe watu... WAHUBIRI AU WAFUNDISHE...

Angalia... **Luka 24:46-47**

*[46] Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu;*

*[47] na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalem.*

Shida ni kwamba mara nyingi watu wakiona neno toba... akili zao zinawaza maombi. Hebu tuangalia haya maneno...

**Toba** English ni **REPENTANCE**. (KJV)

**Ondoleo** English ni **REMISSION**. (KJV)

Toba/repentance kwenye **Luka 24:47** ni neno la Kigiriki “*metanoea*” lenye maana rahisi ya “**KUBADILI FIKRA AU MTAZAMO**”.

Neno **Metanoia** limeundwa na maneno mawili...

**Meta**... with, after, behind. (baada ya....)

**noieō**.... to perceive with mind, think upon, heed, ponder, consider. (kujua, kutafakari, kufikiri kwa makini, kujali ..)

Ni sawa na kusema PONDERING AFTER, CONSIDERING...

Ukiangalia haya Maneno... TOBA NI JAMBO LINALOFANYIKA KATIKA UFAHAMU. UFAHAMU UNAATHIRIWA NA TAARIFA.. Kwa hiyo hili ni BADILIKO linalotokana na taarifa fulani kusikika na kufanyiwa kazi. Hapa hakuna maombi.

Kwa muktadha huu toba ni maamuzi unayofanya kuanzia ndani baada ya kusikia INJILI au habari za Ondoleo la dhambi kwa kufufuka kwa Yesu Kristo. MAAMUZI HAYO YANAITWA KUAMINI AU KUWA NA IMANI. Ni sawa kabisa na kusema "ANHAA KUMBE, DAAAHH, SIKUJUA, KUMBE ALICHUKUA DHAMBI ZANGU. AHSANTE YESU..."

Kusema hivyo au namna kama hiyo mtu huyo anakuwa amepokea Msamaha wa dhambi.

Neno la pili ni ONDOLEO AU REMISSION... Ni neno la Kigiriki “*aphesis*” likiwa na maana ya

1. release from bondage or imprisonment
2. forgiveness or pardon, of sins (letting them go as if they had never been committed), remission of the penalty.

Hapa unaona vitu viwili... KUACHWA HURU na ya pili ni KUACHILIWA KAMA VILE HUJAWAHI KUFANYA KOSA LOLOTE.

**Toba anafanya MHUBIRIWA... NA ONDOLEO ANAFANYA YESU...**

Kwa hiyo kutubu ni KUPOKEA ALICHOKIFANYA Yesu Kristo... na mahubiri ni kusema alichokifanya Yesu ili mtu abadili fikra zake jinsi anamvyomtazama Yesu... amuone mwenye kumuondolea dhambi au kumweka huru mbali na dhambi.

Swali linabaki... baada ya agizo hilo la Yesu Kristo, je, mitume walitii?

Kwenye mahubiri yao kulikuwa na KUHUBIRI ONDOLEO LA DHAMBI?

Mahubiri ya kwanza kabisa ya Petro kwenye *Matendo ya Mitume 2:14,22-24,32,37-38*

*[14] Lakini Petro akasimama pamoja na wale kumi na mmoja, akapaza sauti yake,*

*akawaambia, Enyi watu wa Uyahudi, na ninyi nyote mkaao Yerusalem, lijueni jambo hili, mkasikilize maneno yangu.*

[22] *Enyi waume wa Israeli, sikilizeni maneno haya: Yesu wa Nazareti, mtu aliyedhihirishwa kwenu na Mungu kwa miujiza na ajabu na ishara, ambazo Mungu alizifanya kwa mkono wake kati yenu, kama ninyi wenyewe mnavyojua;*

[23] *mtu huyu alipotolewa kwa shauri la Mungu lililokusudiwa, na kwa kujua kwake tangu zamani, ninyi mkamsulibisha kwa mikono ya watu wabaya, mkamwua;*

[24] *ambaye Mungu alimfufua, akiufungua uchungu wa mauti, kwa sababu haikuwezekana ashikwe nao.*

[32] *Yesu huyo Mungu alimfufua, na sisi sote tu mashahidi wake.*

[37] *Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, Tutendeje, ndugu zetu?*

[38] *Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Unaweza ukasoma yote uone Petro alivyokuwa anachambua ahadi ya Ukombozi wa mwanadamu kwenye maandiko ya Agano la Kale...

Bila shaka umeona ya kuwa alifundisha habari ya MATESO, KUFA NA KUFUFUKA KWA YESU KRISTO. Na alipoulizwa TUFANYEJE? Petro akajibu **Tubuni** mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, **mpate ondoleo la dhambi zenu.**

Yale maneno aliyojasema Yesu Kristo TOBA NA ONDOLEO LA DHAMBI yanatumiwa na Petro kwamba WATUBU ILI WAPATE ONDOLEO LA DHAMBI.

Tafadhali usisahau maana ya KUTUBU tuliyojifunza huko juu. Ina maana wasiendelee kumwona Yesu Kristo kama mtoto wa fundi seremala bali BWANA NA KRISTO au mwenye uwezo wa kuondoa dhambi zao...

### **Angalia Matendo ya Mitume 2:36**

*[36] Basi nyumba yote ya Israeli na wajue yakini ya kwamba Mungu amemfanya Yesu huyo mliyensulibisha kuwa Bwana na Kristo.*

Baadaye tena Petro akiwa na Yohana alihubiri tena walipomponya kiwete na watu kukusanyika. ***Matendo ya Mitume 3:12,14-19***

[12] *Hata Petro alipoyaona haya akawajibu wale watu, Enyi Waisraeli, mbona mnastaajabia haya, au mbona mnatukazia macho sisi, kana kwamba tumemfanya huyu aende kwa nguvu zetu sisi, au kwa utauwa wetu sisi?*

[14] *Bali ninyi mlimkana yule Mtakatifu, yule Mwenye haki, mkataka mpewe mwuaji;*

[15] *mkamwua yule Mkuu wa uzima, ambaye Mungu amemfufua katika wafu; na sisi tu mashahidi wake.*

[16] *Na kwa imani katika jina lake, jina lake limemtia nguvu mtu huyu mnayemwona na kumjua; na imani ile iliyo kwake yeye imempatia huyu uzima huu mkamilifu mbele yenu ninyi nyote.*

[17] *Basi sasa, ndugu, najua ya kuwa mliyatenda haya kwa kutokujua kwenu, kama na wakuu wenu walivyotenda.*

[18] *Lakini mambo yale aliyohubiri Mungu tangu zamani kwa kinywa cha manabii wake wote, ya kwamba Kristo wake atateswa, ameyatimiza hivyo.*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

**[19] Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana**

Angalia alivyosema TUBUNI basi, MREJEE, ili DHAMBI ZENU ZIFUTWE. Hapa ametumia KUFUTA badala ya **kuondoa...** neno kufutwa na kuondoa zote zina maana ya kuzifanya zisiwepo tena.

Petro alipofika nyumbani kwa Kornelio alihubiri nini?  
Angalia... *Matendo ya Mitume 10:34,39-43*

**[34] Petro akafumbua kinywa chake, akasema,  
Hakika natambua ya kuwa Mungu hana  
upendeleo;**

**[39] Nasi tu mashahidi wa mambo yote  
aliyoyatenda katika nchi ya Wayahudi na katika  
Yerusalem; ambaye walimwua wakamtundika  
mtini.**

**[40] Huyo Mungu alimfufua siku ya tatu,  
akamjalia kudhahirika,**

**[41] si kwa watu wote, bali kwa mashahidi  
waliokuwa wamekwisha kuchaguliwa na  
Mungu, ndio sisi, tulio kula na kunywa pamoja  
naye baada ya kufufuka kwake kutoka kwa  
wafu.**

**[42] Akatu agiza tuwahubiri watu na  
kushuhudia ya kuwa huyu ndiye aliye amriwa**

*na Mungu awe Mhukumu wa walio hai na wafu.*

*[43] Huyo manabii wote humshuhudia, ya kwamba kwa jina lake kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi.*

Petro ameeleza kufu na kufufuka kwake kisha matokeo yake... na MAAGIZO ya Yesu Kristo kuwa TUWAHUBIRI WATU na KUSHUHUDIA ya kuwa HUYU (YESU) ndiye aliyeamriwa na Mungu awe Mhukumu wa walio hai na wafu.

Yesu anatoa HUKUMU GANI? PETRO ANASEMA "Huyo manabii wote humshuhudia, ya kwamba kwa jina lake kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi." UMEONA TOBA badala ya "AMWAMINIYE".

Tubu, Tubu, Tubu, hapa ametumia AMINI. (Hakuna kilichobadilika "kutubu ni kuamini"). Kwa hiyo kutubu ni kuamini kwamba KWA NJIA YA KUFA NA KUFUFUKA KWA YESU KRISTO NIMEPATA ONDOLEO LA DHAMBI.

### **TOBA NI KUAMINI.**

Angalia Paulo alivyohubiri ujumbe huo huo. Ina maana Paulo (ambaye hakuwa na Yesu Kristo kama mwanafunzi katika wale Thenashara alielewa UJUMBE

WA INJILI). ANGALIA... *Matendo ya Mitume*  
*13:16,27-30,32-39*

[16] *Paulo akasimama, akawapungia mkono, akasema, Enyi waume wa Israeli, nanyi mnaomcha Mungu, sikilizeni.*

[27] *Kwa maana wakao Yerusalem, na wakuu wao, kwa kuwa hawakumjua yeye, wala maneno ya manabii yanayosomwa kila sabato, wameyatimiza kwa kumhukumu.*

[28] *Na ijapokuwa hawakuona sababu ya kumfisha wakamwomba Pilato auawe.*

[29] *Hata walipokwisha kumaliza yote aliyoandikiwa, wakamtelemsha katika ule mti, wakamweka kaburini.*

[30] *Lakini Mungu akamfufua katika wafu;*

[32] *Na sisi tunawahubiri habari njema ya ahadi ile waliyopewa mababa,*

[33] *ya kwamba Mungu amewatimizia watoto wetu ahadi hiyo, kwa kumfufua Yesu; kama ilivyoandikwa katika Zaburi ya pili,*

*Wewe ndiwe Mwanangu, mimi leo nimekuzaa.*

[34] *Tena ya kuwa alimfufua katika wafu, asipate kurudia uharibifu, amenena hivi,*

*Nitawapa ninyi mambo matakatifu ya Daudi yaliyo amini.*

[35] *Kwa hiyo anena na pengine,*

*Hutamwachia Mtakatifu wako kuona uharibifu.*

[36] *Kwa maana Daudi, akiisha kulitumikia shauri la Mungu katika kizazi chake, alilala, akawekwa pamoja na baba zake, akaona uharibifu.*

[37] *Bali huyu aliyefufuliwa na Mungu hakuona uharibifu.*

[38] *Basi, na ijulikane kwenu, ndugu zangu, ya kuwa kwa huyo mnahubiriwa msamaha wa dhambi;*

[39] *na kwa yeye kila amwaminiye huhesabiwa haki katika mambo yale yote asiyoweza kuhesabiwa haki kwa torati ya Musa.*

Kama Petro alivyofanya, yeye pia anaonyesha kuwa YESU ALIKUFA NA KUFUFUKA... KWA HUYO (YESU) WANAHUBIRIWA MSAMAHANA WA DHAMBI. YAANI MSAMAHANA NI MAHUBIRI SIYO MAOMBI AU KINGINE. BAADA YA MAHUBIRI WATU HUAMINI AU KUPOKEA AU KUTUBU NA HIVYO KUPOKEA.

Jambo la kuona hapa ni kwamba Paulo ametuongzea MSAMIATI kwamba **KILA AMWAMINIYE "HUHESABIWA HAKI"**. Tumeona msamiati ambao Paulo ametuongzea wakati anazungumza juu ya Msamaha wa dhambi. Angalia **Matendo ya Mitume 13:38-39**

*[38] Basi, na ijulikane kwenu, ndugu zangu, ya kuwa kwa huyo mnahubiriwa msamaha wa dhambi;*

*[39] na kwa yeye kila amwaminiye huhesabiwa haki katika mambo yale yote asiyoweza kuhesabiwa haki kwa torati ya Musa.*

Sasa Paulo anasema... KWA HUYO (YESU ALIYEKUFA NA KUFUFUKA) MNAHUBIRIWA MSAMAHANA WA DHAMBI... NA KWA KILA AMWAMINIYE HUHESABIWA HAKI KATIKA MAMBO YALE YOTE ASIYOWEZA KUHESABIWA HAKI KWA TORATI YA MUSA.

Haya siyo mambo mawili ni jambo moja... MSAMAHANA WA DHAMBI NA KUHESABIWA HAKI ni kitu kimoja.

Kwa version za Kingereza *Act 13:39 KJV; And by (JESUS) him all that believe are JUSTIFIED from all things, from which ye could not be JUSTIFIED by the law of Moses.*

Maneno KUHESABIWA HAKI kwa King James version wametumia neno moja JUSTIFIED (JUSTIFY). Kwenye Matendo 13:39 neno la Kigiriki lilitumika ni *dikaioō* lenye maana ya kumtangazia mtu kama anayo haki, it's a declaration. Ni lugha ya Kimahakama.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Hapa maana yake mtu anatangaziwa kwamba Yuko sawa wala hana mawaa mbele za Mungu kwa sababu tu AMEMWAMINI YESU KRISTO... katika kazi yake ya ukombozi.

Kwa hiyo KUHESABIWA HAKI NI PALE AMBAPO MWENYE DHAMBI ANATANGAZIWA KWAMBA HANA DHAMBI.

NI KUTANGAZIWA KUWA HUNA DHAMBI. NI KAZI YA YULE ANAYETANGAZA. NI UWEZO NA NGUVU ZAKE. WEWE KAZI YAKO NI KUAMINI TANGAZO LAKE.

**The Guilty is justified Holy! Glory to God.**

Sasa haya mambo ya KUHESABIWA HAKI Paulo ameyazungumza sana kwenye Waraka wa Paulo kwa Warumi. Tuangalie... *Warumi 5:1-2*

*[1] Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na mwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo,*

*[2] ambaye kwa yeye tumepata kwa njia ya imani kuifikia neema hii ambayo mnasimama ndani yake; na kufurahi katika tumaini la utukufu wa Mungu.*

Ukisoma maneno haya ya Waraka wa Paulo ni kama anaagiza kuwepo na amani kwa Mungu lakini ukisoma kwenye KJV **Rom 5:1 KJV Therefore being justified by faith, we have peace with God through our Lord Jesus Christ:** Kwenye KJV anatumia wakati uliopo timilifu AMANI NA MUNGU (**WE HAVE PEACE**) kwa sababu tumeweka imani yetu kwa Kristo hatusimami wakati wowote na hofu mbele za Baba yetu.

Ukipotezea kuanza sura ya 5:1 na kurudi nyuma utaona sababu ya kuhesabiwa haki... Angalia mstari wa mwisho wa Warumi 4 yaani **Warumi 4:25**

*[25] ambaye (KRISTO) alitolewa kwa ajili ya makosa yetu, na kufufuliwa ili mpare kuhesabiwa haki.*

Kuhesabiwa haki ni matokeo ya kuamini katika kufa (kwa ajili ya makosa yako) na kufufuka (ili uhesabiwe haki) kwa Yesu Kristo.

Kuamini katika kufa na kufufuka kwa Yesu Kristo ndiyo KIGEZO pekee cha kuhesabiwa haki.

Paulo anaandika pia, **Warumi 4:6-8**

*[6] Kama vile Daudi aunenavyo uheri wake mtu yule ambaye Mungu amhesabia kuwa na haki pasipo matendo,*

*[7] Heri waliosamehewa makosa yao,*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

***Na waliositiriwa dhambi zao.***

**[8] Heri mtu yule ambaye Bwana hamhesabii dhambi.**

Hii inaonyesha kuwa haki haipatikani kwa matendo (yaani kile anachokifanya mtu ili Mungu afanye) bali kwa kuamini au kukubali KUPOKEA kama zawadi kutoka kwa Mungu.

Vivyo hivyo anawaita WALIOSITIRIWA DHAMBI ZAO AU AMBAO HAWAHESABIWI DHAMBI. Maneno haya Paulo aliyachukua kwenye **Zaburi 32:1-2**

**[1] Heri aliyesamehewa dhambi,**

***Na kusitiriwa makosa yake.***

**[2] Heri BWANA asiyemhesabia upotovu,**

***Ambaye rohoni mwake hamna hila.***

Hii inaonyesha kuwa swala la Mungu kumhesabia mtu haki siyo swala mtambuka... Daudi aliona na kutabiri juu ya ahadi hiyo kwa kila amwaminiye Yesu Kristo.

Daudi anasema rohoni mwake hakuna hila ni sawa na kusema rohoni mwako kuko sawa... hana udanganyifu (guile) au KUTOAMINI.

Angalia Paulo alivyoandika kwenye... **Warumi 3:21-26**

*[21] Lakini sasa, haki ya Mungu imedhahirika pasipo sheria; inashuhudiwa na torati na manabii;*

*[22] ni haki ya Mungu iliyo kwa njia ya imani katika Yesu Kristo kwa wote waaminio. Maana hakuna tofauti;*

*[23] kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu;*

*[24] wanahesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu;*

*[25] ambaye Mungu amekwisha kumweka awe upatanisho*

*kwa njia ya imani katika damu yake, ili aonyeshe haki yake, kwa sababu ya kuziachilia katika ustahimili wa Mungu dhambi zote zilizotangulia kufanywa;*

*[26] apate kuonyesha haki yake wakati huu, ili awe mwenye haki na mwenye kumhesabu haki yeye amwaminiye Yesu.*

Torati na manabii zina ujumbe mmoja tu HAKI KWA IMANI... Yaani hakuna mtu atakaehesabiwa haki mbele za Mungu na kuonekana kwamba amestahili uzima wa milele ila KWA IMANI TU yaani KUKUBALI KAZI YA MSALABA (KUFA NA KUFUFUKA KWA YESU KRISTO). KWA HIYO YESU NI MWENYE HAKI (NDIYE ALIYEKUFA NA KUFUFUKA) NA KWA

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

SABABU HIYO YEYE NDIYE MWENYE  
KUMHESABIA HAKI kila ANAYEMWAMINI.

Yeye ndiye upatanisho na anawahesabia watu HAKI BURE (Kazi ya mwanadamu ni KUPOKEA tu haki hiyo). Si ya bure kwamba haina gharama ila kwa sababu anayetoa ni MTOAJI (GENDERous).

*A free gift is not necessarily a cheap gift. It so expensive that no man can match the price and the best thing is the owner to give freely.*

**That's our RIGHTEOUSNESS.  
(Hii ni HAKI YETU KATIKA  
KRISTO)**

*(Syo kweli kwamba kweli kila kitu cha bure hakina thamani, wokovu wetu ni wa gharama sana lakini tumepewa bure)*

Ndiyo maana anaendelea kusema *Warumi* 3:27

*[27] Ku wapi, basi, kujisifu? Kumefungiwa nje.  
Kwa sheria ya namna gani? Kwa sheria ya matendo? La! Bali kwa sheria ya imani.*

Hakuna mwanadamu anayeweza kujisifu juu ya haki ya Mungu kwani haitolewi kwa vigezo vya kibinadamu bali udhihirisho wa upendo wa Mungu. LOVE GIVES.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Anaongeza kwa kusema ***Wagalatia 2:16***

**[16] hali tukijua ya kuwa mwanadamu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria, bali kwa imani ya Kristo Yesu; sisi tulimwamini Kristo Yesu ili tuhesabiwe haki kwa imani ya Kristo, wala si kwa matendo ya sheria; maana kwa matendo ya sheria hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki.**

Hii inafunga kesi kabisa... **HAKUNA MWENYE MWILI KWA MATENDO YA SHERIA AU KUJITAHIDI KUFIKA VIWANGO FULANI ILI AHESABIWE HAKI.**

Paulo anaongeza kwenye ***Wagalatia 2:20-21***

**[20] Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.**

**[21] Siibatili neema ya Mungu; maana, ikiwa haki hupatikana kwa njia ya sheria, basi Kristo alikufa bure.**

Paulo anasimama kuonyesha kuwa MATESO ALIYOPITIA KRISTO NI YA KWAKE, KUFUFUKA

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

KWAKE NI KWA AJILI YAKE wala HAHITAJI tena kufanya jambo lolote ili astahili kuhesabiwa haki.

Anaonyesha ya kuwa Kristo alipata mateso na kushinda MAUTI kwa ajili yake... angalia *2 Wakorintho 5:21*

**[21] *Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye.***

Hii ni sawa na kusema alikaa sehemu ya ADHABU yako ili wewe upate HAKI yake. Alikubali mshahara wako wa MAUTI ili Akupe UZIMA WAKE BURE. Angalia *Warumi 6:23*

**[23] *Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.***

KARAMA (UTOAJI BURE) YA MUNGU NI UZIMA WA MILELE KATIKA KRISTO YESU BWANA WETU. Kila Mwamini anatembea katika uhalisia huo. Anayo haki yenye uzima... yaani Mungu amemkubali na kumpa uzima wake ndani yake bila yeye kufanya chochote ila tu KUAMINI KAZI KUBWA YA UKOMBOZI ULIO KATIKA KRISTO YESU.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

**NDUGU YANGU, UMEHESABIWA NA MUNGU YA  
KUWA UMESTAHILI YALE AMBAYO HUSTAHILI  
KWA SABABU UMEMWAMINI KRISTO YESU.**

*Mimi ni haki ya Mungu,*

*Nimehesabiwa haki,*

*Ninayo amani na Mungu,*

*Nimepatanishwa na Mungu,*

*Ninayo haki ya uzima ndani yangu.*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

# 9

SURA YA

**KAMA TUKIFANYA DHAMBI KUSUDI**



**M**ara nyingi mstari huu huchukuliwa nje ya muktadha kuhakikisha kuwa mtu akifanya "dhambi" kwa kujuu anakuwa amepotea milele. Hii si tu kwamba imewafanya watu waone wokovu kuwa ni jambo lisilowezekana ila pia kuna watu wameamua kuishi katika dhambi baada ya kuona hakuna tumaini tena kwao. Wanashiriki tu siku ya "hukumu" waende katika Jehanamu ya moto milele. Na wale wachache wanaojua kuwa wokovu wa Mungu ni wa milele wala hauwezi kupotea kama shilingi kwenye mchanga wamebaki na maswali... sasa huyu ndugu

alikuwa na maana gani? Kama kanuni ya kusoma maandiko isipofanyiwa kazi lazima kila siku unaibuka na mambo yasiyoleweka, yanayokinzana au ambayo mwandishi hakumaanisha kabisa.

Unaposoma maandiko... usikomalie mstari. Usiunyonge, usitafute maana ya yale yaliyomo ndani yake yenyewe, tafuta kuelewa habari nzima kwenye hili eneo.

Jiulize, Kabla ya kufika hapo alisemaje? (Pretext).

Mbele yake aliendeleaje? (Post-text).

Ukifanya hivyo utaepuka mara nyingi kufanya hitimisho la mambo ambayo MWANDISHI hakumaanisha.

Sijajua kwa nini kwenye kusoma Biblia tunakuwa na haraka. Mbona tukisoma riwaya hatutafuti maana kwenye mstari... badala yake unasema "Enhe ikawaje, unaendelea kufuatilia hadi uelewe?"

Lakini kwenye Biblia sasa... yaani unasoma mstari unaibuka nayo.

"Akainuka Farao asiyemjua Yusufu" Mara unaanza kurukaruka... inawezekana umasikini ni Farao wako... afya... n.k. hivi MWANDISHI alikuwa anawaza kama wewe? Au umeweka maneno yako?

Enewei, sasa tuendelee na Waebrania **10:26**

*[26] Maana, kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Kwenye KJV anasema ***Hebrews 10:26 KJV; For if we sin wilfully after that we have received the knowledge of the truth, there remaineth no more sacrifice for sins,***

IF WE SIN WILFULLY... KAMA TUKIFANYA DHAMBI KUSUDI.

Mambo hapa ya kuangalia ni haya. MWANDISHI anawaita akina nani "TU" TUKIFANYA... "WE" IF WE...

Wakati tunachambua 1 Yohan 1:9... Wakati mwingine MWANDISHI kujijumuisha kwenye kundi fulani la watu na kuwapa tahadahari haina maana moja kwa moja anahuksika na tukio hilo.

Mimi Shemeji Melayeki nikaandika baada ya kusikia kikao cha bunge labda na ripoti ya Wizara ya Fedha halafu nikaandika... "**TUSIPOANGALIA MIPANGO YETU, UCHUMI WA NCHI UTADORORA**".

Wewe unafikiri mimi hapo nahusikaje KWENYE kuangalia? Mimi siyo mtunga sera, mimi siyo mbunge, na siyo waziri au mtu mwenye maamuzi juu ya hali ya uchumi. Ila nimejiweka katika Watanzania wote. Wanaoangalia na Wasioweza KUANGALIA. Sasa ukija kuniambia... **WOTE TUSIPOANGALIA...**

Kwa nini nasema haya...? Kwa sababu... ukiendelea kusoma anawaita waamini kwa nafsi ya 2 wingi (NINYI).

Angalia ***Waebria 13:2***

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

**[2] Msisahau kuwafadhili wageni; maana kwa njia hii wengine wamewakaribisha malaika pasipo kujua.**

MSISAHAU... Hawa ni WAAMINI. YES.  
WASISAHAU KWA SABABU NI ASILI YAO.

Sasa turejee... **Waebrania 10:26**

**[26] Maana, kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi;**

Kwenye WARAKA HUU KWA WAEBRANIA, dhambi gani inazungumziwa? Kweli gani ilipokelewa? Au MWANDISHI ameandika juu ya kweli gani?

Kwa sababu tumeshachambua kitabu cha waraka kwa Waebrania huko nyuma... (*UCHAMBUZI UPO UKITAKA utapata Youtube au nakala laini kwa njia ya Whatsapp au Email*) tumeona ya kuwa kitabu hiki kimejikita kuzungumza kwa NGUVU SANA JUU YA **SADAKA/DHABIHU YA YESU KRISTO.**

Sadaka ya Yesu Kristo imeonyeshwa kuwa sadaka bora zaidi kuliko sadaka zote zilizotolewa katika Agano la Kale.

Turudi nyuma kudogo halafu tuangalie, **Waebrania 7:22-27**

**[22] basi kwa kadiri hii Yesu amekuwa mdhamini wa agano LILIGO BORA ZAIDI.**

**[23] Tena wale walifanywa makuhani wengi, kwa sababu wazuiliwa na mauti wasikae;**

[24] *bali yeye, kwa kuwa AKAA MILELE, anao UKUHANI WAKE USIOONDOKA.*

[25] *Naye, kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana YU HAI SIKUZOTE ILI AWAOMBEE.*

[26] *Maana ilitupasa sisi tuwe na kuhani mkuu wa namna hii ALIYE MTAKATIFU, ASIYEKUWA NA UOVU, ASIYEKUWA NA WAA LO LOTE, ALIYETENGWA NA WAKOSAJI, ALIYEKUWA JUU KULIKO MBINGU;*

[27] *ambaye HANA HAJA KILA SIKU, mfano wa wale makuhani wakuu wengine, kwanza kutoa dhabihu kwa ajili ya dhambi zake mwenyewe, kisha kwa ajili ya dhambi za hao watu; MAANA YEYE ALIFANYA HIVI MARA MOJA, ALIPOJITO NAFSI YAKE.*

Umeona Ubora wa SADAKA YA YESU KRISTO?

Twende mbele kidogo. *Waebrania 9:11-14,24-26,28*

[11] *Lakini Kristo akiisha kuja, aliye kuhani mkuu wa mambo mema yatakayokuwapo, kwa hema iliyo kubwa na kamilifu zaidi, isiyofanyika kwa mikono, maana yake, isiyo ya ulimwengu huu,*

[12] *wala si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika Patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele.*

[13] *Kwa maana, ikiwa damu ya mbuzi na mafahali na majivu ya ndama ya ng'ombe waliyonyunyiziwa wenyewe uchafu hutakasa hata kuusafisha mwili;*

[14] *basi si zaidi damu yake Kristo, ambaye kwamba kwa Roho wa milele alijittoa nafsi yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na mawaa, itawasafisha dhamiri zenu na matendo mafu, mpate kumwabudu Mungu aliye hai?*

[24] *Kwa sababu Kristo hakuingia katika patakatifu palipofanyika kwa mikono, ndio mfano wa patakatifu halisi; bali aliingga mbinguni hasa, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu;*

[25] *wala si kwamba ajitoe mara nyangi, kama vile kuhani mkuu aingiavyo katika patakatifu kila mwaka kwa damu isiyo yake;*

[26] *kama ni hivyo, ingalimpasa kuteswa mara nyangi tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu; lakini sasa, mara moja tu, katika utimilifu wa nyakati, amefunuliwa, azitangue dhambi kwa dhabihu ya nafsi yake.*

[28] *kadhalika Kristo naye, akiisha kutolewa sadaka mara moja azichukue dhambi za watu wengi; atatokea mara ya pili, pasipo dhambi, kwa hao wamtazamiao kwa wokovu.*

AMETOLEWA SADAKA MARA MOJA, MAANA YAKE HAKUNA NYINGINE... ONCE AND FOR ALL. Angalia tena mbele yake... **Waibrania 10:10-14**

*[10] Katika mapenzi hayo mmepeata utakaso, kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja tu.*

*[11] Na kila kuhani husimama kila siku akifanya ibada, na kutoa dhabihu zile zile mara nyingi; ambazo haziwezi kabisa kuondoa dhambi.*

*[12] Lakini huyu, alipokwisha kutoa kwa ajili ya dhambi dhabihu moja idumuyo hata milele, aliketi mkono wa kuume wa Mungu;*

*[13] tangu hapo akingojea hata adui zake wawekwe kuwa chini ya miguu yake.*

*[14] Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa.*

Angalia maneno... KWA TOLEO MOJA.... (MAANA YAKE HAKUNA LINGINE).

Sasa utaelewa kwa nini kwenye mstari wa 26 anasema **HAIBAKI TENA DHABIHU KWA AJILI YA DHAMBI...** Kwa sababu iko moja tu nayo ni KRISTO na wao wameikataa... huko KUKATAA NI **KUFANYA DHAMBI KUSUDI.**

Baada ya kuhubiriwa juu ya sadaka ya Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi kisha WAKAKATAA... Hawana option B. NI KRISTO TU.

Kwa hiyo hawa watu, ni wale waliohubiriwa tangu Waembrania 1 na bado wanashupaza shingo. Siyo waamini kabisa.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Post text inasemaje? Mbele mwandishi anaandika nini?  
Angalia **Waebrania 10:27**

*[27] bali kuna kuitazamia hukumu yenyekutisha, na ukali wa moto ulio tayari kuwala wao wapingao.*

Angalia mwandishi anavyowaita... **WAPINGAO.**

Hii ina maana mstari wa 26 unahusu, waliosikia kisha wakakataa au wakapinga habari za ukombozi kwa sadaka ya Yesu Kristo iliyo bora dhidi ya sadaka za wanyama.

Hawa ni watu WAPINGAO ujumbe uliopo tangu Waebrania 1 hadi 10... KRISTO NA WOKOVU WAKE. Hawa siyo watu wenye tabia zisizoendana na mwenendo wa kikristo... siyo wazinzi, wala **wezi, walevi** au waongo au wanaofanana na hao. Hapana.

Hizo zote siyo tabia nzuri wala Injili ya Yesu Kristo haiwapigii makofi watu watendao mambo kama hayo... lakini hawaitwi WAPINGAO... Wapingao wapo hata leo... wanaoukataa Msamaha wa bure katika Kristo Yesu na kutafuta kusamehewa kwa jitihada zao. Wanakesha usiku na mchana wasamehewe, bado wanambembeleza Mungu kwa machozi mengi awasamehe... hawaamini kama sadaka ya Yesu Kristo ilimaliza... wako kwenye mafoleni wanaungama na kukiri dhambi zao ili pengine wasamehewe. Wanatoa sadaka za wanyama au fedha ili Mungu awatazame na kuwasamehe... hawa wanaidharau kazi ya Kristo.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

**Msamaha wa dhambi unapokelewa bure na  
mwanadamu.**

**Jitihada zako hazifui dafu.**

**It's free but costly.**

It took Jesus Christ death and resurrection for you to obtain freely.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

# SURA YA 10

***ISIWE NIKIISHA KUWAHUBIRI  
WENGINE, MWENYEWE NIWE MTU WA  
KUKATALIWA***



**K**ama kweli WOKOVU ni wa milele kwa nini Paulo aliandika maneno haya? Au alimaanisha nini kwenye Waraka wa Kwanza kwa Wakorintho 9:27? *1 Wakorintho 9:27 [27] bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha; isiwe, nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa.*

**Mstari huu** ni kati ya mistari mingi kwenye Biblia inayochukuliwa kuwatishia na kuwahakikishia wakristo kuwa watapoteza wokovu. Wengi huenda mbali sana kwa kutumia mstari huu kujitesa, kufunga bila sababu yoyote au kulala porini (siyo kwa sababu anaomba) ila tu aweze kuutumikisha mwili wake kwa kuutesa ILI MUNGU ASIJE KUMKATAA...

**Hii iko mbali na kweli kabisa...**

Kwanza kabisa kuna ushahidi wa kutosha kuwa Mungu hatukubali kwa sababu tunajitesa ila ni kwa sababu ya kazi kubwa sana ya ukombozi katika Mwanaye.

**Tito 3:4-7**

- [4] *Lakini wema wake Mwokozi wetu Mungu, na upendo wake kwa wanadamu, ulipofunuliwa, alituokoa;*
- [5] *SI KWA SABABU YA MATENDO YA HAKI TULIYOYATENDA SISI; bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu;*
- [6] *ambaye alitumwagia kwa wingi, kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu;*
- [7] *ILI TUKIHESABIWA HAKI KWA NEEMA YAKE, tupate kufanywa WARITHI wa uzima wa milele, kama lilivyo tumaini letu.*

Angalia pia na **Waefeso 2:8-9**

*[8] Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo HAIKUTOKANA NA NAFSI ZENU, NI KIPAWA CHA MUNGU;*

*[9] wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.*

Mtu yejote anayelipia WOKOVU kwa jitihada zake huo sio WOKOVU. Wala hakuna anayehesabiwa haki ama kupokea msamaha wa dhambi kwa kujitesa au kuingia katika ufalme wa Mungu kwa taabu yake mwenyewe. Mchango mkubwa anaoupeleka mwenye dhambi kwa Mungu kwa ajili ya dhambi zake ni hizo dhambi zake, ili akaokolewe.

### **SASA PAULO ALIKUWA ANAMAANISHA NINI?**

1. *Jambo la kwanza la muhimu kabisa unaposoma maandiko Matakatifu, ni kuacha papara. Usiseme vitu kichwani mwako. Hapo hakuna mambo ya "mimi nahisi anamaanisha hivi au vile" acha mwandishi akufundishe alichokusudia.*

2. *Jambo la pili ni kwamba Biblia haijipingi, haiwezi kusema ndiyo hapa na hapana pale kwa jambo lile lile... hivyo inahitaji umakini kujua mwandishi alimaanisha*

*nini. Ukiona Biblia inajipinga ni kwa sababu ufahamu wako haujang'amua kilichoandikwa.*

*3. Jambo la tatu ni muktadha: kujua habari ilipoanza na pengine ilipoishia. Juu ya huo mstari mwandishi alisema nini na chini ya huo mstari alisema nini. Hakuna mtu anayetafsiri lengo la barua nzima kwa kusoma mstari mmoja tu. Mstari unaelezea kwenye sura na mstari hauwezi kuwa kisiwa kwenye sura nzima.*

*4. Jambo la nne, kile alichokisema kinakubaliana na sehemu zingine za Biblia? Au imekaa kama kisiwa? Kumbuka: Kwa vinywa vyta mashahidi wawili au watatu kila neno lithibitike (**Kutoka 17:6**, **Kutoka 19:15**, **Mathayo 18:16**, **2 Wakorintho 13:1**, **1 Timotheo 5:19** na **Waebrania 10:28**).*

*5. Jambo la tano: Ujizoeze kupitia hata tafsiri nyingine zitakusaidia kuona kwenye lugha nyingine namna walivyoandika au version nyingine ya Biblia wameandikaje... kuliko kuishia kusema mambo ambayo hayakutakiwa kusemwa kwa sababu ya kutokuwa makini katika kujifunza.*

UKIJIZOEZA      KUFANYA      MAMBO      HAYO  
MATANO, NI NGUMU SANA KUANGUKIA  
KWENYE MAFUNDISHO POTOFU.

Sasa tuangalie **1 Wakorintho 9:27**

[27] *bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha; isiwe, nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa.*

Sasa tuangalie kwenye muktadha Paulo alikuwa anazungumzia mambo gani?

Mjadala unaanza kwa Paulo kuonyesha haki aliyonayo kama mtume kwa Wakorintho...

Angalia **1 Wakorintho 9:7-9**

[7] *Ni askari gani aendaye vitani wakati wo wote kwa gharama zake mwenyewe? Ni nani apandaye mizabibu asiyekula katika matunda yake? Au ni nani achungaye kundi, asiyekunywa katika maziwa ya kundi?*

[8] *Je! Ninanena hayo kwa kibinadamu? Au torati nayo haisemi yayo hayo?*

[9] *Kwa maana katika torati ya Musa imeandikwa, Usimfunge kinywa ng'ombe apurapo nafaka. Je! Hapo Mungu aangalia mambo ya ng'ombe?*

Anatumia torati kufundisha umuhimu wa kuwategemeza wahudumu wa Injili. Anasema hiyo ni haki yake.

Anakazia mistari inayofuata... **1 Wakorintho 9:10-11**

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

**[10] Au yamkini anena hayo kwa ajili yetu? Naam, yaliandikwa kwa ajili yetu; kwa kuwa alimaye nafaka ni haki yake kulima kwa matumaini, naye apuraye nafaka ni haki yake kutumaini kupata sehemu yake.**

**[11] Ikiwa sisi tuliwapandia ninyi vitu vyatuhonni, je! Ni neno kubwa tukivuna vitu vyenu vyatuhonni mwilini?**

Mambo ni yale yale... Kuwategemeza WAHUDUMU wa Injili.

**Angalia 1 Wakorintho 9:12**

**[12] Ikiwa wengine wanashiriki uwezo huu juu yenu, sisi si zaidi? Lakini hatukuutumia uwezo huo; bali twayavumilia mambo yote tusije tukaizuia Habari Njema ya Kristo.**

Angalia maneno haya... LAKINI HATUKUUTUMIA UWEZO HUO; BALI TWAYAVUMILIA MAMBO YOTE TUSIJE TUKAIZUIA HABARI NJEMA YA KRISTO.

Umeona haya Maneno? Huku ni kujitesa... ni kutoruhusu haki yako ikufanye ulegee katika utumishi wako eti kwa sababu wahusika hawaitimizi... anabaki katika KUVUMILIA... awe anapewa au hapewi chochote.

### **Anaongeza 1 Wakorintho 9:13-15**

*[13] Hamjui ya kuwa wale wazifanyao kazi za hekaluni hula katika vitu vya hekalu, na wale waihudumiao madhabahu huwa na fungu lao katika vitu vya madhabahu?*

*[14] Na Bwana vivyo hivyo ameamuru kwamba wale waihubirio Injili wapate riziki kwa hiyo Injili.*

*[15] Lakini mimi sikutumia mambo hayo hata moja. Wala siyaandiki hayo ili iwe hivyo kwangu mimi; maana ni heri nife kuliko mtu awaye yote abatilishe huku kujisifu kwangu.*

Angalia tena maneno ya Paulo kwa umakini LAKINI MIMI SIKUTUMIA MAMBO HAYO (YA KUDAI HAKI YANGU YA MHUDUMU WA INJILI) HATA MOJA.

### **1 Wakorintho 9:17-18**

*[17] Maana nikiitenda kazi hii kwa hiari yangu nina thawabu; ila ikiwa si kwa hiari yangu, nimeaminiwa uwakili.*

*[18] Basi thawabu yangu ni nini? Ni hii, ya kuwa nihubiripo, nitaitoa Injili bila gharama, bila kutumia kwa utimilifu uwezo wangu nilio nao katika Injili.*

Paulo, akitenda kwa hiari ana THAWABU... THAWABU ni malipo ya uaminifu kwa Injili ambayo Bwana huwapatia watenda kazi katika shamba lake a.k.a huduma. Siyo wokovu huu! Ni THAWABU. Unafanya kazi. Ni malipo ya uaminifu. WOKOVU hauufanyii kazi, THAWABU unafanya kazi... ndiyo maana Kiingereza wanatumia neno REWARD... kitu unapewa baada ya kushinda...

Anaendelea kuzungumzia hiyo Reward a.k.a THAWABU. Angalia ***1 Wakorintho 9:24-25***

***[24] Je! Hamjui, ya kuwa wale washindanao kwa kupiga mbio, hupiga mbio wote, lakini apekeaye tuzo ni mmoja? Pigeni mbio namna hiyo, ili mpate.***

***[25] Na kila ashindanaye katika michezo hujizuia katika yote; basi hao hufanya hivyo kusudi wapokee taji iharibikayo; bali sisi tupokee taji isiyoharibika.***

Anatumia mfano wa michezo kufundishia juu ya hiyo THAWABU.

Kwenye michezo unapewa taji inayoharibika lakini kwa Mungu unapewa taji isiyoharibika.

Hiyo ndiyo tofauti. Angalia sasa ***1 Wakorintho 9:26-27***

*[26] Hata mimi napiga mbio vivyo hivyo, si kama asitaye; napigana ngumi vivyo hivyo, si kama apigaye hewa;*

*[27] bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha; isiwe, nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa.*

Mpaka hapo tumeona mazungumzo yalijikita kwenye THAWABU na akawashauri... pigeni mbio mpate. Kisha anawaambia HATA MIMI NAPIGA MBIO VILE VILE... tena kwa kuutesa mwili wangu. hayo mateso ameyataja hapo juu... UVUMILIVU KATIKA MAZINGIRA YOYOTE ILI AWEZE KUHUBIRI INJILI kwa watu wa aina zote...

Angalia namna alivyoutesa na kuutumikisha mwili wake. **I Wakorintho 9:18-23**

*[18] Basi thawabu yangu ni nini? Ni hii, ya kuwa nihubiripo, nitaitoa Injili bila gharama, bila kutumia kwa utimilifu uwezo wangu nilio nao katika Injili.*

*[19] Maana, ingawa nimekuwa huru kwa watu wote, nalijifanya mtumwa wa wote, ili nipate watu wengi zaidi.*

*[20] Nalikuwa kama Myahudi kwa Wayahudi, ili niwapate Wayahudi; kwa wale walio chini ya sheria, nalikuwa kama chini ya sheria, (ingawa*

*mimi mwenyewe si chini ya sheria), ili niwapate walio chini ya sheria.*

**[21] Kwa wale wasio na sheria nalikuwa kama sina sheria, (si kwamba sina sheria mbele za Mungu, bali mwenye sheria mbele za Kristo), ili niwapate hao wasio na sheria.**

**[22] Kwa wanyonge nalikuwa mnyonge, ili niwapate wanyonge. Nimekuwa hali zote kwa watu wote, ili kwa njia zote nipate kuwaokoa watu.**

**[23] Nami nafanya mambo yote kwa ajili ya Injili ili kuishiriki pamoja na wengine.**

*Ukisoma 1 Corinthians 9:27 KJV But I keep under my body, and bring it into subjection: lest that by any means, when I have preached to others, I myself should be a castaway.*

Neno "**CASTAWAY**" ni neno la Kigiriki "*adokimos*" ikiwa na maana ya *to be disqualified or to miss a reward. Kukosa THAWABU.*

Hata TKU imeandikwa... *Ninaudhibiti mwili wangu kikamilifu na kuufanya unitii kwa kila jambo ninalotaka kutenda. Ninafanya hivi ili mimi binafsi NISIIKOSE THAWABU baada ya kuwahubiri wengine Habari Njema. (1 Wakorintho 9:27 TKU)*

Kwenye baadhi ya tafsiri za kisasa za Kingereza wameondoa neno "castaway".

Mfano... Hebu tuangalie NIV ...

*"Everyone who competes in the games goes into strict training. They do it to get a crown that will not last, but we do it to get a crown that will last forever. Therefore, I do not run like someone running aimlessly; I do not fight like a boxer beating the air. No, I strike a blow to my body and make it my slave so that after I have preached to others, I myself will not be disqualified for the prize." (NIV).*

Kwenye Boxing (ngumi) ukishindwa unapoteza mkanda... haupotei na wewe... lakini wewe utaokolewa na refa.

NLT nao wanasema *"All athletes are disciplined in their training. They do it to win a prize that will fade away, but we do it for an eternal prize. So, I run with purpose in every step. I am not just shadowboxing. I discipline my body like an athlete, training it to do what it should. Otherwise, I fear that after preaching to others I myself might be disqualified." (NLT).*

Kuwa "*disqualified*" ni kupoteza kitu, siyo wewe kupotea. Yaani kila ulichokifanya kimepotea hakina matumizi. Fikiria mtu aki "disco" chuoni hata kama yuko mwaka wa tatu anakuwa kama hajawahi kusoma. Amepoteza cheti.

*Inawezekana mtu kupoteza THAWABU kwa kuhubiri Injili kwa nia isiyopasa? NDIYO.*

Ameelezea kwenye sura za nyuma... **1 Wakorintho 3:12-15**

*[12] Lakini kama mtu akijenga juu ya msingi huo, dhahabu au fedha au mawe ya thamani, au miti au majani au manyasi, kazi ya kila mtu itakuwa dhahiri.*

*[13] Maana siku ile itaidhihirisha, kwa kuwa yafunuliwa katika moto; na ule moto wenyewe utaijaribu kazi ya kila mtu, ni ya namna gani.*

*[14] Kazi ya mtu aliyoijenga juu yake ikikaa, atapata thawabu.*

*[15] Kazi ya mtu ikiteketea, atapata hasara; ila ye ye mwenyewe ataokolewa; lakini ni kama kwa moto.*

### **KAZI YAKO NDIYO ITAKAYOTEKETEA...**

Ni vyema kujua kuwa msukumo wa huduma siyo mambo ya kidunia, mahitaji ya kimwili, umaarufu au mazingira ya kuvutia, ni uaminifu kufanya ulichoagizwa katika mazingira yote. Yesu aliwahi kutumia mfano

alifundisha UMUHIMU wa UAMINIFU NA  
UAMINIFU KAMA KIGEZO CHA HUDUMA.

*Mathayo 20:1-16*

- [1] *Kwa maana ufalme wa mbinguni umefanana na mtu mwenye nyumba aliyetoka alfajiri kwenda kuajiri wakulima awapeleke katika shamba lake la mizabibu.*
- [2] *Naye alipokwisha kupatana na wakulima kuwapa kutwa dinari, aliwapeleka katika shamba lake la mizabibu.*
- [3] *Akatoka mnamo saa tatu, akaona wengine wamesimama sokoni wasiokuwa na kazi;*
- [4] *na hao nao akawaambia, Enendeni nanyi katika shamba langu la mizabibu, na iliyo haki nitawapa. Wakaenda.*
- [5] *Akatoka tena mnamo saa sita na saa kenda, akafanya vile vile.*
- [6] *Hata kama saa kumi na moja akatoka, akakuta wengine wamesimama, akawaambia, Mbona mmesimama hapa mchana kutwa bila kazi?*
- [7] *Wakamwambia, Kwa sababu hakuna mtu aliyetuajiri. Akawaambia, enendeni nanyi katika shamba la mizabibu.*
- [8] *Kulipokuchwa, yule bwana wa shamba akamwambia msimamizi wake, Waite*

*wakulima, uwalipe ujira wao, ukianzia wa mwisho hata wa kwanza.*

*[9] Na walipokuja wale wa saa kumi na moja, walipokea kila mtu dinari.*

*[10] Na wale wa kwanza walipokuja, walidhani kwamba watapokea zaidi; na hao pia wakapokea kila mtu dinari.*

*[11] Basi wakiisha kuipokea, wakamnung'unikia mwenye nyumba,*

*[12] wakisema, Hao wa mwisho wametenda kazi saa moja tu, nawe umewasawazisha na sisi tuliostahimili taabu na hari za mchana kutwa.*

*[13] Naye akamjibu mmoja wao, akamwambia, Rafiki, sikudhulumu; hukupatana nami kwa dinari?*

*[14] Chukua iliyo yako, uende zako; napenda kumpa huyu wa mwisho sawa na wewe.*

*[15] Si halali yangu kutumia viliyyo vyangu kama nipendavyo? Au jicho lako limekuwa ovu kwa sababu ya mimi kuwa mwema?*

*[16] Vivyo hivyo wa mwisho watakuwa wa kwanza, na wa kwanza watakuwa wa mwisho.*

Hivyo UAMINIFU NI KUFANYA YALE TU AMBAYO NI KIPAUMBELE CHA BWANA WAKO.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

UKINIULIZA THAWABU NI NINI, ninajua ni ya milele. Anayetoa ni yule anayepima uaminifu katika kazi.

Hii siyo hukumu ya wenyе dhambi, hii ni hukumu ya wenyе haki. Ni watoto wa Baba katika kutoa hesabu zao. Haiwahusu waliokataa INJILI. Siyo hukumu ya mauti.

Tubaki kufanya kwa uaminifu.

Ni katika Kristo kwa namna ya Kristo.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

# 11

SURA YA

***HAIWEZEKANI KUWAFANYA UPYA TENA HATA  
WAKATUBU***



**V**ita juu ya kuondoa uhakika wa wokovu kwa waamini ni vita inayochagizwa na uchambuzi mbaya au kunukuu maandiko bila kuyachambua na kuyapa tafsiri iliyokusudiwa na mwandishi. Mara nyingi watu wamekuwa wakifundisha kinyume na uhakika wa WOKOVU, kwamba WOKOVU unaweza kupotea kwa kutumia kitabu cha ***Waembrania 6:4-6***

- [4] *Kwa maana hao waliokwisha kupewa nuru, na kukionja kipawa cha mbinguni, na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu,*  
[5] *na kulionja neno zuri la Mungu, na nguvu za zamani zijazo,*  
[6] *wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu; kwa kuwa wamsilibisha Mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao, na kumfedhehi kwa dhahiri.*

Sasa naomba uchukue kalamu na daftari yako na Biblia yako pembeni tufanye uchambuzi yakinifu kwenye kitabu cha Waebrania ili tuone mwandishi alikusudia nini.

**Mambo ya msingi kabisa unaposoma Biblia yako** (sasa naomba ujizoeze kufanya kazi hizi kanuni kabla hujauliza swali). Ongezeza **na yale** ya mwanzo.

**Jambo la kwanza** la muhimu kabisa unaposoma maandiko matakatifu ni kuacha papara. Usiseme vitu kichwani mwako. Hapo hakuna mambo ya "mimi nahisi anamaanisha hivi au vile" acha mwandishi akufundishe alichokusudia.

**Jambo la pili** ni kwamba Biblia haijipangi, haiwezi kusema ndiyo hapa na hapana pale kwa jambo lile lile...

hivyo inahitaji umakini kujua mwandishi alimaanisha nini.

**Jambo la tatu** ni muktadha: kujua habari ilipoanzia na pengine ilipoishia. Juu ya huo mstari mwandishi alisema nini na chini ya huo mstari alisema nini. (Pretext and post text).

**Jambo la nne**, kile alichokisema kinakubaliana na sehemu zingine za Biblia? Au imekaa kama kisiwa? Kumbuka: Kwa vinywa vya mshahidi wawili au watatu kila neno lidhibitike (*Kutoka 17:6, Kutoka 19:15, Mathayo 18:16, 2 Wakorintho 13:1, 1 Timotheo 5:19 na Waebrania 10:28*). Hii itakusaidia kuona aidha kuna kitu hukioni au version hiyo ina shida mahali.

**Jambo la tano:** Ujizoeze kupitia hata versions(tafsiri) zingine zitakusaidia kuona kwenye lugha nyingine namna walivyoandika au version nyingine ya Biblia wameandikaje... kuliko kuishia kusema mambo ambayo hayakutakiwa kusemwa kwa sababu kutokuwa makini katika kujifunza.

Niongeze la sita...

**Jambo la sita:** Kama unajua kutumia *Greek and Hebrew Concordance* itakusaidia kuona asili ya neno lililotumika

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

(hii inahitaji muda kufundishwa namna ya kutumia ndiyo maana nashauri hii iwe ya mwisho kabisa).

**UKIJIZOEZA KUFANYA MAMBO HAYO  
MATANO, NI NGUMU SANA KUANGUKIA  
KWENYE MAFUNDISHO POTOFOU.**

Kabla ya kurudi Waebrania 6:4-6, swal la msingi ni hili,  
***HUO WOKOVU WENYEWE UNAPATIKANAJE?***

Angalia 2 *Timotheo 3:15*

*[15] na ya kuwa tangu utoto umeyajua  
maandiko matakatifu, ambayo yaweza  
kukuhekimisha hata upate wokovu kwa imani  
iliyo katika Kristo Yesu.*

WOKOVU KWA IMANI iliyo KATIKA KRISTO YESU. Kwa hiyo WOKOVU ni kwa imani... hapo neno imani KINYUME chake siyo hofu kama watu wanavyoeleza bali ni MATENDO au jitihada za mtu.

Angalia *Waefeso 2:8-9*

*[8] Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa  
njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na  
nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu;  
[9] wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije  
akajisifu.*

Timotheo anaambiwa ni kwa Imani... Waraka kwa Waefeso SI KWA MATENDO. Kwa hiyo WOKOVU NI KWA IMANI SI KWA MATENDO... Na hapo matendo maana yake MATENDO MEMA.

Angalia hapa... *Tito 3:4-7*

- [4] *Lakini WEMA wake Mwokozi wetu Mungu, na UPENDO wake kwa wanadamu, ulipofunuliwa, ALITUOKOA;*
- [5] *SI kwa sababu ya MATENDO ya HAKI TULIYOYATENDA sisi; bali kwa REHEMA YAKE, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu;*
- [6] *ambaye alitumwagia kwa wingi, kwa njia ya YESU KRISTO MWOKOZI WETU;*
- [7] *ili tukihesabiwa haki kwa neema yake, tupate kufanywa warithi wa UZIMA WA MILELE, kama lilivyo tumaini letu.*

Iko wazi ya kwamba WOKOVU haupatikani kwa matendo na Paulo anamwambia Tito, huo WOKOVU ni kuoshwa ni kuzaliwa kwa pili, ni kufanywa UPYA na Roho Mtakatifu, ni kuhesabiwa haki, ni kufanywa WARITHI wa UZIMA WA MILELE... haya maneno ni msingi sana... hapa maana yake UZIMA WA MILELE

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

NI ROHO YA MUNGU NA YA MWANADAMU  
KUWA KITU KIMOJA.

Angalia 1 *Wakorintho 6:17*

*[17] Lakini yeye aliyeungwa na Bwana ni roho  
moja naye.*

Hii ni zaidi ya homogeneous solution... They are not separable... Angalia hapa 1 *Yohana 4:14-15*

*[14] Na sisi tumeona na kushuhudia ya kuwa  
Baba amemtuma Mwana kuwa MWOKOZI wa  
ulimwengu.*

*[15] Kila akiriye ya kuwa Yesu ni Mwana wa  
Mungu, Mungu HUKAA NDANI YAKE, NAYE  
NDANI YA MUNGU.*

Umeelewa hii? Ndiyo maana ni zaidi ya homogeneous solution ni roho ya mwanadamu na Mungu zinaungana milele.

Kwa hiyo namna ya kuokolewa ni Mungu kuja na kukaa ndani yako au Roho wa Mungu na roho yako kuwa MOJA. ANGALAU hii ikae vizuri kwenye ufahamu wako.

Sasa mara nyingi watu wanaoitwa wameokoka hawajui kweli hii. Wanajua Roho wa Mungu anawatembelea tu

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

kwa kitambo, wakikosea anaondoka, "wakitubu" anarudi... au wakiimba wimbo wa kuabudu anashuka na kama bado hawajaimba hayupo kabisa au wafanye kwanza maombi ya kumkaribisha au kumkaribia... WAKATI MWAMINI NI MAKAO YA MUNGU.

*"A believer is God's dwelling place not occasional visiting centre"*

## **HUYU MWOKOZI SASA KAZI YAKE NI DHABITI AU YA KUUNGAUNGA?**

Kama WOKOVU ni kazi ya mwokozi na siyo mwokolewaji, bila shaka uimara au udhabit wa hiyo kazi huelezewa kwenye UWEZO, UAMINIFU NA UIMARA wa MWOKOZI mwenyewe... siyo MWOKOLEWAJI! Kwa sababu anayeokolewa kwa jina lake tu hilo inaonekana hana uwezo wa kujioako... ndiyo maana anahitaji WOKOVU utokao kwa MWOKOZI.

*"The power and assurance of Salvation is in the power of the SAVIOUR"*

*"If the saviour is weak then his salvation is weak, if the Saviour is powerful then His salvation is trustworthy"*

Kitabu cha Waebrania kinafundisha sana juu ya huyu MWOKOZI na WOKOVU wake.

Angalia **Waebrania 5:9**

*[9] naye (YESU) alipokwisha kukamilishwa,  
akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu  
wote wanaomtii;*

Angalia "WOKOVU WA MILELE", watu wote wanaomtii Yesu pale ni WAAMINI (BELIEVERS).

Angalia pia **Mathayo 1:21**

*[21] Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina  
lake Yesu, maana, ye ye ndiye atakayewaokoa  
watu wake na dhambi zao.*

Huu wokovu wa milele ni kuokolewa kutoka kwenye "DHAMBI".

Tukiunganisha **Waebrania 5:9** na **Mathayo 1:21...**  
"KUOKOLEWA KUTOKA KWENYE DHAMBI NI JAMBO LA MILELE" ina maana mtu akiokoka kutoka kwenye dhambi anakuwa ameokolewa na anadumu kutokuwa na "DHAMBI MILELE"

Yohana kuna namna ameandika kwenye **Yohana 1:29**

*[29] Siku ya pili yake amwona Yesu anakuja  
kwake, akasema, Tazama, Mwana-kondoo wa  
Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu!*

Angalia "AICHUKUAYE DHAMBI"; kuchukua maana yake "HAIPO PALE ILIPOKUWA" kumbe hii ni kazi

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

ya milele. Tunaendelea kumwangalia huyu MWOKOZI WETU YESU KRISTO...

*Tito 2:10,13*

*[10] wasiwe waibaji; bali wauonyeshe uaminifu mwema wote, ili wayapambe mafundisho ya Mwokozi wetu Mungu katika mambo yote.*

*[13] tukilitazamia tumaini lenye baraka na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu, Mungu mkuu na Mwokozi wetu;*

Kristo Yesu, Mungu mkuu na mwokozi wetu...

*Tito 3:4,6*

*[4] Lakini wema wake Mwokozi wetu Mungu, na upendo wake kwa wanadamu, ulipofunuliwa, alituokoa;*

*[6] ambaye alitumwagia kwa wingi, kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu;*

Yesu Kristo mwokozi wetu...

Kwa hiyo, Yesu Kristo ni Mungu mkuu aokoaye au MWOKOZI.

*Petro naye pia... 2 Petro 1:1,11*

*[1] Simoni Petro, mtumwa na mtume wa Yesu Kristo, kwa wale waliopata imani moja na sisi, yenye thamani, katika hali ya Mungu wetu, na Mwokozi Yesu Kristo.*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

**[11] Maana hivi mtaruzukiwa kwa ukarimu  
kuingia katika ufalme wa milele wa Bwana  
wetu, Mwokozi wetu Yesu Kristo.**

Mungu wetu na mwokozi wetu Yesu Kristo...

Bwana wetu, Mwokozi wetu Yesu Kristo...

Halafu anasema Ufalme wa Milele wa Bwana wetu,  
Mwokozi wetu Yesu Kristo.

Anaendelea kwa kusema **2 Petro 3:18**

**[18] Lakini, kueni katika neema, na katika  
kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo.  
Utukufu una yeye sasa na hata milele.**

Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo...

Kwa hiyo ni dhahiri kwamba Yesu ni Mungu au Bwana  
au ni Kristo aokoaye au MWOKOZI.

Turudi nyuma kidogo, tuliposoma **Yohana 1:29**

**[29] Siku ya pili yake amwona Yesu anakuja  
kwake, akasema, Tazama, Mwana-kondoo wa  
Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu!**

Hii ina maana kwamba ulimwengu wote umeokolewa!  
Au kila mtu ameokoka? Kubaki kwenye **Yohana 1:29**  
peke yake ni kusahau kanuni za kufasiri maandiko  
tuliojifunza hapo juu.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Kwenye **1 Timotheo 4:10**

*[10] kwa maana twajitaabisha na kujitahidi kwa kusudi hili, kwa sababu tunamtumaini Mungu aliye hai, aliye Mwokozi wa watu wote, hasa wa waaminio.*

Neno hasa pale ni "SPECIALLY" kuonyesha kwamba ni kwa waaminio. Hii ina maana WOKOVU siyo kazi Mungu anafanya kila siku, ni kazi aliyoifanya mara moja. Kazi ya mwanadamu ni kupokea tu. Ndiyo maana tunahubiri Injili. Je, inawezekana kufa njaa wakati chakula kiko ndani ya nyumba? Ndiyo. Kwa sababu kuwepo siyo kula.

Yesu anasemaje? **Yohana 10:28**

*[28] Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu.*

Angalia kwa makini mstari huu.

Nawapa UZIMA WA MILELE...

Hawatapotea KAMWE...

HAKUNA mtu ATAKAYEWAPOKONYA katika MKONO WANGU...

Lengo letu ni kuona lengo na maana ya mwandishi kusema **Waebria 6:4-6**

- [4] *Kwa maana hao waliokwisha kupewa nuru, na kukionja kipawa cha mbinguni, na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu,*  
[5] *na kulionja neno zuri la Mungu, na nguvu za zamani zijazo,*  
[6] *wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu; kwa kuwa wamsilibisha Mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao, na kumfedhehi kwa dhahiri.*

Hasa yale maneno... HAIWEZEKANI KUWAFANYA UPYA TENA WAKATUBU. Wengi wakiwa wanamaanisha kuna hatua MWAMINI akifika, akishakosea hawezি tena kuokolewa inakuwa IMETOKA HIYO. Tunajadili haya kwa sababu yanapingana na WOKOVU wa MILELE NA UHAKIKA WAKE (ETERNAL SALVATION AND IT'S SECURITY).

Sasa ni vyema kuwa makini na Kitabu cha Waraka kwa Waebrania kwa sababu ni kitabu chenye mtiririko wa kipekee na mada ikiwa inafafanuliwa hatua kwa hatua. Ukibakia mahali pamoja na kutengeneza fundisho bila kuhusisha sura zingine unaweza kujikuta unafikia HITIMISHO ambalo ni sumu.

Kwanza, mwandishi ameandika kwa lengo la kuitukuza kazi ya Ukombozi ulio katika Yesu Kristo kwa kuchambua vitabu vya agano la Kale huku akifananisha:-

- ◆ Yesu na malaika,
- ◆ Yesu na Musa,
- ◆ Yesu na Yoshua,
- ◆ Yesu na Melkizedeki,
- ◆ Yesu na Haruni,
- ◆ Yesu na sadaka zote zilizotolewa kwenye hema ya kukutania,
- ◆ Yesu na wazee wa walioandikwa kwenye Agano la Kale.

UKIANGALIA KWA MAKINI, Lengo lake hasa ni kuonyesha, UTIMILIFU, UWEZO, NA UHAKIKA WA KAZI YA UKOMBOZI ULIO KATIKA KRISTO YESU.

Ukiangalia kwa makini kitabu cha Waebrania utagundua kuwa mwandishi aliandika akiwataja watu wa aina mbalimbali kwenye kitabu cha Waraka kwa Waebrania.

#### 1. Wayahudi walioamini *Waebrania 4:2*

*[2] Maana ni kweli, sisi nasi tumehubiriwa habari njema vile vile kama hao. Lakini neno lile lililosikiwa halikuwafaa hao, kwa sababu*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

*halikuchanganyika na imani ndani yao waliosikia.*

Angalia pia *Waebrania* 10:39

*[39] Lakini sisi hatumo mionganoni mwao wasitao na kupotea, bali tumo mionganoni mwa hao walio na imani ya kutuokoa roho zetu.*

Hawa ni waamini (SISI)...

2. Wayahudi wasioamini: Angalia *Waebrania* 3:12

*[12] Angalieni, ndugu zangu, usiwe katika mmoja wenu moyo mbovu wa kutokuamini, kwa kujitenga na Mungu aliye hai.*

Angalia pia *Waebrania* 10:27-29

*[27] bali kuna kuitazamia hukumu yenyе kutisha, na ukali wa moto ulio tayari kuwala wao wapingao.*

*[28] Mtu aliyeidharau sheria ya Musa hufa pasipo huruma, kwa neno la mashahidi wawili au watatu.*

*[29] Mwaonaje? Haikumpasa adhabu iliyo kubwa zaidi mtu yule aliyemkanyaga Mwana wa Mungu, na kuihesabu damu ya agano aliyotakaswa kwayo kuwa ni kitu ovyo, na kumfanyia jeuri Roho wa neema?*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

3. Wayahudi waliofanya migumu mioyo yao.  
(WAMESIKIA INJILI ILA WAMEGOMA KUAMINI).

***Waebrania 10:29***

*[29] Mwaonaje? Haikumpasa adhabu iliyo kubwa zaidi mtu yule aliyemkanyaga Mwana wa Mungu, na kuihesabu damu ya agano aliyotakaswa kwayo kuwa ni kitu ovyo, na kumfanyia jeuri Roho wa neema?*

Tena... ***Waebrania 3:16-19***

*[16] Maana ni akina nani waliokasirisha, waliposikia? Si wale wote waliotoka Misri wakiongozwa na Musa?*

*[17] Tena ni akina nani aliochukizwa nao miaka arobaini? Si wale waliokosa, ambao mizoga yao ilianguka katika jangwa?*

*[18] Tena ni akina nani aliowaapia ya kwamba hawataingia katika raha yake, ila wale walioasi?*

*[19] Basi twaona ya kuwa hawakuweza kuingia kwa sababu ya kutokuamini kwao.*

Anaendelea... ***Waebrania 4:1***

*[1] Basi, ikiwa ikaliko ahadi ya kuingia katika raha yake, na tuogope, mmoja wenu asije akaonekana ameikosa.*

Kwenye hili kusanyiko lenye watu wa aina 3 anawaandikia ILI: -

1. Kuwahakikishia wale walioamini juu ya UHAKIKA WA WOKOVU WALIOUPOKEA.
2. Kuwashawishi wale ambao bado hawajashawishika na Injili ili waamini.
3. Kuwakaribisha wale wasioamini ili waamini.

Angalia AKIWAKARIBISHA... *Waebmania 4:16*

*[16] Basi na tukikaribie kitii cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.*

ANAWAKARIBISHA WAKIKARIBIE KITI CHA REHEMA. Anarudia tena: *Waebmania 10:22*

*[22] na tukaribie wenye moyo wa kweli, kwa utimilifu wa imani, hali tumenyunyiziwa mioyo tuache dhamiri mbaya, tumeoshwa miili kwa maji safi.*

Anawakaribisha tena... NA TUKARIBIE. HAWA SIO WAAMINI... ANGALIA KWA UPANA HAPA KWENYE *Waebmania 4:14-16*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

*[14] Basi, iwapo tunaye kuhani mkuu aliyeingia katika mbingu, Yesu, Mwana wa Mungu, na tuyashike sana maungamo yetu.*

*[15] Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi.*

*[16] Basi na tukikaribie kitit cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.*

(LET'S COME BOLDLY).

HAPA ANAWASHAWISHI KABISA WAKARIBIE...  
KUHUSU MWAMINI Petro aliandika... **1 Petro 2:9-10**

*[9] Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpare kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu;*

*[10] ninyi mliokuwa kwanza si taifa, bali sasa ni taifa la Mungu; mliokuwa hamkupata rehema, bali sasa mmepeata rehema.*

MWAMINI amepata REHEMA wala hasogelei kitit cha REHEMA.

Ndiyo maana juu yake anasema kwenye **Waembrania 4:1-3**

*[1] Basi, ikiwa ikaliko ahadi ya kuingia katika raha yake, na tuogope, mmoja wenu asije akaonekana ameikosa.*

*[2] Maana ni kweli, sisi nasi tumehubiriwa habari njema vile vile kama hao. Lakini neno lile lililosikiwa halikuwafaa hao, kwa sababu halikuchanganyika na imani ndani yao waliosikia.*

*[3] Maana sisi tulioamini tunaingia katika raha ile; kama vile alivyosema,  
Kama nilivyoapa kwa hasira yangu,  
Hawataingia rahani mwangu:  
ijapokuwa zile kazi zilimalizika tangu kuwekwa  
misingi ya ulimwengu.*

SISI TULIOAMINI TUNAINGIA KWENYE RAHA YAKE... ASIYEAMINI ANAITWA ILI AINGIE. Maana aliyeamini yuko katika Raha au Sabato ya Bwana. Kwenye Waembrania pia MWAMINI anaonekana AMEFIKA WALA HASOGEI...

Angalia **Waembrania 12:22-24**

*[22] Bali ninyi mmeufikilia mlima Sayuni, na mji wa Mungu aliye hai, Yerusalemu wa mbinguni, na majeshi ya malaika elfu nyngi,*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

*[23] mkutano mkuu na kanisa la wazaliwa wa kwanza walioandikwa mbinguni, na Mungu mwamuzi wa watu wote, na roho za watu wenye haki waliokamilika,*

*[24] na Yesu mjumbe wa agano jipy, na damu ya kunyunyizwa, inenayo mema kuliko ile ya Habili.*

WE HAVE COME (ARRIVED)... Lakini pia UTAKASO WAKE NI SETTLED. *Waebrania 10:10*

*[10] Katika mapenzi hayo mmeputa utakaso, kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja tu.*

MMEPATA UTAKASO KWA KUTOLEWA MWILI WA YESU MARA MOJA.

Ina maana kazi imeisha. DEAL DONE. CASE CLOSED. PROBLEM SOLVED. KWA KUAMINI TU!

Angalia anavyokazia kwenye mistari inayofuata...  
*Waebrania 10:11-14*

*[11] Na kila kuhani husimama kila siku akifanya ibada, na kutoa dhabihu zile zile mara nyingi; ambazo haziwezi kabisa kuondoa dhambi.*

*[12] Lakini huyu, alipokwisha kutoa kwa ajili ya dhambi dhabihu moja idumuyo hata milele, aliketi mkono wa kuume wa Mungu;*

*[13] tangu hapo akingojea hata adui zake wawekwe kuwa chini ya miguu yake.*

*[14] Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa.*

Hivyo wakati wa kusoma Kitabu cha Waraka kwa Waembrania uwe makini utazame aina 3 za watu na aina 3 ya kazi ya mwandishi kwao. Angalia kama anawaonyesha UHAKIKA WA WOKOVU AU ANAWASHAWISHI WAAMINI AU ANAWAHUBIRIA WAPOKEE INJILI.

Tujikumbushe ya mwandishi wa kitabu cha Waraka kwa Waembrania amejikita sana kuonyesha nguvu ya MWOKOZI na Uhakika wa WOKOVU wake akitofautisha kwa nguvu sana na sadaka za akina Haruni na Walawi zisizoweza kuondoa dhambi.

Sasa turudi kwenye sehemu yetu iliyokuwa inasumbua yaani *Waembrania 6:4-6*

*[4] Kwa maana hao waliokwisha kupewa nuru, na kukionja kipawa cha mbinguni, na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu,*

*[5] na kulionja neno zuri la Mungu, na nguvu za zamani zijazo,*

*[6] wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu; kwa kuwa wamsilibisha Mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao, na kumfedhehi kwa dhahiri.*

Angalia King James Version walivyoandika... ***Heb 6:4-6***  
**KJV**

*4 For it is impossible for those who were once enlightened, and have tasted of the heavenly gift, and were made partakers of the Holy Ghost,*

*5 And have tasted the good word of God, and the powers of the world to come,*

*6 If they shall fall away, to renew them again unto repentance; seeing they crucify to themselves the Son of God afresh, and put him to an open shame.*

Sasa tuangalie, Hawa watu ni watu gani?

WALIOKWISHA                    KUPEWA                    NURU  
(ENLIGHTENED), NA KUKIONJA KIPAWA CHA  
MBINGUNI, WASHIRIKA WA ROHO MTAKATIFU,  
NA KULIONJA NENO ZURI LA MUNGU, NA  
NGUVU ZA ZAMANI ZIJAZO.

Bila kufanya uchambuzi wa **kiundani** "deep study" ni dhahiri ya kuwa hawa watu ni WAAMINI. Kwa nini? Nitatumia kigezo kimoja tu... ijapokuwa tungeweza kuchambua kitu kimoja baada ya kingine... ambayo ni KUFANYWA WASHIRIKA WA ROHO MTAKATIFU (Partakers of Holy Ghost). Mwamini ameshirikishwa Roho wa Mungu, Mungu anakaa ndani yake na hiyo ndiyo arabuni ya Ukombozi wetu, Roho ndani yetu. **I Yohana 4:13**

*[13] Katika hili tunafahamu ya kuwa tunakaa ndani yake, naye ndani yetu, kwa kuwa ametushirikisha Roho wake.*

## **2 Wakorintho 5:5**

*[5] Basi yeye aliyetufanya kwa ajili ya neno lilo hilo ni Mungu, aliyetupa arabuni ya Roho.*

## **Waefeso 1:13-14**

*[13] Nanyi pia katika huyo mmekwisha kulisikia neno la kweli, habari njema za wokovu wenu; tena mmekwisha kumwamini yeye, na kutiwa muhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu.*

*[14] Ndiye aliye arabuni ya urithi wetu, ili kuleta ukombozi wa milki yake, kuwa sifa ya utukufu wake.*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Kwa sababu hiyo.... uzito wa mambo yaliyoonyeshwa hapo... ni hakika HAWA NI WAAMINI.

Ukiangalia kwenye KJV, maneno ya Kiswahili (SUV) "WALIOWISHA KUPEWA NURU" ni maneno ya Kingereza (KJV) "Those who were ONCE enlightened..."

Kusema WALIOWISHA maana yake ni jambo lililokamilika katika utendaji wake. Imekwisha. Settled.

Kinyume chake ni "KUWAFANYA UPYA TENA" au "TO RENEW THEM AGAIN"

Neno lililochagiza maeneo haya mawili.

WALIOWISHA na KUWAFANYA UPYA ni neno HAIWEZEKANI. (It is impossible).

Hebu tufanyie utafiti kidogo haya maneno... WALIOWISHA (ONCE) na KUWAFANYA UPYA (RENEW).

Neno **ONCE** limetumika kwa Kigiriki kama "**hapax**" likiwa na maana ya **one time au once for all**.

Neno limetumika kuonyesha ukamilfu wa dhabihu ya Yesu Kristo. Angalia *Waibrania 9:26*

*[26] kama ni hivyo, ingalimpasa kuteswa mara  
nyingi tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu;*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

*lakini sasa, mara moja tu, katika utimilifu wa nyakati, amefunuliwa, azitangue dhambi kwa dhabihu ya nafsi yake.*

MARA MOJA TU.

*Waebrania 10:10*

*[10] Katika mapenzi hayo mmeputa utakaso, kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja tu.*

MARA MOJA TU.

*Waebrania 7:27*

*[27] ambaye hana haja kila siku, mfano wa wale makuhani wakuu wengine, kwanza kutoa dhabihu kwa ajili ya dhambi zake mwenyewe, kisha kwa ajili ya dhambi za hao watu; maana yeeye alifanya hivi mara moja, alipojitoa nafsi yake.*

MARA MOJA.

*Waebrania 10:2*

*[2] Kama ndivyo, je! Dhabihu hazingekoma kutolewa; kwa maana waabuduo, wakiusha kusafishwa mara moja, wasingejiona tena kuwa na dhambi?*

MARA MOJA WAKISAFISHWA WASINGEJIONA TENA KUWA NA DHAMBI? Hii ina maana kwa dhabihu inatolewa mara moja na baada ya hapo haitolewi TENA. Lakini pia wale wanaosafishwa, wanasafishwa mara MOJA TU na baada ya hapo... HAWAHITAJI KUSAFISHWA TENA WALA HAWAJIONI WENYE DHAMBI TENA. INAKUWA IMEISHA KABISA.

Hii ina maana "HAIWEZEKANI" mtu kuokoka mara mbili au zaidi!

Ni aidha umeokoka MARA MOJA au HUJAWAHI KUOKOKA kabisa.

Neno la Pili ni **RENEW** (KUWAFANYA UPYA) ni neno la Kigiriki "*anakainizō*" ni "**to restore**" kama tunavyofanya kwenye simu... yaani kurudisha mwanzo kabisa... au "**to start afresh**" yaani mtu arudi kuanza hatua mpya za WOKOVU. Ahubiriwe kisha aamini tena halafu apate uzima wa milele. Yaani awe kama hakuwahi kuamini halafu afanywe aamini kwa upya.

Hili neno limetumika sehemu moja tu kwenye Biblia (*Waraka kwa Waibrania 6:6*) kuonyesha ya kuwa si jambo la kawaida. Limewekwa hapa kwa sababu linatumika kwenye "defence" au kulinda UHAKIKA wa

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

WOKOVU. Na ndiyo lengo hasa la mjadala ulioko Waebrania 6.

Sasa tunaweza kuchukua maneno haya sasa  
**"WAKISHAOKOLEWA MARA MOJA,  
HAIWEZEKANI WAKAANGUKA KIASI CHA  
KUWARUDISHA HATUA YA MWANZO KABISA ILI  
WAANZE KUTUBU UPYA"**

Neno "Kutubu" kwa habari ya imani ILETAYO WOKOVU AU ONDOLEO LA DHAMBI ni kwamba mtu anatubu pale anapohubiriwa INJILI.

Angalia kila baada ya Injili (kufa na kufufuka kwa Yesu Kristo) kinachofuata ni TUBU AU TUBUNI...  
Toba ni mwitikio baada ya kuisikia Injili.

Angalia mifano hii!... **Luka 24:46-47**

**[46] Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu; (INJILI)**

**[47] na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake (KUFA NA KUFUFUKA KWAKE) habari ya TOBA na ONDOLEO la DHAMBI, kuanza tangu Yerusalem.**

Angalia Petro akitii agizo la Yesu Kristo... **Matendo ya Mitume 2:37-38**

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

[37] *Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, TUTENDEJE (MWITIKIO?), ndugu zetu?*

[38] *Petro akawaambia, TUBUNI mkabatizwe kila mmoja kwa JINA lake Yesu Kristo, MPATE ONDOLEO la DHAMBI zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*

Kisha na hapa pia... *Matendo ya Mitume 3:19*

[19] *TUBUNI basi, mrejee, ili DHAMBI ZENU ZIFUTWE, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana;*

Umeona mtiririko huo. Kila penye Injili, mwitikio ni Toba au Kubadili mtazamo na kuamini Injili ili kupata ONDOLEO la DHAMBI. Na huu ndio WOKOVU wenyewe.

Malaika aliweka wazi... *Mathayo 1:21*

[21] *Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao.*

HIVYO TUNAOKOLEWA KWENYE DHAMBI KWA KUAMINI INJILI AU KUFA NA KUFUFUKA KWA BWANA YESU.

Sasa hapo utaelewa maana ya haya maneno...  
**"WAKISHAOKOLEWA MARA MOJA,  
HAIWEZEKANI WAKAANGUKA KIASI CHA  
KUWARUDISHA HATUA YA MWANZO KABISA ILI  
WAANZE KUTUBU UPYA."** Hili ndiyo jambo ambalo haliwezekani kabisa. Mwandishi anaonyesha ya kuwa hakuna kuanguka kwenye WOKOVU. Ugumu wa kuanguka kwenye WOKOVU kiasi cha kurudi kuwa kama hujawahi kuokoka ni kwa sababu ya Nguvu ya Kuhani Mkuu Yesu Kristo na Nguvu ya Sadaka itolewayo. Haitoi mwanya kabisa wa kupoteza WOKOVU.

MWOKOZI au kuhani mkuu ni wa milele na WOKOVU WAKE NI WA MILELE. Sijui kama umeona neno MILELE vizuri hapo? Hebu tuangalie mwandishi wa kitabu cha Waraka kwa Waembrania alivyoweka haya kwa nguvu!

### *Waembrania 10:10*

*[10] Katika mapenzi hayo mmeputa utakaso,  
kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja  
tu.*

MARA MOJA TU.

Kama mtu anaweza kuokoka na kupoteza WOKOVU basi sadaka ya Yesu haina tofauti na sadaka za mafahali na mbuzi na wanyama walitolewa kama iagizavyo

torati. Ni kumfedhehi kwa dhahiri, ni kuonyesha ya kwamba alitakiwa asulubiwe mara kwa mara. Uwezo wa sadaka yake unachuja kulingana na hali ya mtu. Yenyewe haiwezi kuisimamia WOKOVU wake. Ni matusi kwa kazi ya Ukombozi.

**Angalia Waebraania 10:1-4,10-12**

- [1] *Basi torati, kwa kuwa ni kivuli cha mema yatakayokuwa, wala si sura yenyewe ya mambo hayo, kwa dhabihu zile zile wanazozitoa kila mwaka daima, haiwezi wakati wo wote kuwakamilisha wakaribiao.*
- [2] *Kama ndivyo, je! Dhabihu hazingekoma kutolewa; kwa maana waabuduo, wakiisha kusafishwa mara moja, wasingejiona tena kuwa na dhambi?*
- [3] *Lakini katika dhabihu hizo liko kumbukumbu la dhambi kila mwaka.*
- [4] *Maana haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi.*
- [10] *Katika mapenzi hayo mmeputa utakaso, kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja tu.*
- [11] *Na kila kuhani husimama kila siku akifanya ibada, na kutoa dhabihu zile zile mara nyingi; ambazo haziwezi kabisa kuondoa dhambi.*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

**[12] Lakini huyu, alipokwisha kutoa kwa ajili ya dhambi dhabihu moja idumuyo hata milele, aliketi mkono wa kuume wa Mungu;**

NI TOFAUTI NA WANYAMA WALE. Yeye ndiye anaweka dhambi mbali na wewe... hauweki wewe, mbali kidogo, mbali sana, au wastani.

### **Zaburi 103:12**

**[12] Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, Ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi.**

Hivyo ndivyo Daudi alivyotabiri. Mashariki na Magharibi hawawezi kukutana hata siku moja.

Kwenye WOKOVU, una uhuru wa kuamini au kutoamini na ukishaamini huna uhuru wa kupoteza.

Ukiwa umetumia uhuru wako wa kutoamini hakuna mema unayoweza kuyafanya ili uupate isipokuwa utumie huo uhuru wako KUAMINI.

Kama mwenye dhambi akifanya mema yote duniani na hakuamini kazi ya Ukombozi wa Yesu Kristo HAWEZI kupata WOKOVU. Kama mwamini akifanya maovu yote duniani HAWEZI kupoteza huo WOKOVU. Mwamini ana sababu nyingi sana za kufanya mema

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

lakini hajitahidi ili aokolewe... (he is not trying to be SAVED).

Angalia tena... *Waebrania 9:26-28*

[26] *kama ni hivyo, ingalimpasa kuteswa mara nyangi tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu; lakini sasa, mara moja tu, katika utimilifu wa nyakati, amefunuliwa, azitangue dhambi kwa dhabihu ya nafsi yake.*

[27] *Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu;*

[28] *kadhalika Kristo naye, akiisha kutolewa sadaka mara moja azichukue dhambi za watu wengi; atatokea mara ya pili, pasipo dhambi, kwa hao wamtazamiao kwa wokovu.*

Mtu huyu aliyeamini akitenda dhambi (akianguka) ana vitu vya kupoteza lakini si wokovu. Ndiyo maana **mistari** inayofuata imeelezea hayo.

*Waebrania 6:7-8*

[7] *Maana nchi inayoinywa mvua inayoinyeshea mara kwa mara, na kuzaa mboga zenyne manufaa kwa hao ambao kwa ajili yao yalimwa, hushiriki baraka zitokazo kwa Mungu;*

**[8] bali ikitoa miiba na magugu hukataliwa na kuwa karibu na laana; ambayo mwisho wake ni kuteketezwa.**

Nchi inayoinywa mvua hapa ni mtu aliyeamini, anategemewa kuzaa matunda. Sasa akishindwa kuzaa matunda ni jambo lingine. Mwandishi anasema HUKATALIWA.

Neno **HUKATALIWA** ni neno la Kigiriki "**ADOKIMOS**" ambalo lina maana ya "**DISAPPROVAL OF DEEDS OR WORKS**".

Neno "*adokimos*" ni sawa na neno lililotumika kwenye **1 Wakorintho 9:27** "*kukataliwa*" au "*castaway*" au "*rejected*" akiwa na maana ya KUKATALIWA KWA KAZI YA MTU NA SIYO KUKATALIWA KWA MTU.

### ***1 Corinthians 9:27 KJV***

*But I keep under my body, and bring it into subjection: lest that by any means, when I have preached to others, I myself should be a castaway.*

Neno "**CASTAWAY**" ni neno la Kigiriki "*adokimos*" ikiwa na maana ya ***to be disqualified or to miss a reward.*** TKU imeandikwa... ***1 Wakorintho 9:27 TKU***

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

*Ninaudhibiti mwili wangu kikamilifu na  
kuufanya unitiii kwa kila jambo ninalotaka  
kutenda. Ninafanya hivi ili mimi binafsi  
NISI KOSE THAWABU baada ya kuwahubiri  
wengine Habari Njema.*

Kwenye baadhi ya versions za kisasa za Kingereza  
wameondoa neno **castaway**...

Mfano... Hebu tuangalie NIV...

*“Everyone who competes in the games goes into strict training. They do it to get a crown that will not last, but we do it to get a crown that will last forever. Therefore, I do not run like someone running aimlessly; I do not fight like a boxer beating the air. No, I strike a blow to my body and make it my slave so that after I have preached to others, I myself will not be disqualified for the prize.” (NIV).*

Kwenye mchezo wa ngumi ukishindwa unapoteza  
mkanda... haupotei na wewe.

NLT nao wanasemaje?

*“All athletes are disciplined in their training. They do it to win a prize that will fade away, but we do it for an eternal prize. So, I run with purpose in every step. I am not just shadowboxing. I discipline my body like an*

*athlete, training it to do what it should. Otherwise, I fear that after preaching to others I myself might be disqualified." (NLT).*

Kuwa "disqualified" ni kupoteza kitu, siyo wewe kupotea. Yaani kila ulichokifanya kimepotea haina matumizi. Fikiria mtu aki "disco" chuoni hata kama yuko mwaka wa tatu anakuwa kama hajawahi kusoma, amepoteza cheti. Inawezekana mtu kupoteza THAWABU? NDIYO. Lakini Yeye anakuwa ameokolewa. **THAWABU SIYO NEEMA NA NEEMA SIYO THAWABU.** Paulo alisema hilo kwenye

### **1 Wakorintho 3:12-15**

*[12] Lakini kama mtu akijenga juu ya msingi huo, dhahabu au fedha au mawe ya thamani, au miti au majani au manyasi, kazi ya kila mtu itakuwa dhahiri.*

*[13] Maana siku ile itaidhahirisha, kwa kuwa yafunuliwa katika moto; na ule moto wenyewe utaijaribu kazi ya kila mtu, ni ya namna gani.*

*[14] Kazi ya mtu aliyoijenga juu yake ikikaa, atapata thawabu.*

*[15] Kazi ya mtu ikiteketea, atapata hasara; ila yeye mwenyewe ataokolewa; lakini ni kama kwa moto.*

Mwamini asiye na matunda ataokolewa lakini kazi yake itateketea ikiwa hakujenga katika Bwana. Angalia sasa

**Waebrania 6:7-8** mwandishi ameonyesha atakachokipoteza MWAMINI kuwa ni THAWABU wala siyo WOKOVU.

Sasa umeelewa lengo la mstari wa 4 hadi 6?

Na kwa msisitizo anawatia moyo kwa ajili ya kuwa na bidii katika kazi njema zenyenye THAWABU. Angalia anavyokazia kwenye sura hiyo hiyo

**Waebrania 6:9-12**

*[9] Lakini, wapenzi, ijapokuwa twanena hayo, katika habari zenu TUMESADIKI MAMBO YALIYO MAZURI ZAIDI, na yaliyo na WOKOVU.*

*[10] Maana Mungu si dhalimu hata aisahau kazi yenu, na pendo lile MLIOLIDHIHIRISHA kwa jina lake, kwa kuwa MMEWAHUDUMIA watakatifu, na hata hivi sasa mangali MKIWAHUDUMIA.*

*[11] Nasi TWATAKA SANA kila mmoja wenu aidhihirishe BIDII ile ile, kwa utimilifu wa matumaini hata mwisho;*

*[12] ili MSIWE WAVIVU, bali mkawe wafuasi wa hao wazirithio ahadi kwa imani na uvumilivu.*

Unaona anachowaambia? Angalia maneno haya niliyoyaweka kwa herufi kubwa. Ni mwenendo wao

wenye THAWABU. Wakaze kutenda mema, wakaze ku wahudumia WATAKATIFU. Kazi yao si bure. Mwandishi anawaambia WAWAIGE wanaofanya vizuri, wanaovumilia kama Paulo alivyoonyesha uvumilivu wake katika hali zote (**1 Wakorintho 9**)

Ni mwenendo wenye matunda. Wawe na bidii katika hayo. Hili tunajitahidi kufanya kwa uaminifu.

Mungu akifanya hivyo ndani yetu kwa Roho Mtakatifu aliyetupa. Hatuachi kuzaa matunda, hata kama hatutapoteza WOKOVU wetu.

Mwenendo mwema ni asili yetu.

Tunamtazama Kristo na kumdhahirisha.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

# 12

SURA YA

***NA HUO UTAKATIFU, AMBAO HAPANA MTU  
ATAKAYEMWONA BWANA ASIPOKUWA NAO***



**K**atika sehemu zilizopita nimeandika uchambuzi wa kimaandiko kuhusiana na uhakika wa wokovu na kuweka maelezo baadhi ya mistari kwenye Biblia yanayotumika kuonyesha kuwa wokovu siyo wa milele au mwamini hana uhakika na msamaha wa dhambi au kuhesabiwa haki na mambo kama hayo. Hapa nataka tupitie tena kitabu cha Waraka kwa **Waibrania 12:14**

**[14] Tafuteni kwa bidii kuwa na amani na watu wote, na huo utakatifu, ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao.**

Wazo linalokuja kwenye ufahamu mara nyingi kama haujasoma kwa muktadha au kutumia kanuni za kiuchambuzi wa maandiko na kuishia kusema HAIWEZEKANI SISI KUMWONA MUNGU (BAADAYE) KAMA HATUTAISHI NA AMANI NA WATU WOTE NA KUWA WATAKATIFU. Tunaweza kuongezea na maneno kama "NDUGU TUJITAHIDI KUISHI MAISHA MATAKATIFU ILI TUMWONE MUNGU" na maneno mengine kama hayo.

Sasa twende hatua kwa hatua... HAPANA MTU ATAKAYEMWONA BWANA ASIPOKUWA NAO. Huyu ni mtu gani?

Maana MWAMINI hatafuti kumwona Mungu, hili kwake limekamilika. Yeye ni makao ya Mungu. Mungu anakaa ndani yake. Mungu amemtafuta kwa njia ya Yesu Kristo na amepatikana. Yuko salama.

Shida ya watu wengi wakisoma Biblia na mrengo wa "ubaadaye" yaani mwisho wa dunia wanajikuta wakilazimika kulazimisha maandiko yaseme kile ambacho hayakusema.

Sasa tuangalie, Mwandishi wa kitabu cha Waraka kwa Waembrania anasemaje kuhusu UTAKATIFU? Je, ni jambo la kujitahidi kutafuta?

**Angalia *Waembrania 2:11***

**[11] Maana yeye atakasaye na hao wanaotakaswa wote pia watoka kwa mmoja. Kwa ajili hii haoni haya kuwaita ndugu zake;**

ATAKASAYE NA WANAOTAKASWA. Hakuna wanaojitakasa. Angalia na **Waebrania 10:10**

**[10] Katika mapenzi hayo mmepata utakaso, kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja tu.**

Mapenzi ya Mungu ni kutolewa kwa mwili wa Yesu Kristo... kwa mauti yake TUMEPATA. Yaani ni jambo la kupokea na kumiliki.

Anarudia tena kwenye sura ya 10, **Waebrania 10:14**

**[14]Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa.**

WANAOTAKASWA...

Turudi nyuma kwenye **Waebrania 9:13-14**

**[13]Kwa maana, ikiwa damu ya mbuzi na mafahali na majivu ya ndama ya ng'ombe waliyonuyiziba wenye uchafu hutakasa hata kuusafisha mwili;**

**[14]basi si zaidi damu yake Kristo, ambaye kwamba kwa Roho wa milele alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na mawaa, itawasafisha dhamiri zenu na matendo mafu, mpare kumwabudu Mungu aliye hai?**

Inatakasa zaidi ya mafahali na majivu ya ng'ombe... yenyewe haiachi kumbukumbu ya dhambi. Elewa hilo.

**Kumbuka:** Natumia neno KUTAKASWA kwa sababu ni kitenzi cha UTAKATIFU. UTAKATIFU ni hali. Kitendo ni kutakasa au KUTAKASWA. Ni sawa tukisema MWAMINI ametakaswa. Angalia Paulo anavyowaita waamini walioko Korintho, *1 Wakorintho 1:2*

*[2]kwa kanisa la Mungu lililoko Korintho, wale WALIOTAKASWA katika Kristo Yesu, walioitwa wawe WATAKATIFU, pamoja na wote wanaoliitia jina la Bwana wetu Yesu Kristo kila mahali, Bwana wao na wetu.*

Syo kwamba hawa ndugu hawakuwa na shida au changamoto za kitabia.. walikuwa nazo ila anajua UTAKATIFU ni asili yao katika Kristo na ni kazi ya Ukombozi wa Yesu Kristo ndani yao.

Wito wa Mungu ndani ya Kristo ni kufanywa Mtakatifu. Angalia shida ya baadhi ya waamini walioko Korintho kwenye *1 Wakorintho 5:1*

*[1]Yakini habari imeenea ya kuwa kwenu kuna zinaa, na zinaa ya namna isiyokuwako hata katika Mataifa, kwamba mtu awe na mke wa babaye.*

Lakini bado hakusema baadhi yenu si WATAKATIFU aliwatambulisha kama WATAKATIFU. Utakatifu ni utambulisho wa Mwamini.. siyo jambo analotafuta ili apate.

Angalia Paulo kwa *Waefeso 1:1*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

**[1]Paulo, mtume wa Kristo Yesu, kwa mapenzi ya Mungu; kwa watakatifu walioko [Efeso] wanaomwamini Kristo Yesu.**

Sio kwamba hawa ndugu walikuwa na mwenendo mzuri kwenye kila kitu.

Angalia anavyowaonya *Waefeso 4:28*

**[28]Mwibaji asiibe tena; bali afadhali afanye juhudhi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe, apate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji.**

Inawezekana hili kanisa lilikuwa na watu wana shida ya wizi.. lakini hajaanza kwa kuwaita wachafu, najisi au wasiotakaswa.

Sasa mwandishi wa kitabu cha Waraka kwa Waebrania alimaanisha nini?

"TAFUTENI KWA BIDII" neno TAFUTENI ni kitenzi au kitendo au kufanya jambo. Kwenye KJV Wametumia "FOLLOW" ***Heb 12:14 KJV Follow peace with all men, and holiness, without which no man shall see the Lord:*** Follow ni kufuata njia au jambo lililopo tayari. Halitumiki kumaanisha kukisaka kitu ambacho hakiko. Hapo ndipo Kiswahili kilivyo na shida.

Neno la Kigiriki ni *diōkō* lenye maana ya kufuata.. "pursue" .. uchaguzi wa kutumia "pursue" ni sawa zaidi ya "seek" kwa sababu ya chanzo cha UTAKATIFU ambaao tumeshajifunza hapo juu.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Hili neno limetumika pia kwenye ***1Co 14:1 KJV Follow after charity, and desire spiritual gifts, but rather that ye may prophesy.***

FOLLOW AFTER charity (love)... Following what you have already received.

SUV wametumia ***1 Wakorintho 14:1***

***[1]UFUATENI UPENDO, na kutaka sana karama za rohoni, lakini zaidi kwamba mpare kuhutubu.***

Huku kufuata ni kutenda kazi (practice) upendo.. kwa sababu wanao tayari.

Angalia ***Wagalatia 5:22***

***[22]Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu***

Tunda la Roho ni UPENDO. Ni tunda si mzizi. Ni matokeo ya kuwa na Roho Mtakatifu ndani yao.

Angalia pia ***Warumi 5:5***

***[5]na tumaini halitahayarishi; kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi.***

LIMEKWISHA KUMIMINWA.. namna gani? Kwa Mungu kutupenda kwanza...

Angalia ***1 Yohana 4:19***

***[19]Sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza.***

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Mungu alitupendaje kwanza? Yesu anamweleza Nikodemo *Yohana 3:16*

*[16]Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*

Paulo alisisitiza huo upendo wa Mungu kwetu kwenye *Warumi 5:8*

*[8]Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenyenye dhambi.*

Kwa hiyo, TUNAWEZA KUUFTA UPENDO KWA SABABU TUNAO NA UTAKATIFU PIA. Yaani tunaweza kuenenda kwa namna ambayo huo upendo au huo UTAKATIFU ukaonekana katika matendo yetu.

Neno lingine hapa ni "AMANI" *Warumi 5:1*

*[1]Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na mwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo,*

KJV wameweka hivi "WE HAVE PEACE WITH GOD" Paulo akaendelea mbele kuelezea upendo wa Mungu. Kwa sababu tunao upendo tunaweza KUDHIHIRISHA kwa kuwapenda wengine.

Vivyo hivyo na amani pia... angalia *Warumi 12:17-18*

*[17]Msimlime mtu ovu kwa ovu. Angalieni yaliyo mema machoni pa watu wote.*

*[18]Kama yamkini, kwa upande wenu, mkae katika amani na watu wote.*

Na yamkini kwa upande wenu kwa sababu kukaa na amani na watu haina maana watataka kuwa na amani na wewe. Lakini kwa upande wako fanya sawa sawa na asili yako.

Mkae katika amani na watu wote.

Ndiyo maana akawaambia kwenye **1 Wathesalonike 5:14-15**

*[14]Ndugu, twawasihi, waonyeni wale wasiokaa kwa utaratibu; watieni moyo walio dhaifu; watieni nguvu wanyonge; vumilieni na watu wote.*

*[15]Angalieni mtu awaye yote asimlipe mwensiwe mabaya kwa mabaya; bali siku zote lifuateni lililo jema, ninyi kwa ninyi na kwa watu wote.*

NA HUO UTAKATIFU... neno na pale (**Hapa neno pale umelitumia badala ya ...?** ni neno la Kigiriki "kai" ambalo mara nyingi linatumika kama kielezi, tofauti na "de" ambayo huunganisha vitu viwili tofauti. Amani na Utakatifu si vitu viwili tofauti. Badala ya kuweka **NA** tunaweza kuweka neno "ambao, ambacho au ambalo".

Mpaka hapa tunaweza kusema Mwandishi wa kitabu cha Waraka kwa Waembrania alimaanisha "**TEMBEA KATIKA MWENENDO WAKO WA AMANI AMBAO NI UTAKATIFU KATIKATI YA WATU WOTE**"

Ili iweje?

Tuangalie maneno mengine: HAPANA MTU ATAKAYEMWONA BWANA ASIPOKUWA NAO... KJV wameandika WITHOUT WHICH NO MAN MAN

SHALL SEE THE LORD.. kwa kutafsiri moja kwa moja kwenda Kiswahili kutoka KJV ningeandika.. PASIPO HUO HAKUNA MTU ATAMWONA BWANA.

Tumeshaweka sawa kuwa MWAMINI ni makao ya Mungu, hatafuti kumwona Bwana.

Wanaotafuta kumwona Bwana ni nani? Jibu ni WASIOAMINI. Watamwonea wapi? Kwenye mwenendo wa WAAMINI. Mungu anajidhihirisha kwa wasioamini kupitia watoto wake.

### ***Waefeso 5:1***

***[1] Hivyo mfuateni Mungu, kama watoto wanaopenewa.***

Ujuzi tunaopata juu ya Baba hutufundisha namna ya kuenenda kama yeye na wale wasioamini huwaona wanaomini wakimwakisi Baba yao. Tunapodhihirisha huu upendo wa Baba yetu, tunaishi kwa amani (amani ni tabia ya upendo) huu ni utakatifu wetu katika matendo.

**Kumbuka:** Utakatifu ni hali ya kutengwa, Mungu ametutenga tuwe makao yake. Mungu ni pendo na upendo wake uko ndani yetu na tunaweza kuzaa matunda kwa KUDHIHIRISHA huo upendo ambao ni UTAKATIFU wetu. Ikiwa tumetengwa, tumefanyika hekalu lake na hekalu la Mungu ni takatifu, (katufanya WATAKATIFU), tunaweza kuwa na amani na watu wote hata kama hawatataka kuwa na amani na sisi.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Basi Waraka kwa Waebrania 12:14 kwa maelezo haya  
ingesomeka hivi "KWA BIDII MUWE NA AMANI NA  
WATU WOTE, AMBAO NI UTAKATIFU WENU  
MAANA PASIPO HUO DATU HAWAWEZI  
KUMWONA BWANA"

Huu ni mwenendo wa WATAKATIFU.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

# 13

SURA YA

***HALI YAO YA MWISHO IMEKUWA MBAYA  
KULIKO ILE YA KWANZA***



**K**atika sehemu hii nataka tuangalie mjadala kunaozuka mara nyingi kuhusiana na hatima ya wokovu kwa kutumia **2 Petro 2:20-22**

**[20] Kwa maana wale waliokwisha kuyakimbia machafu ya dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo, kama wakinaswa tena na kushindwa, hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya kwanza.**

**[21] Maana ingekuwa heri kwao kama wasingalijua njia ya haki, kuliko kuijua, kisha kuiacha ile amri takatifu waliyopewa.**

**[22]Lakini imetukia kwao sawasawa na ile mithali ya kweli, Mbwa ameyarudia matapiko yake mwenyewe, na nguruwe aliyeoshwa amerudi kugaa-gaa matopeni.**

Kwa sababu ya kutofanya uchambuzi yakinifu 'study' watu wengi huishia kunukuu tu mistari hii kama wanavyonukuu mistari mingine na kutafsiri namna wanavyowaza na siyo kutafuta kuja lengo au nia ya mwandishi kuweka habari hii katika waraka wake.

Kuweka sawa hili ni vyema tukajua kuwa Petro alichukua habari hii kwenye kitabu cha ***Mithali 26:11***

**[11] Kama vile mbwa arudiavyo matapiko yake; Kadhalika mpumbavu afanya upumbavu tena.**

Watu ambao Petro anawaandikia waraka huu wanapatikana mwanzoni kabisa mwa waraka.

### **Angalia 2 Petro 1:1**

**[1] Simoni Petro, mtumwa na mtume wa Yesu Kristo, kwa wale waliopata imani moja na sisi, yenye thamani, katika hali ya Mungu wetu, na Mwokozi Yesu Kristo.**

Wale waliopata IMANI moja na sisi. Hawa ni waamini kabisa. Lakini pia mazingira ya watu hawa anaowaandikia wanajua matumizi ya lugha za mifano

(kufananisha vitu) kama alivyotumia mbwa na nguruwe. Nguruwe na mbwa ni wanyama ambayo kwa sheria za Musa na utamaduni wa Wayahudi ni najisi. Na mara nyingi walitumika kufananisha na mataifa. Mataifa (gentiles) ni namna Wayahudi wanavyowaita watu wasiyo Wayahudi.

Angalia ***Mathayo 7:6***

*[6] Msiwape mbwa kilicho kitakatifu, wala msitupe lulu zenu mbele ya nguruwe, wasije wakazikanyaga chini ya miguu yao, wakageuka na kuwararua.*

MBWA NA NGURUWE WAMETUMIKA PAMOJA.

Angalia hapa ***Mathayo 15:22-28***

*[22]Na tazama, mwanamke Mkananayo wa mipaka ile akatokea, akampazia sauti akisema, Unirehemu, Bwana, Mwana wa Daudi; binti yangu amepagawa sana na pepo.*

*[23]Wala ye ye hakumjibu neno. Nao wanafunzi wake wakamwendea, wakamwomba, wakisema, Mwache aende zake; kwa maana anapiga kelele nyuma yetu.*

*[24]Akajibu, akasema, Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli.*

*[25]Naye akaja akamsujudia, akisema Bwana, unisaidie.*

[26] *Akajibu, akasema, Si vema kikitwaa chakula cha watoto na kuwatupia mbwa.*

[27] *Akasema, Ndiyo, Bwana, lakini hata mbwa hula makombo yaangukayo mezani pa bwana zao.*

[28] *Ndipo Yesu akajibu, akamwambia, Mama, imani yako ni kubwa; na iwe kwako kama utakavyo. Akapona binti yake tangu saa ile.*

Mwanamke Mkananayo (asiye Myahudi). Anaitwa mbwa. Hii ni lugha ya kawaida kuonyesha kuwa si Myahudi.

Paulo pia anasema **Wafilipi 3:2**

[2] *Jihadharini na mbwa, jihadharini na watendao mabaya, jihadharini na wajikatao.*

HAWA PIA NI DATU.

Kwenye **Mathayo 7:6** Yesu aliwaita mafarisayo mbwa. Paulo kwenye **Wafilipi 3:2** anawaita watu wa tohara mbwa. Hawa wanawalazimisha waamini wafuate sheria za Musa. Kwa hiyo "Mbwa na Nguruwe" wanaweza kutumika mazingira tofauti yakionyesha aina mbalimbali za watu. Kwa lugha rahisi waandishi wanaweza kutumia wanyama wenye tabia fulani kuelezea tabia fulani za watu.

Nguruwe: Kugaa-gaa matopeni baada ya kuoshwa.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Mbwa: Kurudia matapiko yake.

Hizi zote mbili ni tabia za ajabu sana kwa wanadamu lakini ni kawaida au asili ya wanyama hao. Ukisoma kwa makini kuanzia mwanzo wa sura ya 1 Petro anaelezea juu ya imani mstari wa 1 hadi 19. Mstari wa 20 utaanza kuona Petro akiendeleza shida iliyopo kwenye tafsiri ya maandiko(unabii).

Angalia 2 **Petro 1:20-21**

*[20]Mkijua neno hili kwanza, ya kwamba hakuna unabii katika maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu.*

*[21]Maana unabii haukuletwu po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinenya yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.*

Kwa hiyo unabii unaweza kufasiri vibaya KAMA APENDAVYO MTU na hiyo ndiyo namna isiyotakiwa. Anaanza sura ya pili kwa kusema ni nani wanaofanya kazi hiyo ya kufasiri unabii wa maandiko vibaya,

Angalia 2 **Petro 2:1**

*[1] Lakini kuliondokea manabii wa uongo katika wale watu, kama vile kwenu kutakavyokuwako waalimu wa uongo,*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

*watakaoingiza kwa werevu uzushi wa kupoteza,  
wakimkana hata Bwana aliyewanunua,  
wakijiletea uharibifu usiokawia.*

Anawaita MANABII WA UONGO NA WAALIMU WA UONGO.

Kuanzia hapo na kuendelea na sura ya pili yote anawaonya juu ya watu hawa. Hawa ndiyo watu Petro anawaita NGURUWE NA MBWA. Kumbuka huu ni waraka kwa kanisa, anawaonya juu ya watu ambao watakuwa katikati yao kama wenzao. Lengo lao siyo Bwana Yesu Kristo bali kuwahadaa waaamini kwa ajili ya mapato yao au ujisadi wao.

Petro anawaelezea 2 *Petro 2:18-19*

*[18]Maana wakinena maneno makuu mno ya kiburi, kwa tamaa za mwili na kwa ujisadi huwahadaa watu walioanza kuwakimbia wale wanaoenenda katika udanganyifu;*

*[19]wakiwaahidia uhuru, nao wenyewe ni watumwa wa uharibifu, maana mtu akishindwa na mtu huwa mtumwa wa mtu yule.*

Ndipo Mstari wa 20 unasema 2 *Petro 2:20*

*[20]Kwa maana wale waliokwisha kuyakimbia machafu ya dunia kwa kumjua Bwana na*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

***Mwokozi Yesu Kristo, kama wakinaswa tena na kushindwa, hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya kwanza.***

Hii ina maana hawa watu wameelezwa Injili lakini wao hawakuwa na nia ya injili. Angalia 2 **Petro 2:21**

***[21]Maana ingekuwa heri kwao kama wasingalijua njia ya haki, kuliko kuijua, kisha kuiacha ile amri takatifu waliyopewa.***

Wameijua na kuiacha. Wakaendelea kufundisha mapotofu. Anamalizia kwa kusema 2 **Petro 2:22**

***[22]Lakini imetukia kwao sawasawa na ile mithali ya kweli, Mbwa ameyarudia matapiko yake mwenyewe, na nguruwe aliyeoshwa amerudi kugaa-gaa matopeni.***

Kwa hiyo hawa ni manabii wa uongo na walimu wa uongo, watu wafundishao mapotofu kwa ajili ya ufisadi na faida yao wenyewe. Hawa siyo waamini walipoanguka katika dhambi kama ambavyo mara nyingi imekuwa ikichukuliwa.

Haina maana ya mwamini aliyeachach kuvuta sigara akarudi kuvuta sigara au aliyeachach pombe akarudi kulewa na mambo yanayofanana na hayo. Ijapokuwa kurudi kufanya mambo uliyoyaachach baada ya

kumwamini Yesu Kristo siyo jambo zuri LAKINI Petro hakumaanisha hivyo.

Ningemaliza kwa kusema nguruwe na mbwa ni vitu najisi kulingana na sheria ya Musa ambayo ambayo tafsiri yake ni wasioamini. Petro kwenye maono alikataa kula vitu alivyoonyeshwa akaviita najisi ikiwa na mataifa yaani Kornelio na familia yake.

*Matendo ya Mitume 10:9-17*

*[9] Hata siku ya pili, walipokuwa wakisafiri na kuukaribia mji, Petro alipanda juu darini, kwenda kuomba, yapata saa sita ya mchana;*

*[10] akaumwa na njaa sana, akataka kula; lakini walipokuwa wakiandaa, roho yake ikazimia,*

*[11]akaona mbingu zimefunuka, na chombo kikishuka kama nguo kubwa, inatelemshwa kwa pembe zake nne hata nchi;*

*[12]ambayo ndani yake walikuwamo aina zote za wanyama wenye miguu minne, na hao watambaa, na ndege wa angani.*

*[13]Kisha sauti ikamjia, kusema, Ondoka, Petro, uchinje ule.*

*[14]Lakini Petro akasema, Hasha, Bwana, kwa maana sijakula kamwe kitu kilicho kichafu au najisi.*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

*[15]Sauti ikamjia mara ya pili, ikimwambia,  
Vilivytakaswa na Mungu, usiviite wewe najisi.*

*[16]Jambo hili likatendeka mara tatu; kisha kile  
chombo kikapokewa tena mbinguni.*

*[17]Hata Petro alipokuwa akiona shaka ndani  
ya nafsi yake, maana yake ni nini maono hayo  
aliyoyaona, wale watu waliotumwa na Kornelio,  
wakiisha kuiulizia nyumba ya Simoni,  
wakasimama mbele ya mlango.*

Sasa unaweza kuelewa Petro alijua alichokuwa anaandika. Angalia *Matendo ya Mitume 10:28*

*[28]Akawaambia, Ninyi mnajua ya kuwa si  
halali mtu aliye Myahudi ashikamane na mtu  
aliye wa taifa lingine wala kumwendea, lakini  
Mungu amenionya, nisimwite mtu awaye yote  
mchafu wala najisi.*

Paulo wakati anaelezea kwamba mwamini asioane na asieamini.. ananukuu maneno ya Musa na kusema 2 *Wakorintho 6:14-17*

*[14]Msifungiwe nira pamoja na wasioamini,  
kwa jinsi isivyo sawasawa; kwa maana pana  
urafiki gani kati ya haki na uasi? Tena pana  
shirika gani kati ya nuru na giza?*

*[15]Tena pana ulinganifu gani kati ya Kristo na  
Beliali?*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

*Au yeye aaminiye ana sehemu gani pamoja na  
yeye asiyeamini?*

*[16]Tena pana mapatano gani kati ya hekalu la  
Mungu na sanamu? Kwa maana sisi tu hekalu  
la Mungu aliye hai; kama Mungu alivyosema,  
ya kwamba, Nitakaa ndani yao, na kati yao  
nitatembea, nami nitakuwa Mungu wao, nao  
watakuwa watu wangu.*

*[17]Kwa hiyo,  
Tokeni kati yao,  
Mkatengwe nao, asema Bwana,  
Msiguse kitu kilicho kichafu,  
Nami nitawakaribisha.*

SANAMU/BELIARI/GIZA/KITU KICHAFU ni MTU ASIYEAMINI.

Kuwafananisha hawa manabii wa uongo na walimu wa uongo na vitu najisi ni dhahiri ya kuwa hawakuwa waamini. Nimalize na *Mithali 26:11*

*[11]Kama vile mbwa arudiavyo matapiko yake;  
Kadhalika mpumbavu afanya upumbavu tena.*

MPUMBAVU AFANYA UPUMBAVU TENA.

Hakuwahi kuwa mwenye hekima. Yuko kwenye asili yake. Mbwa kurudia matapiko yake ni asili yake. Nguruwe kugaa-gaa matopeni ni ulimwengu wake. Hali

yao inakuwa mbaya, maana baada ya kuelezwu njia ya kweli bado waliendelea katika ubaya. Angalia mfano alioutumia wa Balaamu. Huyu nabii alionywa mara nyingi asilaani lakini akaendelea mbele hadi pundu akaamua kuongea.

### Angalia 2 **Petro 2:15-16**

*[15]wakiicha njia iliyonyoka, wakapotea,  
wakiifuata njia ya Balaamu, mwana wa Beori,  
aliyependa ujira wa udhalimu;  
[16]lakini alikaripiwa kwa uhalifu wake  
mwenyewe; pundu, asiyeweza kusema, akinena  
kwa sauti ya kibinadamu, aliuzuia wazimu wa  
nabii yule.*

Hii utaona kwenye kitabu cha Hesabu sura ya 22 hadi sura ya 24. Pamoja na Balaamu kuongeleshwa na pundu bado aliendelea kutafuta namna ya kulaani.

Kwa hiyo HALI YAO YA MWISHO KUWA MBAYA KULIKO HALI YAO YA KWANZA maana yake.. KWANZA WANA HALI MBAYA hawakuwahi kuwa na hali nzuri.. lakini wanavyoendelea kufanya ufisadi wao na kufundisha mapotofu ndivyo wanaharibika zaidi. Haina maana ile wengi wanafikiri kuwa wameokoka akiwa mlevi wa bia 10 akirudi nyuma nakuwa mlevi wa bia 40. Hii sicho alichandika Petro.

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

# 14

SURA YA

***YANIPASA NIFANYE NINI NIPATE KUOKOKA?***



**B**aada ya kumaliza maelezo kuhusu mwokozi, jinsi alivyookoa na matokeo ya wokovu hebu tuangalie chanzo cha swali hili *Yanipasa nifanye nini nipate KUOKOKA?*

Baada ya Paulo na Sila kuhubiri Injili kisha watu wakafanya ghasia iliyopelekea kupigwa na kutupwa gerezani.. mambo yaliyoendelea huko gerezani ndiyo chanzo hasa cha swali hilo hapo juu.

Ukisoma ***Matendo ya Mitume 16:25-30***

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

[25] *Lakini panapo usiku wa manane Paulo na Sila walikuwa wakimwomba Mungu na kumwimbia nyimbo za kumsifu, na wafungwa wengine walikuwa wakiwasikiliza.*

[26] *Ghafula pakawa tetemeko kuu la nchi, hata misingi ya gereza ikatikisika, na mara hiyo milango ikafunguka, vifungo vyta wote vikalegezwa.*

[27] *Yule mlinzi wa gereza akaamka, naye alipoona ya kuwa milango ya gereza imefunguka, alifuta upanga, akataka kujiua, akidhani ya kuwa wafungwa wamekimbia.*

[28] *Ila Paulo akapaza sauti yake kwa nguvu, akisema, Usijidhuru, kwa maana sisi sote tupo hapa.*

[29] *Akataka taa ziletwe, akarukia ndani, akitetemeka kwa hofu, akawaangukia Paulo na Sila;*

[30] *kisha akawaleta nje akasema, Bwana zangu, yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Angalia swalii alilouliza na jibu walilotoa kwenye  
**Matendo ya Mitume 16:31**

[31] *Wakamwambia, Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako.*

Jibu rahisi kabisa. **MWAMINI BWANA YESU NAWE UTAOKOKA.**

Ukisoma kwa haraka unaweza kufikiri mtu akiokoka basi na nyumba yake wote watakuwa wameokoka. Lakini maelezo yanayofuata yanaonyesha hiyo nyumba yake itaokokaje.. maana hakuna mtu anayeweza kuamini nafasi ya mwingine. Huyo mwingine lazima naye aaminili aokoke.

*Angalia Matendo ya Mitume 16:32*

*[32]Wakamwambia neno la Bwana, yeye na watu wote waliomo nyumbani mwake.*

Hii ina maana Luka aliandika mstari wa 31 akiwa na ufahamu wa tukio la mstari wa 32. Mistari inayofuata ni ya msingi sana.

*Matendo ya Mitume 16:33*

*[33]Akawakaribisha saa ile ile ya usiku, akawaosha mapigo yao, kisha akabatizwa, yeye na watu wake wote wakati uo huo.*

Aliamua kuwakaribisha usiku na kuwashudumia nyumbani mwake. Angalia mstari unaofuata..

*Matendo ya Mitume 16:34*

*[34]Akawaleta juu nyumbani kwake, akawaandalia chakula, akafurahi sana, yeye na*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

***nyumba yake yote, maana amekwisha kumwamini Mungu.***

MAANA AMEKWISHA KUMWAMINI MUNGU. Alimwaminije Mungu? Kwa kumwamini Bwana Yesu kama mwokozi. Kumbuka maneno haya "MWAMINI BWANA YESU NAWE UTAOKOKA". Yesu ni Bwana aokoaye au Yesu ni Bwana na Mwokozi.

Yesu aliulizwa swalii muhimu sana ambalo ni vyema hata wewe ujiulize ili ujue Mungu anataka nini kwako baada ya kusoma kitabu hiki. Kwenye *Yohana 6:28*

***[28]Basi wakamwambia, Tufanyeje ili tupate kuzitenda kazi za Mungu?***

Majibu ya Yesu yalikuwa marahisi tu. Kwenye kitabu *Injili ya Yohana 6:29*

***[29]Yesu akajibu, akawaambia, Hii ndiyo kazi ya Mungu, mmwamini yeye aliyetumwa na yeye.***

Hii ndiyo kazi ya Mungu na huku ndiko kumfurahisha Mungu. Kumwamini Bwana Yesu kama mwokozi wako, aliyeokuoaa katika dhambi, akakupa Roho wake hivyo una uzima wa milele kwa sababu unaye Roho wa Mungu wa milele ndani yako. Unaо msamaha wa dhambi yaani umehesabiwa haki na Mungu mwenyewe, hakuna wa kukuhesabia kuwa na hatia, Mungu anakutazama kama

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

mwanaye mpendwa kwa sababu ya tendo moja tu  
KUMWAMINI YULE ALIYEMTU yaani YESU  
KRISTO BWANA WETU.

## **UMEBARIKIWA.**

**ଶ୍ରୀ**

**ଜୀବନ**

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*



**Vitabu vingine vya mafundisho ya Neno la Mungu  
vilivyoandikwa na Shemeji Melayeki**

1. *Ukombozi Reloaded*
2. *Kufunga Reloaded*
3. *Kabla Ya Kuomba*
4. *Moyo wa Baba*
5. *Akaanza Kutoka Musa*
6. *Kiumbe Kipyta*



*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Shemeji Melayeki ni muasisi wa huduma ya Global Family Gatherings Ministries na mnenaji katika makongamano mbalimbali. Yeye, mke wake na watoto wanaishi jijini Dar es Salaam. Kwa maombi au ushauri tumia anuani zifuatazo.

Email: *shemeji.melayeki@gmail.com*

Instagram: *apostleshemejimelayeki*

Facebook: *Apostle Shemeji Melayeki*

YouTube: *Ap Shemeji Melayeki*

Twitter: *@melayeki*

*Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?*

Kufika kwenye ibada zetu na kambi za mafundisho ya neno la Mungu tumia simu +255 714 548 565.

Unaweza kujiunga na vikundi vyta mafundisho kwa njia ya mitandao kwa namba hiyo hiyo.

Ukitaka kuwa sehemu ya watu wanaowekeza fedha zao katika kutusaidia kufika injili kwa watu wengine kwa njia ya maandishi na redio tumia +255 763 965 297.

Ku download application yenyet mafundisho:

<https://play.google.com/store/apps/details?id=com.melayeki>

Kuingia                    katika                    Website                    yetu:

<http://globalfamilygatherings.co.tz>

Kuingia channel ya telegram: <https://t.me/apostleshemeji>

Kuingia Youtube channel:

<https://youtube.com/c/shemejimelayeki>

Facebook page: <https://facebook.com/ShemejiMelayeki>

Whatsapp:

<https://chat.whatsapp.com/JXzsoD5qHIFADN9LdW5Xzo>

## **UMEBARIKIWA!**